**10 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Tatu– Tarehe 10 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 297

### Marekebisho ya Kanuni ya Kikokotoo cha Mafao ya Wastaafu

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Kanuni ya Kikokotoo ili kuongeza kiwango cha mafao ya mkupuo kwa wastaafu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao ikijumuisha malipo ya mkupuo kwa wastaafu. Sheria inaitaka mifuko kufanya tathimini ya kupima uhimilivu kila baada ya miaka mitatu na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ikiwemo maboresho ya mafao ya wanachama ambapo kanuni mpya imeanza kutumika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni muhimu kuzingatia ushauri wa wataalam kuhusu uendeshaji, usimamizi na uendelevu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwa unazingatia utaalamu wa sayansi ya watakwimu-bima *(actuarial science)*. Aidha, uamuzi wa

kubadilisha Kanuni ya Kikokotoo cha Mafao ya Wastaafu ni lazima utokane na tathmini ya kina ya kisayansi ya watakwimu-bima kama ilivyoelezwa na Makamu wa Rais katika sherehe za Mei Mosi mwaka huu 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nashukuru pia kwa majibu ya Serikali ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inalipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuiongezea ukwasi mifuko hiyo ili iendelee kuwanufaisha wanachama wake? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda sana wafanyakazi na inaamini wafanyakazi ndio chachu ya kuleta maendeleo katika Taifa letu na kujenga uchumi. Kwa kuzingatia hilo iliweza kukuta kunakuwa kuna madeni ambayo yalikuwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mojawapo ilikuwa Mfuko wa *PSSSF* ambayo iliridhi deni la mwaka 1999 kabla ya hapo wanachama wa *PSPF* walikuwa hawachangii fedha, lakini Serikali ilikuwa inatoa fedha na mfumo ulivyokuja kubadilika maana yake walilazimika kuwa wanachangia fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kwa kuwapenda wafanyakazi hawa iliamua kubeba deni hilo na iliendelea kuwalipa wastaafu hawa fedha na kulikuwa kuna deni la shilingi bilioni 4.6 ambazo tayari Serikali imekwishakulipa shilingi bilioni

2.176 kwa kupitia hati fungani, hili ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pili katika hatua hiyo katika upande wa Mfuko wa *NSSF* tayari kulikuwa kuna deni la shilingi bilioni 430 ambalo tayari jana wamekwisha kufanya kikao na katika kikao hicho Katibu Mkuu wa Hazina amekwishasaini kwamba fedha hizo zitaenda kulipwa ili kuweza kuongeza nguvu katika mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inaimarisha mifuko hii na kuangalia maslahi ya wafanyakazi ambao wamestaafu na kulitumikia Taifa kwa uhodari mkubwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali kwa kifupi.

**MHE. SOPHA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, japokuwa sheria hii tulipitisha hapa Bungeni, sasa Serikali haioni haja ya kuleta marekebisho ya kikokotoo ili wafanyakazi waweze kulipwa mafao yao yote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda Bunge lilipitisha sheria, Serikali imetengeneza kanuni, hiyo kanuni siyo sisi tumetengeneza hapa ndani, sasa uliza swali lako upya.

**MHE. SOPHA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Waziri hauoni haja sasa kanuni hiyo ikarekebishwa ili wafanyakazi wetu waweze kulipwa mafao kwa kazi waliofanyia kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda kuwa ni kwamba kweli Serikali tayari imekwishaanza kufanyia kazi utaratibu wa kuweza kufanya

*actuarial evaluation* ili iweze kuangalia namna gani inaweza kunufaisha zaidi wastaafu wetu hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali kwa kifupi.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, wapo wastaafu ambao walikuwa kwenye mfuko wa zamani wa *NPF,* baada ya kuanzishwa *PSSSF* na *NSSF* mafao yao yalihamishwa kwenda kwenye mifuko mipya, lakini wana madai ya miaka mingi mpaka leo wanazungushwa hawajalipwa; nini kauli ya Serikali kwa wastaafu hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hapa *to be specific* kwa upande wa Serikali, labda nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge aniletee taarifa ya hao watumishi ambao wanalalamika, kwa sababu rekodi zetu zinatuonesha madeni yaliyorithiwa na *PSSSF* pia na *NSSF* baada ya mabadiliko ya kuunganisha mifuko mwaka 2018, zaidi ya asilimia 78 wamelipwa na wengine malipo yao yanaendelea kufanyiwa uhakiki kuweza kuhakikisha kwamba wanalipwa.

Kwa hiyo, hakuna sehemu kubwa ya malalamiko ya watu ambao walionesha kwamba takwimu zao zilikuwa sahihi na ufasaha wa nyaraka, wote wamekwishakulipwa labda kama kuna hiyo changamoto *specific* nitafurahi Mheshimiwa Mbunge akinipatia ili niweze kwenda kufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri yule amezungumza kuhusu mafao ya wale ambao ni wa kitambo na wamedai muda mrefu. Kuna hao wanaostaafu sasa hivi, anasubiri miezi mitatu, minne, sita mpaka mwaka kwa sababu inakuwa inajulikana anaanza kustaafu lini na lengo la mafao ni kumuweka huyu mtu mazingira ambayo alikuwa nayo hapo nyuma yasishuke. *(Makofi)*

Sasa miezi sita mtu hajapata mshahara na alikuwa anatarajia mshahara, amestaafu malipo yake hayaji anatakiwa

kufanyaje? Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wanachoka na *message* zinajaa kwenye simu zao. Kwa ujumla mmejipanga vipi kwa maana mtu anapostaafu inajulikana. Kwa nini hamjajiandaa muda wote anapostaafu aanze kulipwa hela yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ukweli tu nieleze kwa upande wa Serikali tumejipanga nalo hilo na tulishaboresha mpaka sasa hata taarifa za wafanyakazi hata wale wanapoendelea kuelekea kustaafu zinaandaliwa mapema miezi sita kabla na hatuna tena lile suala ambalo Bunge lako Tukufu liliagiza hapa na tulifanyia kazi kwamba lile suala la kuombwa mtu barua ya kuajiriwa na nini hayo yote ni zilipendwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tayari ndani ya siku 60 mtu analipwa mafao yake, labda kama kuna changamoto ambazo hazipo na kama kuna watu *specific* ambao hawajalipwa ndani ya siku 60 hata kama ni siku saba mafao yake yakiwa tayari analipwa, hatujawa na ucheleweshaji. Sasa hivi kesi za kuzidi siku 60 zimekuwa hazipo kwenye ofisi yetu na kama zipo kwa sasa labda pengine kwa taarifa za zamani, lakini kama kuna taarifa hizo naomba nipate hizo taarifa nikafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, utakuta kama kuna mtu ambaye amechelewa ndani ya siku 60 ni yule ambaye pengine kuna dosari za wazi ambazo zinaweza zikasababisha/kupelekea changamoto katika kumfanyia malipo yake, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ushauri wa jumla kama ambavyo waajiri wakichelewesha fedha, sheria inataka walipwe riba kwa yule mwajiri ambaye amechelewesha na upande wa mifuko inapomcheleweshea huyu mtu fedha zake na kwenyewe kule tuweke riba ili wawe wanawahisha, ahsante sana. Kwa hiyo, hapo tutatarajia mabadiliko ya sheria ili na wao wakibanwa hivi na wao watawahisha fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 298

**Kurejesha Fao la Kujitoa kwa Watumishi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha fao la kujitoa kwa watumishi na kupatiwa michango wanapoacha kazi bila kusubiri umri wa miaka 55 au 60?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge Wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kinga ya jamii unalenga katika kuhakikisha kuwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanapata sifa ya kulipwa pensheni badala ya michango yao. Hata hivyo, inapotokea mwanachama kuondoka kazini kabla ya umri wa kustaafu Serikali imetayarisha Kanuni za Mafao za mwaka 2023 ambazo zinamuwezesha mwanachama kupata mafao ya mkupuo maalum kulingana na sifa alizonazo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Serikali ni kuwakinga wananchi wake dhidi ya majanga kama umaskini uliokithiri, uzee, ugonjwa na kukosa kipato. Hivyo natoa rai kwa wanachama na wananchi kuwa na utamaduni wa kuendeleza uchangiaji wa mafao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanapobadilisha waajiri ili kutopoteza haki yao ya kupata pensheni pindi wanapostaafu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Mgungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kulingana na majibu ya Naibu Waziri nasema kwamba kuna wale ambao wanajitoa kabla muda wa kustaafu, kuna utaratibu maalum kwenye kanuni kwamba watalipwa mafao kwa mkupuo kulingana na sifa ambazo wanazo kwa wakati huo.

Je, ni sifa gani ambazo mtu anapaswa awe nazo kwa wakati huo ili aweze kurejeshewa fedha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hawaoni haja ya kuruhusu watu wale ambao wanaacha kazi kabla ya muda hawajafika sifa ya pensheni kwa maana miezi 180 kurejeshewa walau michango yao na michango ya mwajiri ili iweze kuwa mtaji kwa wao kujiajiri kama ambavyo tunahubiri siku zote kuhamasisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye kanuni inaeleza kuwa mwanachama ambaye pengine namna gani ambavyo anaweza akapewa mafao yake kwa mkupuo kama jinsi alivyouliza. Sifa ambazo zimeainishwa moja ni kwamba kanuni zinaeleza awe ameachishwa kazi na akiwa ameachishwa kazi katika kipindi ambacho ni cha miezi sita ataanza kulipwa fedha hizo kwa kuangalia akiwa na matarajio au matazamio kwamba anaweza akapata ajira nyingine. Ikitokea hajapata ajira ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu hapo anaweza akafanya maombi ya kuweza kupewa fao lake sasa la kujitoa.

Mheshimiwa Spika, nikijibu pamoja na swali lake la pili katika msingi huo huo kwamba hata yule ambaye amechangia kama ikitokea amechangia kwa zaidi ya miezi 180 maana yake huyu atakuwa tayari na sifa ya kuweza kupata pensheni, lakini ikiwa chini ya miezi 180 huyu anaweza akaomba kama jinsi ambavyo nimeeleza katika kipengele cha kwanza na kwenye jibu langu la msingi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali.

Na. 299

**Uhitaji wa Hosteli katika Shule za Sekondari Nchini**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga hosteli katika shule za sekondari nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kuwashirikisha wananchi kujenga na kuendesha hosteli katika shule za kutwa za kidato cha kwanza hadi cha nne katika maeneo yenye uhitaji ili kutatua changamoto za ulinzi na usalama wa wanafunzi na kupunguza umbali wa kutoka nyumbani kwenda shuleni.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa mabweni ya kidato cha tano na sita kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu kidato cha nne wanapata fursa ya kusoma elimu ya sekondari ya ngazi ya juu. Aidha, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuhamasisha wananchi kupitia mamlaka za Serikali za mitaa kujenga na kuziendesha hosteli katika shule za sekondari za kidato cha kwanza hadi cha nne.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri haya ambayo Serikali imeyatoa; nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ninataka kufahamu kwa kuwa yapo maeneo ambayo hawana kipato cha kuweza kujenga hizo hosteli na hata wakianza wanaishia njiani na Mfano mzuri uko katika Shule ya Sekondari Nakalulu, Ileje na Shule ya Sekondari Mukulu kule Halmashauri ya Momba.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kuwasaidia kupata fedha za kumalizia ujenzi wa hosteli hizi kwa sababu ni hitaji lao la msingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali ina mkakati gani wa kujenga hosteli ya shule za msingi kwa sababu yapo maeneo ambayo watoto wako katika hatari ya matendo ya ukatili na ni kitu ambacho kipo, mfano Mji wa Tunduma watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya ukatili wakiwa mashuleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kujenga mabweni na Serikali inafanya mikakati mbalimbali za kuweza kujengea halmashauri zetu uwezo ili ziweze kuwa na miradi endelevu itakayoweza kutosheleza au kuongeza uwezo wa ujenzi wa miundombinu muhimu na hasa miundombinu ya elimu kama mabweni.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala hili Serikali inalipa uzito mkubwa sana, naamini kwamba, baada ya wakati fulani miundombinu yote hii itakuja kujengwa, lakini kwa wakati huu tunazihamasiaha na tuzielekeza halmashauri ziweze kutenga bajeti kwenye mapato yao ya ndani ili ziweze kuendeleza miundombinu hii ya mabweni. Tunawahamasisha pia wananchi waweze kushirikiana na halmashauri katika ujenzi wa

hosteli kwa ajili ya wanafunzi wetu hao wa kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, ametoa ushauri wa ujenzi wa hosteli katika shule za msingi; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hayo ni mawazo umeyatoa tumeyapokea tutayachakata, tukiona yanaweza kutekelezeka hatutosita kutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 300

**Vipimo vya Viazi Mviringo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatangaza rasmi vipimo sahihi vya ununuzi na uuzaji wa viazi mviringo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali kupitia Sheria ya Vipimo sura 340 mapitio ya 2002 na marekebisho yake ya mwaka 2018 kupitia *The Weights and Measures Act (Amendment) Order, G.N. No. 725 of 2018* imetoa tangazo rasmi la vipimo sahihi vya ununuzi na uuzaji wa mazao ikiwemo viazi mviringo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma wakiwemo wakulima na wanunuzi juu ya manufaa ya kutumia vipimo sahihi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka swali hili kwenye mtego kwa sababu hivyo vipimo hajavitaja, sasa nataka kufahamu Serikali inatambua kwamba huko vijijini vipimo vinavyotumika kuuza mazao ya wakulima ni madebe, ndoo na magunia? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa kufuatilia sana kuhusiana na matumizi sahihi ya vipimo na nitumie nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu, lakini pia na wananchi wenzangu kwamba madebe, ndoo, magunia na vingine ni vifungashio, siyo vipimo, vipimo sahihi ni kutumia mizani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunahamasisha na tunaendelea kuhakikisha wananchi wote wanaelimishwa ili kuhakikisha wanapouza mazao yao kama alivyosema viazi mviringo, lakini pia na mazao mengine watumie vipimo kwa maana ya mizani na hapa tunasema kwa mfano gunia lisizidi uzito wa kilogramu 100, lakini pia hata kama unauza nusu debe au sijui basi upime kwamba ni kilo kumi, kilo ishirini, kilo tano lakini siyo debe au ndoo au gunia kama vipimo, kwa sababu hii inapelekea kumnyonya mkulima na tumeanzisha kampeni ya komesha au tokomeza lumbesa kwa sababu ndiyo njia ambazo wanazitumia wanunuzi kuwanyonya wakulima. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 301

**Hitaji la Jengo la Kisasa Kituo cha Polisi Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa katika Kituo cha Polisi Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, Kituo cha Polisi cha Mbinga ni kituo cha Daraja B na kinakidhi mahitaji ya kutoa huduma ya polisi katika eneo hilo. Kwa sasa kituo hicho ni chakavu na tathmini kwa ajili ya kubaini kiwango cha uchakavu imefanyika, ambapo kiasi cha fedha shilingi 123,776,650 zinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa kufikiria kutenga zaidi ya shilingi milioni 123 kwa ajili ya kufanya matengenezo kwa kipindi cha mwaka 2025/2026, lakini nilikuwa nataka kujua kwa nini Serikali isitenge fedha hizo katika kipindi hiki cha mwaka 2024/2025 kwa kuwa mazingira ya kufanyia kazi siyo rafiki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kituo hicho kinahudumia eneo kubwa sana katika Wilaya ya Mbinga na kina changamoto ya usafiri; Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kupeleka gari kwa ajili ya kusaidia wafanyakazi wale kufanya kazi katika mazingira mazuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeweka kwenye bajeti ya mwakani kwa sababu wakati tathmini inafanyika tayari mpangilio wa bajeti ya mwaka huu ulikuwa umeshafikia hatua za mwisho, lakini kuhusiana na suala la gari nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba magari ambayo Mheshimiwa Rais ametoa kwa ajili ya wilaya zote nchini yameendelea kufika hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni siku ya Jumamosi kwa maana ya kesho tunatarajia Mheshimiwa Makamu wa Rais wakati atakapokuja kuzindua kituo bora kabisa cha Jeshi la Polisi pale Mtumba ataendelea na zoezi la ugawaji wa magari hayo kwa wilaya ambayo safari hii tumeamua kupanga kwa zile wilaya ambazo zinachangamoto ya wafugaji na wakulima. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu inayofuata ya magari yatakapofika wilaya yake tutaipa kipaumbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 302

**Kuimarishwa kwa Mawasiliano ya Simu Pemba**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Mkoani Kusini – Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *UCSAF* ilijenga minara miwili iliyojengwa na Zantel katika Kata ya Kengeja na Mgagadu na katika Kata ya Mtangani mnara ulijengwa na Kampuni ya Simu ya Halotel.

Mheshimiwa Spika, Serikali itakwenda tena kufanya tathmini ili kujua maeneo yaliyobaki yenye changamoto na kuona iwapo minara hiyo itahitaji kuongezewa nguvu au kuna uhitaji wa ujenzi wa minara mipya na utekelezaji utafanyika kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa katika Wilaya ya Mkoani Pemba nini *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha Mkongo wa Taifa unaungwa katika wilaya hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kufuatana na mimi kwenda kuona mawasiliano na changamoto katika wilaya hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha Mkongo wa Taifa unatumika vizuri. Sisi kama Wizara tumeshafikisha pale Mkongo, sasa ni sehemu ya *ZICTIA* ambayo ni *Zanzibar ICT Infrastructure Agency* ambayo inafanya kazi kule

Zanzibar kuweza kuhakikisha inasogeza huduma kwa wananchi, lakini tutashirikiana kwa maslahi mapana ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na kuongozana na Mheshimiwa Mbunge nikutoe hofu nipo tayari na mara baada ya Bunge hili tutakwenda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano ya simu katika maeneo ya Mkoa wa Simiyu ambayo hayana minara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Simiyu ambayo hayana minara tayari kazi zinaendelea maeneo mbalimbali ya nchi na Mheshimiwa Mbunge kadiri tutakavyoendelea kupata fedha ile minara ambayo tumeielekeza maeneo haya ya Simiyu na yenyewe itapata kujengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Kichonda Wilayani Liwale ina vijiji vitatu vya Nyela, Kichonda na Ngumu na vijiji hivi vyote havina mawasiliano ya simu; je, ni lini Serikali itawapatia mawasiliano vijiji hivi vitatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kata hii uliyoitaja katika hivi vijiji vyote Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara furaha yetu ni kuona wananchi wanapata mawasiliano mazuri. Hivyo na wenyewe wapo kwenye mpango wa kuhakikisha tunakuja kuwajengea minara ya mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 303

**Ujenzi wa Daraja la Sanza – Wilaya ya Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Sanza lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya kusaini mkataba wa ujenzi wa Daraja la Sanza lenye urefu wa mita 75 na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 14.5. Inatarajiwa mkataba wa ujenzi utakuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2024. Baada ya mkataba kusainiwa kazi za ujenzi zitaanza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwa kuwa mwaka jana Mheshimiwa Rais alikuja Manyoni mwezi Oktoba na aliagiza Wizara ya Ujenzi wahakikishe wanakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi; nini kilichopelekea kuchelewa kusaini mkataba huu mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Daraja ya Sanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nini *commitment* ya Serikali kwa kuwa imechukua miezi sita kwamba kabla ya mwezi wa sita mkandarasi atakuwa ameshasaini mkataba na kazi itaanza? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema maagizo ya Mheshimiwa Rais apatikane mkandarasi na ndiyo maana tayari mkandarasi ameshapatikana. Kwa hiyo tunachofanya ni kukamilisha kwa taratibu zote ili tuweze kusaini, mkandarasi alishapatikana na *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hilo daraja tunalijenga pamoja na barabara yote ya kutoka hapa Bihawana - Sanza hadi Manyoni ambayo tunategemea baadaye itakuwa kama *bypass* ya magari badala ya kuingia Dodoma yaweze kupita Bihawana – Manyoni, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Na. 304

**Ujenzi kwa Kiwango cha Zege Barabara ya Simbo hadi Kalya – Uvinza**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE K.n.y. MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha zege kwenye maeneo korofi katika barabara ya Simbo hadi Kalya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwango cha zege kwenye maeneo korofi ya barabara ya Simbo – Ilagala – Kalya lenye urefu wa kilometa 234 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa ujenzi kwa kiwango cha zege unaendelea katika eneo la Lungonya mita 100 lililopo kilometa 102 kutoka Simbo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege katika maeneo ya Sigunga ambapo watajenga mita 100 na Kawibili itajenga mita 200 kwa kiwango cha zege, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika hiyo Barabara ya Simbo – Kalya pamoja na maeneo aliyoyataja, lakini bado yako maeneo mengine hasa maeneo ya milimani nayo yanahitaji kujengwa kwa kiwango hicho cha zege. Ni lini Serikali itajenga maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Kasulu Vijijini barabara ya kutokea Makele – Nyarugusu – Herushingo mpaka Kitanga ni mbaya haipitiki; je, ni lini Serikali itajenga maeneo haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi maeneo korofi ya Barabara ya Simbo – Kalya yataendelea kujengwa kwa awamu na tayari tumeshatenga maeneo ambayo tunaamini ni korofi zaidi kuyaanza kuyajenga, lakini tutaendelea kutafuta fedha ili yale maeneo ambayo yanaweza yakakwamisha kabisa safari, najua barabara hii sasa imefunga tutajifunza pia maeneo mengine tuweze kuongeza fedha kwa ajiili ya kujenga kwa kiwango cha zege maeneo korofi kwa hiyo utaratibu huo upo na utaendelea.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili barabara aliyoitaja ya Makele – Nyaruguswe – Mshingo kulekea Kitanga. Barabara hii ilikuwa inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*, tunachofanya sasa hivi kwanza ni kubadilisha makalavati ambayo yalikuwa yana uwezo mdogo. Kazi ambayo inaendelea na baada ya hapo ni kuibadilisha barabara kutoka kuwa ya udongo kwenda ya changarawe ambayo tayari katika mwaka huu tutafanya hiyo kazi na tunavyoongea sasa hivi mkandarasi tayari yuko anabadilisha makalavati ili kuingia kwenye viwango vya barabara za kiwango cha *TANROADS,* ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, je, lini Serikali itaanza ujenzi wa upanuzi wa Barabara ya Moshi – Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tayari mhandisi mshauri yuko *site* kwa msaada wa *JICA* ambapo tutajenga pale tulipoishia barabara ya *bypass* kilometa tisa Daraja la Kikafu, lakini pamoja na barabara za Mji wa Moshi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Samahani Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nyandekwa Manispaa ya Kahama kwenda Nyamilangano – Ushetu kipindi hiki cha mvua haipitiki; je, nini mpango wa Serikali kujenga barabara ya lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara nyingi kwa sasa zimekuwa na changamoto ya kupitika kutokana na mvua nyingi na barabara aliyotaja ni kati ya hizo barabara, lakini barabara hiyo iko kwenye mpango wa kuijenga yote kwa kiwango cha lami na tumeanza pale Mjini Nyamilangano na katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kuendelea kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, swali lake litaulizwa na kwa niaba yake na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

Na. 305

**Kuwalipia Gharama za Matibabu Wanafunzi**

**MHE. MARGARET S. SITTA K.n.y. MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwalipia wanafunzi gharama za matibabu wanapougua wakiwa shuleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu maalum wa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambapo wanafunzi wanajiunga kwa makundi kupitia shule wanazosoma kwa kuchangia shilingi 50,400 kwa mwaka. Mpango huu wa Bima ya Afya kwa wanafunzi unawasaidia kupata huduma za matibabu wakiwa masomoni na wakati wa likizo. Aidha, kuanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote itakuwa suluhisho la kudumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi yote ikiwemo wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuna maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri ya Serikali, lakini haioni kwamba kuna baadhi ya wazazi wanaweza kushindwa kumudu gharama hiyo, kwa hiyo kuwe na utaratibu tofauti kama ilivyo elimu bure na afya iwe bure? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kuhimiza kurudisha yale masanduku ya huduma ya kwanza katika shule kama ilivyokuwa zamani kuliko sasa hivi mtoto akiugua tu anarudishwa kwa wazazi wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo amesema, ni kweli kwamba kuna wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia hii shilingi 50,400, lakini kuna utaratibu wa Kiserikali wa kuwasaidia wale watu wasiyojiweza ambao kuna utaratibu wa kuainisha na kuwasaidia na wamekuwa wakitibiwa bure.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hili la kusema kwamba afya iwe bure kama ilivyo elimu ni ngumu, kutibu tu peke yake kisukari unahitaji bilioni 321 peke yake huo ugonjwa mmoja maana yake na hapa Bungeni tunapitisha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa kwa hiyo unaweza ukaona ugumu wake.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili, suala la kuweka na kurudisha zile huduma za kwanza shuleni kwanza zipo na zinasimamiwa na kila shule za sekondari na msingi zina walimu wa afya, lakini kikubwa tutaendelea kuboresha jinsi tunavyojenga zahanati kila mahali ili kuboresha kuwa kwenye shule zetu pia pawepo huduma na mawasiliano ya kila wakati kuhakikisha huduma za afya shuleni zinazingatiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, umetumia mfano wa kisukari hapa kana kwamba watoto wote wa shule wanaumwa kisukari. Kwa hiyo ni ghali sana kuwatibu na anayeumwa malaria? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, hapana, nimejaribu tu kuonesha ilivyo ngumu kuliendesha hili limdude la afya. Tukikosea hapa, tutasimamisha Wizara nyingine zote tuhangaike na afya. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nafikiri utaratibu ule mnaotumia hata sasa wa kuwasaidia wale wasiojiweza na huko shuleni wale watoto wanaotoka familia hizo, inabidi muende na ule ule utaratibu. Kama nyumbani mnawasaidia, basi wasaidiwe na huku kwingine. Nafikiri ni kale kale kautaratibu kawekwe tu, siyo kwa maana ya wanafunzi wote, kwa sababu elimu sawa inatolewa bila malipo na kuna ambao wanajiweza. Kwa hiyo wale wakate

bima, lakini hawa ambao wanatoka zile familia ambazo hazijiwezi na Serikali inawafahamu kama hawa wa *TASAF* na mambo kama hayo, nafikiri hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya kuitazama Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Lini Serikali itaanza kuwapatia matibabu bure, wazee wenye umri mrefu hapa nchini Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza…

**SPIKA:** Umri mrefu ni kuanzia ngapi?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ni kuanzia miaka 60 na kuendelea.

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ulichokieleza tutakiboresha kwa kuhakikisha tunashirikiana na Maafisa Watendaji wa Kata pamoja na Maendeleo ya Jamii kufanya hicho ulichokielekeza hapa.

Mheshimiwa Spika, pia kwenda kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge, kwanza kuna utaratibu huo wa kuwasaidia wazee wasiojiweza ambao wanakuwa na kadi maalum kwa ajili ya kuwasaidia. Hata sasa kuna wazee ambao ni miaka 60 wako kwenye Mfuko wa Bima ya Afya. Kuna wazee wa miaka 60 ambao wanajiweza na kuna wale ambao hawajiwezi, wanaainishwa kule wilayani kwa utaratibu maalum na wamekuwa wakisaidiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Bima ya Afya kwa Wote bado haijaanza ambayo inajumuisha pia watoto katika kaya.

Je, Serikali haioni haja ya kuendelea kurudisha Bima ya Afya kwa mtoto mmoja mmoja ile ya shilingi 50,400? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tuelewe kwamba Bima ya Afya siyo mfuko wa kusaidia wasiojiweza, Bima ya Afya ni namna ambayo tunachangia kwa pamoja ili mmoja wetu anapougua basi zile fedha zetu ambazo tumechangia kwa pamoja ziweze kumsaidia huyo mmoja wetu ambaye anaumwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye huo utaratibu wa mmoja mmoja umeonesha kwamba, wanachangia shilingi bilioni tano kwa mwaka na wanatumia shilingi bilioni 49 kwa mwaka ambazo zinatoka wapi? Zinatoka kwenye hela yako wewe Mbunge na hela ya wafanyakazi wa Serikali ambao siku moja wataenda wasizikute na hatutakuwa na maelezo ya kuwaeleza hela zao zimekwenda wapi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 306

**Kutangaza Mlima Meru kama Kivutio cha Utalii**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, lini Bodi ya Utalii itautangaza Mlima Meru kama kivutio cha utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Utalii Tanzania imeendelea kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana nchini ikiwemo Mlima Meru. Utangazaji wa vivutio hivyo huzingatia shughuli za utalii zinazoweza kutekelezwa katika kivutio husika. Mathalani, Bodi ya Utalii Tanzania imekuwa ikiutangaza Mlima Meru kama kivutio cha shughuli za upandaji mlima ambapo watalii huhamasishwa kupanda mlima huo kabla ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika kuhakikisha Mlima Meru unafahamika kwa wadau mbalimbali wa Utalii Duniani, Bodi ya Utalii Tanzania imekuwa ikiandaa ziara za mafunzo za mawakala wa biashara ya utalii kutembelea mlima huo, kwa lengo la kuutangaza ipasavyo. Pia utangazaji wa Mlima Meru umekuwa ukienda sambamba na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii vinavyouzunguka mlima huo ikiwemo Hifadhi ya Taifa Arusha, Hifadhi ya Misitu ya Ziwa Duluti na maeneo ya utalii wa utamaduni katika vijiji vinavyozunguka Mlima Meru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake kubwa katika kukuza shughuli za utalii hapa nchini kupitia programu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona kasi ya Wizara hii katika kutangaza shughuli za utalii pamoja na kuibua vivutio vipya vya utalii bado ni ndogo sana. Hivyo kwanza, naomba nishauri Wizara iweze kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii pamoja na kuibua vivutio vipya, ili iendane na jitihada kubwa alizofanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina swali moja; akina mama wa Mkoa wa Arusha wengi wa najishughulisha na shughuli za kutengeneza shanga za Kimasai pamoja na vinyago, ambavyo ni vivutio vikubwa vya watalii wetu wakija hapa nchini.

Je, ni lini sasa Serikali itaweza kuwatambua akinamama hawa rasmi, ili waweze kuongeza hamasa ya shughuli za utalii, lakini pia na wao waweze kupata fursa mbalimbali zinazotokana na sekta hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika kutangaza shughuli za utalii imekuwa ikijumuisha matukio mbalimbali na hili la wafanyabishara hawa wanaoshughulika na shanga, ni miongoni mwa wadau muhimu wanaotumika katika kutangaza utalii. Tunapokuwa na makongamano mbalimbali, wamekuwa wakishirikishwa kuwa sehemu ya utangazaji wa utalii. Kwa hiyo, nitoe rai kwa taasisi zetu ziendelee kuwatumia wajasiriamali hawa ili kuongeza tija katika vivutio vya utalii wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, katika jitihada zakutangaza vivutio vilivyo Kusini Nyanda za Juu; je, Bodi ya Utalii itakuwa tayari kutangaza kwa nguvu kubwa Maporomoko ya Kalambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tayari tumeweka kwenye mpango wetu jinsi ya kuyatangaza Maporomoko ya Kalambo kuwa sehemu mahsusi ya vivutio vya utalii vya nchi yetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tumekuwa tukizungumza mara baada ya Bunge hili kuisha, mimi nikiongozana na wataalam tutakwenda kuona eneo lile la Maporomoko ya Kalambo ili kuweka mkakati mahsusi wa kuendelea kutangazwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 307

**Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo wa Madini - Singida Mashariki**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawawezesha wachimbaji wadogo wa madini katika Jimbo la Singida Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kufuatia utafiti uliofanywa na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* katika mikoa tisa nchini, Serikali imeweza kubaini maeneo manne ya changamoto zinazowakibili wachimbaji wadogo wa madini wakiwemo wa Singida Mashariki.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo ni pamoja na kutokuwa na uelewa kuhusu sheria na kanuni za sekta ya madini, taarifa za kijiolojia ya maeneo wanayochimba, mitaji na upatikanaji wa maeneo ya kuchimba madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kutatua changamoto hizo kwa kutoa elimu, kuwapatia vifaa vya uchorongaji, kuwaunganisha na taasisi za kutoa mikopo na vifaa vya uchimbaji sambamba na kutenga maeneo mahsusi kwa ajili yao. Hivyo, wachimbaji wadogo wa Singida Mashariki wako katika mpango endelevu wa Serikali wa kuwezesha ili waweze kufanya uchimbaji wenye tija. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2015 wachimbaji wadogo waliondolewa katika eneo namba moja la uchimbaji la Mang'onyi, Kata ya Mang'onyi, Jimbo la Singida Mashariki na hawajalipwa fidia mpaka leo, jambo ambalo limekuwa likisababisha mgogoro kati ya mwekezaji wa Mgodi wa Shanta pamoja na wale wananchi, kwa sababu baadhi yao ndiyo wale wachimbaji wadogo waliokuwepo hapo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Ulikuwa una swali la pili?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, swali ni moja tu; ni kwa nini mpaka leo hawajalipwa fidia, kwa sababu wanasababisha mgogoro uendelee na wale wachimbaji sasa hivi wanaomba warudishwe pale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, *Shanta Gold Mine* ulioko Singida, ulishawalipa wananchi wote wanaoishi katika eneo ambalo tayari wanafanyia uchimbaji wa madini. Kwa wale ambao wako ndani ya eneo la leseni, ambao bado hawajafidiwa, kuanzia mwaka huu wanaendelea na mchakato wa kufanya *baseline* na wamerusha ndege nyuki au *drone* kwa lugha ya kigeni ambayo imefanya tathmini ya kujua uhalisia wa makazi na mali ambazo zitakwenda kufidiwa na lengo lao ni kuanza kufidia wale ambao bado hawajafidiwa kufikia mwaka kesho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, katika Mgodi wa *Barrick North Mara,* Nyamongo kumekuwa na matatizo ya madhara ya hapa na pale, majeraha na mauaji kwa sababu vijana wanahitaji eneo la wachimbaji wadogo. Ningetamani kujua, ili kutenganisha mgogoro uliopo pale kati ya vijana na

mgodi; ni lini Serikali itachukua maeneo ambayo mgodi hauwezi kuchimba kwa ukubwa wake, wawakabidhi wananchi na hasa vijana wa eneo lile, ili kupunguza malalamiko na mgogoro uliopo kati ya vijana wa Tarime na Barrick ili ifanye kazi ya kibishara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na mwekezaji mkubwa wa *North Mara Gold Mine* umeshaweka utaratibu wa kumwomba mwekezaji huyo asaidie wachimbaji wadogo kuwafanyia utafiti katika maeneo yanayozunguka mgodi wake, sambamba na kutoa ardhi ya maeneo ambayo anaona hamna uchimbaji au uzalishaji wenye tija kwa kampuni kubwa kama ile, ili hawa vijana ambao wanavamia mgodi kila wakati na kusababisha madhara katika wao kujeruhiwa au kufikwa na maafa, waweze kupewa maeneo ambayo kampuni hiyo pia imeahidi kama sehemu ya mchango wao kwa jamii kuwasaidia mitaji ya kuwekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawaona mmesimama, lakini maswali mnaweka historia ndefu kwa hiyo mnamaliza muda. Mheshimiwa Ester Bulaya, swali kwa kifupi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni lini Serikali mtawasaidia wachimbaji wadogo katika eneo la Kinyambwiga, Jimbo la Bunda Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wachimbaji walioko Kinyambwiga na maeneo mengine yote nchini, changamoto zao ndio hizo ambazo nimezitaja katika majibu ya swali la msingi kwamba wale ambao hawana maeneo mahsusi ya uchimbaji, Wizara ya Madini imeendelea na mchakato wa kufanya utafiti kwa kutumia zana za kisasa ili tupate maeneo mengi zaidi yenye madini katika kila eneo la mikoa ya madini, ili wachimbaji hawa wadogo na wote wenye kutaka kuingia

kwenye sekta wapate migodi yao halisi yenye taarifa sahihi za kijiolojia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali kwa kifupi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta mitambo ya *GST* katika Mkoa wa Iringa ili kusaidia utafiti wa wachimbaji wadogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imeshapeleka mitambo mitano ya kufanya utafiti au uchorongaji wa madini katika baadhi ya mikoa nchini na kuna mitambo mingine kumi ambayo imeshaagizwa na hiyo itakapofika hata Mkoa wake wa Iringa na mikoa mingine ambayo ni ya kimadini, watakwenda kufaidika na zana hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida kuna mgodi mkubwa wa *Shanta Gold Mine,* unapozunguka kuna watu wanachimba pale lakini wanabahatisha.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia kwenda kufanya utafiti wa kina *(exploration)* ili na wenyewe wapate tija? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema tayari tumeshaanzisha mpango wa utafiti wa kina wa maeneo mbalimbali nchini kwa kutumia hizo ndege nyuki na eneo alilotaja Mheshimiwa Mbunge ni kati ya maeneo ambayo ndege ile imesharushwa na taarifa zile zinaendelea kuchakatwa ili wachimbaji wadogo wapate maeneo yenye taarifa sahihi za kijiolojia, wafanye uchimbaji wenye tija. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mahamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 308

**Mradi wa Maji Tanki Mgulu wa Ndege- Morogoro**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamaliza Mradi wa Maji Tanki la Mgulu wa Ndege na kuanza kusambaza maji Kata za Mkundi, Kiegea na Kihonda – Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa Mradi wa Maji Mgulu wa Ndege unaohusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma maji *(booster station),* ujenzi wa matanki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita milioni tatu na mtandao wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 250. Hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 93% na baadhi ya wananchi wa Kata ya Kihonda wameanza kunufaika wakati utekelezaji ukiendelea kwa ajili ya kufikisha huduma kwenye kata zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na wananchi wapatao 135,000

watanufaika na huduma ya maji safi kwenye Kata za Mkundi, Kiegea na Kihonda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, wakati mradi huo ukiendelea, je, Serikali ina mpango gani wa visima virefu kandokando ya Mji wa Morogoro Mjini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Mkoa wa Morogoro, pia kuna Mradi wa Maji wa Miji 28 wa Ifakara – Viburugutu; je, ni lini mradi huo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mbunge wa Morogoro Mjini pamoja na Mbunge aliyeuliza swali wa Ifakara, Mheshimiwa Asenga; ni kweli kabisa Serikali inaendelea na tathmini na kujiridhisha na uhitaji wa maji katika Mji wa Morogoro na mkoa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa suala la miji 28 upande wa Ifakara, mradi huu unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2025 na utakuwa umeanza kutoa maji na mtandao wa maji utakuwa umekamilika kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Asenga wataanza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Morogoro Mjini na maeneo ya pembezoni kuhusu visima ambavyo vitaweza kusaidia; ni kweli kabisa jana hapa katika bajeti yetu ya Maji. Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ametoa zawadi ambayo imetoka kwa Mheshimiwa Rais, kwa kila Mbunge wa Jimbo kupata visima vitano. Kwa hiyo, tunaamini kwamba katika visima hivyo vitano naamini kabisa kwamba kwa namna moja au nyingine unaenda kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali kwa kifupi.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu huu Mradi wa Mgulu wa Ndege umechukua muda mrefu na wananchi wa kata hizi wamekuwa muda mrefu hawapati maji; je, Mheshimiwa Waziri unawaagiza nini watendaji wa maji kusudi huu mradi ukamilike kwa wakati ili hizi kata ziweze kupata maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, mradi huu umefikia wastani wa 93%. Mradi huu utakapokamilika na ndipo utakapoanza kutoa maji. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu umekaa muda mrefu na kwamba umekuwa ni changamoto, lakini miradi hii inaenda kukamilika katika mwaka huu wa fedha kama ambavyo wananchi wa Morogoro wanavyotarajia kupata huduma ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Kata ya Ng'ang'ange umechukua muda mrefu kumpata mkandarasi, sasa kwa kuwa, ameshapatikana; je, ni lini mkandarasi huyo ataanza kazi, ili wananchi wa Kata ya Ng'ang'ange waweze kupata maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, natambua na Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji katika Jimbo la Kilolo ambapo Mheshimiwa Nyamoga anatoka pale.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitenga fedha na mkandarasi

ameshapatikana na kati ya kipindi hiki cha Bunge, tumeshakubaliana na Mheshimiwa Mbunge tutaenda kusiamia utiaji wa saini wa mikataba hiyo, ili mkandarasi aingie na kuanza kufanya kazi mara moja. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali isichimbe visima kama suluhisho la muda mfupi kwa Sekondari ya Nyandoto, Tagota na Nkongole kwa kipindi hiki ikisubiria mradi wa Ziwa Victoria ukamilike kutoka Tarime, Rorya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Esther kwa kuendelea kufuatilia miradi inayotekelezwa ndani ya Mkoa wake wa Mara, lakini vilevile Serikali ina mipango mitatu; mpango wa muda mfupi, mpango wa muda wa kati na mpango wa muda mrefu. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wakati Watanzania wanasubiri miradi ya muda mrefu ikiwa inakamilika, basi mpango wa muda mfupi uweze kuwasaidia ili kuhakikisha kwamba wanaondokana na changamoto ambayo inaweza ikawapata kiafya kwa kukosa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana jana Mheshimiwa Waziri, ninarudia, Mheshimiwa Jumaa Aweso ametoa ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu visima 900 ambavyo vinaenda kuchimbwa nchi nzima na katika visima hivyo ni kila jimbo wanaenda kupata visima vitano. Kwa hiyo, kama Mkoa wa Mara una majimbo kumi, maana yake wanaenda kupata visima 50. *(Makofi)*

Meshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaamini kwamba katika kutatua changamoto ya muda mfupi, basi Serikali itakuwa imefanya kazi hiyo ili Watanzania waendelee kupata maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan.

Na. 309

**Tatizo la Maji Newala na Tandahimba**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaimarisha miundombinu ya Mamlaka ya Maji ya Makonde ili kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 6,720 hadi 23,741?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukarabati wa Mradi Wa Maji Makonde ili kuboresha huduma ya maji kwenye Wilaya za Newala na Tandahimba. Ukarabati huo unahusisha uchimbaji visima virefu vitatu vyenye uwezo wa kutoa maji lita milioni 26 kwa siku ambapo uchimbaji wa kisima kimoja umekamilika katika eneo la chanzo cha maji Mitema na kina uwezo wa kuzalisha maji lita 150,000 kwa saa. Uchimbaji wa visima viwili unaendelea na utakamilika mwisho wa mwezi Desemba, 2024. Kazi ya ujenzi wa miundombinu kupitia visima hivyo inatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Newala na Tandahimba ni miongoni mwa Wilaya nufaika za mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ambapo hadi sasa utekelezaji umefikia 24%. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mainuma Pathan, swali la nyongeza.

**MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, mradi huu unasuasua kwa sababu Serikali haijamlipa mkandarasi kwa muda mrefu. Sasa je, lini Serikali itapeleka fedha ili mkandarasi huyu aweze kulipwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna miradi miwili ambayo ilianza kuchimbwa mwaka 2021 katika Kijiji cha Mpalu na Luchino. Je, nako ni lini watapeleka pesa ili miradi hiyo iweze kuendelea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshmiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, lililoulizwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto iliyopo na tayari Serikali imeshapokea hati ya madai kutoka kwa mkandarasi ya kiasi cha shilingi bilioni 3.4. Kwa hiyo, tunaamini kwamba muda wowote kuanzia sasa mkandarasi huyo atalipwa na baada ya hapo ataendelea na kazi na mradi huo utakamilika.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili kuhusu visima viwili ambavyo vimechimbwa katika vijiji viwili; ni kweli kabisa visima hivyo tulikuwa hatujapata fedha na sasa tayari Serikali imeshaelekeza kupeleka fedha na tumeshanunua pampu, tumeshanunua *solar* na vilevile tuna ujenzi wa tenki la lita 5,000 ambapo baada ya ukamilishaji wake basi wananchi wa eneo hilo wataendelea kupata maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele kabla hatujaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni waliko Jukwaa la Spika; wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni walimu wa Shule ya Msingi Boma kutoka Ilala Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Andrew Paul Koti, Mwalimu Mkuu; karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Joyce Tuli Shalua, Mwalimu wa Uhasibu na Uchumi; na yupo Ndugu Nunu Ibrahim Uiso, Mwalimu wa Mipango, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso; yupo Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuyo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Musoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana Hussein Sufian, Mwenyekiti wa Bodi Bonde la Mto Wami na Ruvu; yupo Bi. Monica Ngenzi Mbega ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Felician Komu, Mwenyekiti Bodi ya Chuo cha Maji; yupo Mhandisi Joshua Mgeyekwa, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Kahama na Shinyanga; na yupo Dkt. Fungo Ally Fungo, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Bi. Edina Mwaigomole, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Mbeya, yupo Bi. Naomi Lupimo, Mwenyekiti wa Bodi Bonde la Rufiji; yupo pia Bwana Lazaro Msaru, Mwenyekiti wa Bodi Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini; na yupo Bwana William Mabula, Mwenyekiti wa Bodi Bonde la Kati; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Bi. Grace Kidunda, ambaye ni mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Haya karibu sana, karibu sana. *(Makofi)*

Unajua wakati nasoma hapa nilianza kusita, nikawa ninawaza kumbe Mheshimiwa Waziri wa Maji ameongeza wa tatu

na hatuna habari. Sasa kumbe leo ni mke wa Naibu Waziri, karibu sana, karibu sana wifi yetu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 11 wa Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, hawa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Bariadi Mkoa wa Simiyu, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Ally Kassinge ambaye ni mdau wa maendeleo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambaye ni rafiki yake kutoka Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mipango Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira kutoka Manispaa ya Moshi Mkoa wa Kilimanjaro *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Robert Maboto ambaye ni mjasiriamali kutoka Bunda. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ndugu yake kutoka Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Eeh! Sasa hapa sina uhakika sana, hawa si hawaruhusiwi kuwa wanasiasa hawa. Ama! Mheshimiwa Shangazi, ama sisi ndiyo tumekosea kuandika hapa. Maana kama wanatoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto Mkoa wa Tanga labda kama ni karibu kama wanatokea maeneo hayo.

Haya Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni viongozi wa dini kutoka Arumeru Mashariki, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni Wajumbe wawili wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi Taifa kutoka Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 94 na walimu watano wa Shule ya Sekondari Msalato ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma Ndaki ya Insia na Sayansi ya Jamii, karibuni sana. *(Makofi)*

Haya wageni waliotangazwa kutokea Bariadi ninaambiwa hawa ni Madiwani Viti Maalum, karibuni sana Bungeni Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo tarehe 10 Mei, 2024 kutakuwa na Semina kuhusu Elimu ya Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza, sambamba na elimu kuhusu vilevi, ikiwemo pombe na tumbaku.

Semina hii itaendeshwa na Wizara ya Afya na itafanyika mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana, katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria mafunzo haya muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linalotoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba siku ya kesho Jumamosi tarehe 11 Mei, 2024 kutakuwa na semina kuhusu mkakati wa ushirikishwaji wa wakandarasi wazawa na washauri elekezi kwenye kazi za ujenzi *(Local Content Strategy)* itakayotolewa na Wizara ya Ujenzi. Semina hii itaanza saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na tunao Wabunge hapa ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii.

Tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mugita Kajege, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania na hasa katika kuboresha huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kusema kwamba mimi nimekuwa mdau mkubwa wa kufuatilia huduma za jamii. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amefanya kazi kubwa sana katika kuboresha huduma za jamii. Tukienda kwenye sekta ya afya, sekta ya elimu, sekta ya maji na sekta zingine mbalimbali ambazo zinawagusa wananchi au zinagusa Watanzania moja kwa moja. Mama huyu amefanya kazi kubwa na kwa kweli lazima tumpe hongera yake, tumpe maua yake kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitizama katika miradi ya maji, mimi nimekuwa msimamizi mkubwa, mmenipa kazi ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Afya. Kuna fedha nyingi zinatengwa kwa ajili ya huduma za afya na katika huduma za afya, moja ya shughuli ambazo zinatakiwa zifanyike ni kupambana na kuzuia magonjwa mbalimbali. Magonjwa ya kuambukiza na magojwa yasiyo ya kuambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Rais kupeleka maji vijijini ni hatua muhimu sana ya mapambano dhidi ya magonjwa ya kuambukiza. Usipopeleka fedha kwenye miradi ya maji kwenda kuzuia magojwa ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya watu kupata maji, tatizo kubwa linalokuja au linalofuatia ni watu kupata magonjwa ya kuambukiza pale wanapoishi katika mazingira yenye maji duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu alipoingia madarakani alisema anakwenda kumtua mama ndoo kichwani. Kazi hii ameifanya vizuri na chini ya Waziri wa Maji na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na Naibu aliyeondoka, dada yangu Makundi, wamefanya kazi kubwa. Kwa kweli tuwape sifa na wananchi wa Tanzania wanaona juhudi zenu. Hii yote ni kwa sababu ya usimamizi na uimara wa Rais tuliyenaye ambaye anatambua matatizo na haja ya Watanzania kwa maana ya kutatua changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipeleka dola moja kwenye huduma ya maji unakuwa umeokoa dola nne kwenye kumtibu mtu ambaye anayepata huduma ya maji. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kupeleka maji kwa wananchi ni uungwana wa hali ya juu. Tuzidi kumwombea Rais wetu afya njema kwa sababu ana nia njema ya Watanzania kuwa na afya njema kwa sababu ya kuwapelekea maji na ambapo maji hayo ni afya na wanasema maji ni uhai. Uhai maana yake ni uhai wa kuishi lakini ni uhai wa kuepukana na magonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, tumeona bajeti yako, jitahidi sana wananchi wa Tanzania

waendelee kupata maji na salama kwa sababu ndiyo uhai wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuendelea kushukuru, katika Jimbo langu la Maswa Mashariki nimeweza kupata miradi mingi ya maji na hii ni katika mkakati uleule wa kumkomboa Mtanzania kwa kumpelekea maji safi na salama. Katika Jimbo la Maswa Mashariki, niendelee kusema ninashukuru, katika Mji wa Maswa tumepata fedha, tumejenga mradi mkuwa wa tenki la maji katika Mji wa Nyalikungu, tumepata tenki kubwa la maji linaloweza kuhifadhi lita milioni moja na tumeweza kutengenezewa mtandao wa maji katika Mji wa Maswa. Sasa maji yanafika na ni maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipata shilingi bilioni tatu za kujenga chujio katika Bwawa la Zanzui, sasa maji yanachujwa na maji yanawafikia Watanzania yakiwa safi na salama. Tulipata mradi mwingine, mradi wa maji kutoka Mandang'ombe kwenda Lalago tumefikisha maji katika Mji wa Lalago na maeneo ya pembeni ya Mji wa Lalago. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto kidogo iliyopo, maji yetu yana chumvi, tunaomba wataalamu waendelee kutusaidia katika kufanya utafiti, waweze kutafuta vyanzo vizuri vya maji kwa sababu maeneo yetu kuelekea mpaka maeneo ya kule Meatu yana ukanda ule wa maji ya chumvi. Kwa hiyo, watutafutie maji maeneo hayo ambayo ni salama ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hapo tu, kuna mradi wa maji wa Nguliguli kwenda katika Kata ya Mwamanenge, Mheshimiwa Rais amefika hadi Mwamanenge huko, wananchi wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine ambao sasa unakwenda kujengwa katika ya Ipililo; Kata ya Ipililo ni kata kubwa, ina wananchi wengi wanahitaji maji safi na salama, lakini leo mradi umekwenda kule na leo fedha zimefika na mradi unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata maji katika mradi mwingine wa tenki la maji kuelekea katika Mji wa Maswa, tenki lingine nje na lile la milioni moja katika Kijiji cha Hinduki. Tenki la milioni mbili linakwenda kujengwa, ninakuomba Mheshimiwa Waziri fedha zimeletwa, lakini fedha zilizoletwa zimekwisha, mkandarasi amesimama. Tunaomba fedha za kumalizia mradi huo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais mmetuletea ni Mradi wa Ziwa Victoria. Tumeona katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri mradi huu ambao ni wa kwenda kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambao una thamani ya *Euro* milioni 171, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako umeeleza vizuri mmetenga fedha hizo, lakini haujatuambia mradi huo unakamilika lini. Tunaomba sasa mradi huo ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Simiyu toka mwaka 2015 wameahidiwa kupata maji kutoka Ziwa Victoria ambapo yanakwenda katika zile wilaya tano za Mkoa wa Simiyu, tunaomba toka tumeahidiwa mradi huu haujaleta maji. Tunaomba basi imefika wakati isiwe kelele na porojo, tunakujua wewe ni mpiga kazi, hebu tunaomba mradi huu uanze, wananchi wa Mkoa wa Simiyu ambao wanapambana na mabadiliko ya tabianchi na tuna ukavu ambao unatukabili katika mkoa wetu, tunaomba mradi huu ufike kwa sababu mradi huu ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kushukuru, kuna mabwawa yamejengwa, Bwawa la Kijiji cha Zebea, Kata ya Senani, kuna bwawa limejengwa pale chini ya utawala wa Rais wetu ambaye ndiye Rais ameleta huduma kubwa ya maji. Watu wa Zebeya leo wamejengewa bwawa na bwawa hii linakwenda kuwahudumia wananchi wa Kata ya Senani na Zebeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba basi bwawa hili waendelee kulitolea fedha kwa maana ya ukarabati na bwawa hili liendelee

kufanya kazi lakini siyo hivyo tu kuna mabwawa mengine ambayo yametengenezwa, kuna Bwawa la Kijiji cha Igumangobo, kuna Bwawa la Kijiji cha Ilambambasa, kuna Bwawa la Kijiji cha Mwadila. Sisi kama wananchi tunaendelea kumshukuru Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nimekwisha kukufuata, nimekwisha kukueleza pale Mwadila tulikwenda mimi na wewe, lile bwawa limejengwa pale sawa, lakini bwawa hilo linachangamoto. Wananchi wa pale wanaozunguka katika bwawa hilo walilalamika, walisikia inasemekana lile bwawa walipewa watu wa Bonde la Ziwa Victoria bure na wananchi kwa ajili ya kujenga au ujenzi wa bwawa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekwishamwambia Mheshimiwa Waziri kuwa bwawa hilo hayo maeneo hayakutolewa bure, yale maeneo yanatakiwa yalipwe fidia, lakini wananchi mpaka leo wameandika barua, wamekuja kwangu mimi Mbunge, nimefika na kwako, Mheshimiwa Waziri, walipeni fidia ya yale maeneo, wananchi wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba muwalipe fidia ili kusudi wakae kwa amani na wao waweze kutunza lile eneo kwa sababu ni chanzo cha maji na wanufaika ni wananchi wengi. Sasa wale wachache waliotoa maeneo yao tunaomba walipwe kwa sababu, sababu ya kutokuwalipa haipo, hawajatoa bure yale maeneo Mheshimiwa Waziri, naomba niseme hili na nimeamua leo kusema hapa kwa sababu nimekwishakukwambia na kwa kweli naomba wananchi wangu wanalia na kila siku wananifuata wananiambia maeneo hayo yametwaliwa bure, lakini wanatakiwa walipwe haki yao ya kulipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, niendelee kushukuru kwa kweli kwa ujenzi wa mabwawa, naomba kuna maeneo mengine kwa mfano Kijiji cha Mwamashindike. Kijiji cha Mwamashindike wanahitaji kujengewa bwawa, tunaomba muwatengee fedha wawezekujengewa bwawa kwa sababu maeneo hayo wananchi wanapata shida na kwa kweli hali siyo nzuri tunaomba sana

Mwamashindike, Mheshimiwa Naibu Waziri hapo anapafahamu vizuri sana, Mwamashindike nikisema Mwamashindike ananielewa, aende na wapeleke fedha, waende mkajenge Bwawa la Mwamashindike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, tumeona upatikanaji wa maji katika nchi yetu tumeona ni wa hali ya juu, vyanzo vya maji tulivyonavyo ni vingi. Ukiangalia katika hotuba yako, *population* ya watu zaidi au karibia milioni 60 ya Watanzania wanawastani wa kupata maji lita 2,000 kila mmoja. Naomba niendelee kutoa ushauri, katika miradi mingine kwa mfano ya umeme na miradi mingine ya afya kuna ile kutoa miradi kwa kufuata *PPP* kwa maana ya *Public Private Partnership*. Kama *Public Private Partnership* kwa nini isitumike na kwenye maji? Wale wajasiliamali wenye uwezo wa kujenga miradi mbalimbali kutoka kwenye vyanzo vya maji basi wapewe nafasi wajenge halafu Serikali ifanye, i-*subsidize* kwa maana ya kuwapelekea maji wananchi kwa huduma ambayo itakuwa ya bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, naunga mkono hoja katika Wizara hii, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, majina yaliyoletwa hapa ya Wabunge ambao wanaomba kuchangia ni mengi kuliko muda ambao tunao leo, kwa hiyo wale Wabunge ambao hawajachangia kabisa na wale ambao wamechangia mara moja, watachangia kwa dakika saba. Wale ambao wamechangia zaidi ya mara moja watachangia kwa dakika tano, tano.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnataka tupige kura ili tufanye maamuzi nani achangie na nani asichangie, lakini hivyo ndiyo vigezo nilivyoviweka hapa mbele ili muda wetu uweze kutosha, kwa sababu la sivyo kuna watu hawatapata nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Mugita Kajege, atachangia kwa dakika saba, atafuatia na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah kwa dakika saba, Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ajiandae dakika saba.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwanza kabisa labda naomba nirekebishe majina yangu, naitwa Charles Muguta Kajege, Muguta Kajege nafikiri labda kutakuwa na makosa katika uandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake bora na wa kiwango cha juu sana. Mama anatenda zaidi kuliko kusema, mama hongera sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na timu yake nzima ya Wizara ya Maji na taasisi zake zote, mnafanya makubwa sana katika sekta hii ya maji, maji ni uhai, mnastahili kupata maua yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutushika shavu sisi Wana-Mwibara kwa kutupa miradi mingine mingi sana katika kila sekta, kwa mfano katika sekta hii ya maji tumepata miradi ya maji katika maeneo yafuatayo; Buzimbwe kwenda Kabainja, Kabainja kwenda Lagata, Kasuguti, *Scheme* ya Kalukekele, Buzimbwe na mradi mkubwa wa Kisorya hadi Kibara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu utaunganisha maji katika vijiji zaidi ya 33 na kama nilivyozungumza wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais kule Bunda mwaka juzi, nilisema mradi huu mkubwa ni suluhisho la matatizo ya maji katika hizi kata sita za kutoka Kisorya hadi Kibara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mimi bado napata wasiwasi katika bajeti hii kama tunaweza kufikia malengo. Kwanza ni ufinyu wa bajeti, mimi nilitegemea kwamba kwa sababu mahitaji ya maji yanaongezeka kila siku, nilitegemea kuona kwamba bajeti hii

inaongezeka lakini bahati mbaya imepunguzwa kwa zaidi ya shilingi 128,420,765,000.

Mheshimiwa Spika, sasa nikiangalia mahitaji tuliyonayo ya maji hasa katika maeneo ya vijijini, kwa mfano katika Jimbo langu la Mwibara bado tunahitaji maji katika maeneo mengi sana. Sasa nikiona ufinyu huu wa bajeti na bajeti itapunguzwa nashindwa kuelewa, lakini vilevile mahitaji ya maji yameongezeka, nilitegemea sasa kuwe na ongezeko kubwa zaidi la bajeti hii hapa.

Mheshimiwa Spika, kingine ni katika Mfuko wa Maji; Mfuko wa Maji unatakiwa upate pesa *straight* kama zilivyo taasisi zingine, kama *EWURA* na *TANROADS,* lakini kwa bahati mbaya hizi pesa kwanza zinakwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali, halafu baadaye ndiyo ziweze kurudi katika Wizara ya Maji. Mimi nilikuwa napendekeza hizi pesa ziende moja kwa moja katika Wizara, lakini pia tuangalie ugawaji wake, mpaka sasa hivi hakuna *formula* ya kuzigawa hizi pesa ni kiasi gani ziende vijijini na kiasi gani ziende mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wananchi wengi wanakaa vijijini na vilevile matatizo mengi makubwa ya maji yapo vijijini, nilikuwa napendekeza *at least* 80% ya pesa hizi sasa kwanza zitengenezwe kanuni ya kuhakikisha kwamba zinakwenda vijijini, kwamba ni kiasi gani kinakwenda vijijini na asilimia ngapi zinakwenda vijijini. Mimi nilikuwa napendekeza 80% iende vijijini na inayobakia ndiyo iende mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni miradi ambayo ipo chini ya programu ya *P4R*. Tunaelewa kwamba hizi pesa ni *readily available* zipo pale, lakini kunakuwa na tatizo la kutolewa pale ambapo mkandarasi anapokuwa amemaliza kazi ambayo imependekezwa, inachukua zaidi ya mwezi mmoja. Tatizo lake linakuwa kwamba hapa kuna hatari kama mkandarasi katika muda aliopewa huenda asimalize katika muda wake, kwa mfano kama atamaliza sasa hivi hapa aka-*submit certificate* ikachukua zaidi ya mwezi mmoja maana yake tayari ameshapoteza mwezi mmoja kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu hawezi ku-*submit* hiyo *certificate* mara moja, ata-*submit* labda kama mara tatu maana yake kuna miezi mitatu mizima ambayo itapotea bila kufanya kazi. Inapofika mwishoni kama amechelewa anakuwa anakatwa *liquidated damage*. Sasa hii kidogo inatoa usumbufu sana kwa wakandarasi, lakini tatizo lingine ni madeni makubwa ambayo sasa yapo katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, hawa wakandarasi ni kama *buffer zone* ya Wizara ya Maji, wanatumia pesa zao, wanatumia mikopo kupata pesa ili waweze kufanya hii kazi, lakini inapofikia kupata malipo wanakuwa hawapati malipo yao kwa wakati. Mimi nafahamu wakandarasi wawili ambao wamepata *stroke* kutokana na tatizo la kukabiliwa na madeni katika benki ya *CRDB*. Vilevile *CRDB* sasa hivi inakataa ku-*sponsor* miradi ya maji kwa sababu kuna madeni makubwa sana ya maji. Mimi nilikuwa niiombe Serikali yangu iangalie suala hili ili madeni haya yaweze kulipika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo machache, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso na timu nzima ya *RUWASA* wakina Dkt. Kivegalo yaani *DG* wa *RUWASA* na watendaji wake wengine kwa kazi nzuri, hawa wanastahili vilevile maua yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mheshimiwa John Marko Sallu ajiandae. Wote wanachangia kwa dakika saba, saba.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, lakini kadhalika kwanza kabla sijaanza mchango wangu, nimshukuru *Allah Subhanahu wa Ta'ala*, leo Ijumaa kwa kutujaalia uzima na salama na kuweza

kukusanyanyika wote hapa tukaendelea na majukumu ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ningeanza pia kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na jopo lake zima la Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Waswahili wanasema kwamba; wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri jamii na Watanzania wanaona jinsi Mheshimiwa Wazri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Maji inavyofanya kazi vizuri na sisi kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati, nimeweza kutembea maeneo mbalimbali ya Tanzania, tumeweza kwenda Morogoro, Tabora, tumeweza kwenda vilevile maeneo ya Manyara, Songea, maeneo ya Ludewa kule wapi hapa na nihii, lakini kote humo waheshimiwa tumeangalia miundombinu ya maji kwa kweli kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama Waswahili wanavyosema kwamba usione kobe yupo kwenye mti, lakini lazima kuna mtu amempandisha. Sasa hii inaonesha wazi kwamba Mheshimiwa Waziri na jopo lake wanafanyakazi, lakini hii ni ishara kuwa mama yupo kazini, kwamba mama anafanya kazi kubwa, ametenga fedha na hadi sasa ukiangalia miradi kila pahala, *pipes* zinapelekwa, miundombinu inahimarishwa, matanki yanajengwa, hii ni kuonesha wazi kwamba mama kwa kweli amedhamiria kumtua mwanamama ndoo kichwani, ahsante sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia inakabiliwa na tishio kubwa sana la uharibifu na la upungufu wa maji na hii imepelekea watu wengi duniani kuweza kuwa maisha yao hatarini kutokana na upungufu wa maji safi na salama. Sasa sisi kama Tanzania, wenzetu wa jopo la sayansi ya mabadiliko ya tabianchi ya dunia *(IPCC)* ambalo bahati nzuri Makamu Mwenyekiti wake ni Mtanzania mwezetu ambaye sasa hivi ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wamehusisha masuala

mazima ya maji upungufu wake pamoja na masuala mazima ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Tanzania tunahitajika kama Taifa tujue kwamba mabadiliko ya tabianchi nayo ni changamoto ambayo imekuja juu ya mambo mengine mengi, uharibifu wa mazingira, lakini mabadiliko ya tabianchi nayo yameongeza petroli kwenye moto ambao tayari unawaka, kwa hiyo, lazima tujipange vizuri na tuchukue hatua za haraka ili kuweza kuhakikisha kwamba rasilimali ya maji tunaisimamia vyema, lakini halikadhalika tunasambaza na kuweza kuhudumia wananchi kwa kuhifadhi vyanzo vyetu vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini tufanye ili kukabiliana na matatizo haya; nukta ya kwanza hapa lazima twende tukafanye mapitio ya ile sera yetu ya maji ya mwaka 2002, kwa sababu hii sera ina miaka 22 sasa, bila shaka nafikiri sisi ni mashuhuda kwamba huu ni muda mrefu sana na zaidi ukitilia maanani kwamba ukuaji wa sekta na mabadiliko mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, teknolojia halikadhalika na mabadiliko ya mambo chungu mzima ya kidunia tunahitajika lazima hapa tuhakikishe kwamba sera hii imebadilishwa. Tumebadilisha Sheria Namba Tano ya mwaka 2019 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira. Sasa sheria tumerekebisha lakini bado tunalega lega kwenda kufanya mapitio hii Sera ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri na hili alifanyie kazi kwa haraka, kwa sababu kuna mambo mengi ya kuyazingatia hapa. Kwanza kuendana na mwelekeo mpya wa huduma za maji, tulikuwa tumejipangia kwamba tufikishe maji katika vijiji 12,000 hivi na kidogo tuwafikishie maji angalau tupate katika upeo wa mita 400. Sasa hivi dunia imebadilika na hili tumelifanya vizuri mpaka sasa hivi kwa sababu ukiangalia sasa hivi tumebakisha vijiji visivyozidi 2,000 ambavyo havijafikiwa na maji katika *premises* hiyo ambayo tumejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba tu kwamba ili mwelekeo huu mpya tuuweke kwenye sera kila mtu aweke maji ndani sasa badala ya ile mita 400 sasa twende tukabadilishe mwelekeo wa

sera tuweke maji sasa hivi wananchi waweke maji nyumbani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kuna suala zima la uhifadhi wa vyanzo vya maji, wenzetu hawa wameainisha vyanzo karibu 2,880 hivi, lakini vyanzo 282 tu ndivyo ambavyo mpaka hivi sasa vimeweza kuwekewa mipaka na kupimwa lakini vyanzo 59 tu ambavyo vimeweza kuwa *gazetted*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa ni asilimia haizidi 20 au pungufu yake ambavyo vyanzo vya maji vimeweza kupimwa na kuwa *gazetted*. Sasa ningeomba hili Mheshimiwa Waziri akalitilie maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala zima la bajeti, hali ya bajeti ni mbaya na hili hapa nakusudia kushika shilingi kwa sababu Mheshimiwa Waziri lazima atuambie atafanya miujiza gani katika bajeti ambayo imepungua na madeni yaliyopo ambayo yanatakiwa yalipwe, lakini halikadhalika tunakwenda kusambaza maji katika vijiji vilivyobakia zaidi ya vijiji 2,000 na kidogo. Sasa hii miujiza hapa nataka ndiyo Mheshimiwa Waziri aje na mpango hapa ataniambia wakati anafanya majumuisho yake atafanya nini kwa bajeti ndogo aliyonayo kuweza kukidhi hayo mahitaji na katika hili nitashika shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine zima ni suala zima la Gridi ya Taifa. Suala la Gridi ya Taifa ameliongelea vizuri na huyu mshauri elekezi ameshapangwa, ningeomba hili tukalichukulia jitihada, tukalitafutia fedha na tukalifanya kwa haraka na kwa sababu bila ya hivyo matatizo ya kidunia, mabadiliko ya tabia ya nchi bila kuwa na gridi ya kitaifa basi hayatatuacha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri suala hili alichukulie kwamba ni suala la muhimu, alifanyie kazi na bila kuisahau Zanzibar, mmetupelekea umeme tunashukuru na tunalipia vizuri kwa hiyo pia hii Gridi ya Taifa hii tuwekeeni angalau *pipe* ambayo inaelekea Zanzibar ili baadaye yakitokea matatizo ya mabadiliko ya tabianchi, chumvi imekuwa nyingi, tuweze kusaidia na Zanzibar tupelekee maji... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, atafuatiwa na Mheshimiwa John Marko Sallu, Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo ajiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika sekta hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri sana anayoifanya katika nchi yetu na hasa katika sekta hii ya maji, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya katika kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kusudi aweze kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi katika sekta hii ya maji. Siyo yeye tu ni pamoja na Naibu Waziri, lakini na watumishi wote wa Wizara hii ya Maji, wapewe maua yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu tukiwa tunaendelea mwaka 2022 sekta ya maji ilikuwa na asilimia ndogo sana. Mwezi Disemba, 2022 upande wa vijiji tulikuwa na 77% lakini kufikia mwaka 2023 tumepata 79% ya upatikanaji wa maji vijijini. Mwaka 2022 mwezi Disemba mijini tulikuwa na 88%, lakini mwaka 2023 mijini tumekwenda mpaka 90% kwa upande wa maji na ndiyo maana nasema Dkt. Samia apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusema Dkt. Samia apewe maua yake, akiwa Makamu wa Rais hii ilikuwa ni ajenda yake ya kumtua mama ndoo na sisi wote tunaona kwa macho na kwa dhati kwamba ametekeleza na anaendelea kutekeleza kuhakikisha anamtua mwanamke wa Kitanzania ndoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema hayo kama shahidi kabisa wa dhati katika Mkoa wa Mara, tumepata miradi mingi na mikubwa ya maji. Ukianza katika Wilaya ya Bunda, tumepata Mradi wa Maji wa Nyebehu. Mradi ule tumepata zaidi ya shilingi bilioni 10, kwa ajili ya utekelezaji wa maji na mpaka sasa mradi ule umekamilika 100% na sasa tunahitaji tu pesa nyingi kwa ajili ya usambazaji ili kusudi wakina mama wa Mkoa wa Mara na wananchi wote wa Mkoa wa Mara, wakiwemo wale wa Bunda, waweze kupata maji katika vijiji vyote. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakutuacha hapo ametupa mradi mwingine mkubwa wa maji, Miradi ya Miji 28, ametupa katika Wilaya ya Rorya na Tarime, na mpaka sasa mradi ule upo 13%. Mimi ninachoweza kumwomba Mheshimiwa Waziri, ni pesa. Namwomba Mheshimiwa Mwigulu, amuangalie kwa jicho la pili sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, ampe pesa ili kusudi aweze kutekeleza mradi ule. Ule mradi ukiisha utaenda kuwanufaisha wananchi wa Rorya na vijiji vyake vyote. Utaenda kuwanufaisha wananchi wa Tarime na vijiji vyote wananchi wa Tarime Mjini na Vijijini, lakini na wale wa karibu maeneo ya Serengeti. Mradi ule utaenda kuwagusa akina mama na akina baba wa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mama ametupa Mradi wa Mgango, Kiabakari mpaka Butiama, mradi ule upo 95% na sasa tumeshaanza majaribio. Ombi letu nikuhakikisha vijiji vyote vinapata maji. Tunaomba watupe fedha kwa ajili ya usambazaji ili akina mama wa Mkoa wa Mara waende kupata maji kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kusema Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi kubwa na nzuri sana katika Mkoa wetu, ninaendelea kuwapa ushahidi, sisi katika Mkoa wa Mara, tuna majimbo kumi na katika majimbo kumi na Jimbo la Serengeti limepata Mradi wa Mugumu, pale Mugumu mradi ule umepewa shilingi bilioni 20 na wakandarasi yupo *site* mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoendelea kukiomba ni fedha hizo ili kusudi miradi iweze kukamilika. Tunapoacha kupekeleka fedha hizi katika miradi tunaendelea kuongeza gharama kubwa, lakini pia kuendelea kuchosha wale wananchi kwamba mradi upo, lakini hautekelezeki. Ninaomba sana fedha zitoke, ziende kwenye miradi ili kusudi wakandarasi waendelee kupata hamu ya kuendelea kufanya kazi na siyo kuiongezea Serikali gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Mkoa wa Mara, nimesema tuna majimbo kumi na katika majimbo kumi, tunalo Jimbo la Bunda Vijijini, mpaka sasa Jimbo la Bunda Vijijini, tumepewa vijiji 30 ambavyo mpaka sasa vimefanyiwa upembuzi yakinifu, lakini Mwibara vijiji 24, upembuzi yakinifu. Tunaomba fedha ziende ili kusudi miradi ile itekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni lile lile na ninaendelea kuomba, ninaendelea kumwomba sana babu yetu Mheshimiwa Mwigulu, ampe fedha Mheshimiwa Aweso ili aweze kuangalia kwa jicho pili Mkoa wa Mara, akina mama wa Mkoa wa Mara, wanampenda sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wanaona kazi nyingi na kubwa anayoifanya katika mkoa wetu ili kusudi miradi ya maji iweze kukamilika ni fedha zinatakiwa. Tunakuomba kwa unyenyekevu mkubwa awaone wakandarasi waliopewa kazi katika Mkoa wa Mara, waweze kupewa fedha na kumaliza ile miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kusihi na kusema kwamba Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba sasa ataenda kuweka lile jambo la *pre-paid* ili kusudi wananchi waweze kulipa maji. Wananchi wamekuwa wakilalamika sana kwamba wanalimbikiziwa bili, sasa ikija hii *pre-paid* itatusaidia sana kwa wananchi wetu, ili kusudi yale malalamiko yaweze kupungua. Ninaendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri, yeye ni mchapakazi, yeye ni mbunifu na yeye ni kinara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba Wizara ya Maji, sekta ya maji haiwezi kufanya vizuri pasipo kuwaona wafanyakazi wa Mkoa wa Mara wa Wizara ya Maji. Wametekeleza vizuri na

wanaendelea kufanya vizuri. Meneja wetu wa Mkoa wa *RUWASA* yupo vizuri na watendaji wake wote wanachapakazi kuhakikisha Mkoa wa Mara, maji yanapatikana kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Marko Sallu, atafuatiwa na Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, ajiandae.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii na vilevile nikushukuru kwa kutuongoza vyema ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi alivyotumiminia miradi mingi Wana-Handeni ikiwemo miradi ya maji. Kwa kweli mama huyu kwa kule Handeni hatuna lingine la kumpa ila ni kumwombea dua nyingi Mwenyezi Mungu, ampe afya njema na umri mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana ndugu yangu Waziri Mheshimiwa Aweso na timu yake yote akiwemo Katibu Mkuu, ndugu yangu *Engineer* Mwajuma, Naibu Waziri, Mkurugenzi wa *HTM* kule kwenye *ground,* Mkurugenzi wa *RUWASA* wa Mkoa na Wilaya, kwa kazi kubwa wanayofanya tafsiri kwa vitendo ya maono makubwa ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye ardhi ya Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wana-Handeni tumepata miradi miwili mikubwa Mradi wa Miji 28 ambao mradi huu unaenda pale Handeni katikati na pale Bongi kuna tenki linajengwa la milioni 1,000,000, ambalo ukichukua na lile la zamani la lita 1,000,000 patakuwa na lita 2,000,000 kwa ajili ya kusaidia ile Handeni ya katikati, lakini kama haitoshi vilevile, tumepata mradi mwingine wa Handeni ya Mashariki wa shilingi bilioni 25, kwa ajili ya Kata za Mashariki na litajengwa tenki kubwa kwenye Mlima wa Chanika

Kofi, tenki lenye lita 2,000,000 ambalo litasambaza kwenye Kata zote za Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kata tano hazitafikiwa na hii miradi ikiwemo Kata ya Kang'ata, Kata ya Kwa Sunga, Kata ya Kwa Msisi, Kata ya Mkata na Kata ya Misima. Kata ya Misima ambayo Kijiji cha Msomera ndicho kipo ndani ya Kata ya Misima. Tunaishukuru Wizara ya Maji, imejitahidi sana kutupa visima na hata pale Msomera maji wanayotumia ni ya visima, lakini historia ya Handeni ilivyo wakati wa jua kali panaweza kutokea ukame ambao visima visiwe na maji ya kutosha. Hivyo, ninatoa ushauri kwa Wizara, watumie namna ya kuchukua maji kutoka Mto Pangani kuleta kwenye mradi mkakati wa Mama Samia, Mradi wa Msomera, ili pasije pakatokea janga ya ukame kama patatokea ukame mrefu tukakosa maji pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tuombe mradi unaotokea kwenye Mto Wami ufike pale Mkata, kwa sababu mradi ule ukifika Mkata utatusaidia kwenye mji wetu wa Mkata ambao ni Makao Makuu ya Halmashauri. Vilevile itasadia Kata ya Kwa Sunga na Kata ya Kwa Msisi ambapo maji yanaweza kwenda tu kwa mteremko *(gravity)*. Hiyo itatatua tatizo kubwa kwenye haya maeneo ambayo bado hayajafikiwa na hii miradi mikubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nipende kumshauri Mheshimiwa Waziri, malipo kwa wakandarasi, tunajua lipo nje ya uweze wake na Mheshimiwa Mwigulu, amsaidie Wakandarasi wapate malipo kwa wakati, ili miradi hii iishe kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nipende kutoa tena shukurani kwa Mheshimiwa Jumaa Aweso na timu yake ya Wizara, kwa kuwa namba moja kwenye Mradi wa *P4R,* ambao ni nchi 40 duniani zimeshiriki, lakini sisi Tanzania tumeibuka kidedea kwa kufanya vizuri sana. Hongera sana Bwana Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, ninashukuru sana. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, ajiandae.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara nyeti Wizara ya Maji.

Kwanza, kabisa nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema, lakini kutupatia ridhaa na kibali cha kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu, lakini pia niweze kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha anamtua ndoo mwanamke kichwani kama azimio lake ambalo alikuwa nalo toka mwanzo kuhakikisha mwanamke anafanya kazi akiwa ametulia, lakini asipate changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza kaka yetu, Waziri wetu Mheshimiwa Aweso, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanakwenda kupata maji na si maji tu, ni maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla kabisa sijaanza kuchangia ninaomba nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Bodi ya *MWAUWASA,* Mwanza baba yangu Gachuma kwa kazi nzuri anayoifanya na Mkurugenzi wetu wa *MWAUWASA* dada yetu Nelly Msuya, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, wanahitaji kupewa maua yao, wanafanya kazi nzuri katika Mkoa wetu wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza bajeti ya mwaka jana ya maji ilikuwa shilingi bilioni 750, mwaka huu bajeti imeshuka mpaka shilingi bilioni 627. Mahitaji ya maji katika miji yetu ni makubwa sana, sasa sielewi kwa nini bajeti hii imeshuka wakati maji bado yanahitajika na wananchi wetu wana hali ngumu ya maji na bado wana uhitaji mkubwa wa kupata maji na hayajawafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya haswa katika mkoa wangu wa Mwanza, ametuletea mradi mkubwa sana wa maji unaogharimu shilingi bilioni 71 katika Kata ya Butimba, Wilaya ya Nyamagana na kwenye Jiji langu la Mwanza. Mradi huu wa maji unakwenda kutoa lita 48,000,000 kwa siku, unakwenda kupunguza changamoto ya mahitaji ya maji kwa watu katika Jiji langu la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana kwa sababu hitaji la Mheshimiwa Rais lilikuwa ni kumtua ndoo mwanamke kichwani na tunapoenda kuona kwa vitendo Mheshimiwa Rais anakwenda kumtua ndoo mwanamke kichwani, tuna sababu ya kumpongeza na kumshukuru kwa kazi kubwa, ameweza kugusa pote, mwanamke aliyekuwa na shida ya maji anakwenda kuondokana na shida hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme tuna mradi wa matenki matano, yanayokwenda kujengwa Mwanza, niombe sasa matenki haya yanayokwenda kujengwa katika Kata ya Buhongwa, tenki lenye ujazo wa lita 100,000,000, lakini tunakwenda kujenga Fumagila lita 10,000,000, Nyamazobe lita 5,000,000, Kisesa lita 5,000,000 na Usagara lita 1,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana sasa matenki haya yatakwenda kuwasaidia akina mama kuondokana kasi kubwa ya kukosekana kwa maji na kuacha kulala, kuacha watoto wadogo wakiwa ndani na kuhangaika na maji, watakwenda kupata maji ya karibu na yatawasaidia sana wananchi wetu.

Kwa hiyo, tumesikia mradi huu sasa hii unatarajiwa kwenda kusainiwa na sisi kama viongozi wa wananchi tunawahamasisha wananchi wetu kwamba tutakwenda kuhangaika na mradi huu uweze kusainiwa haraka ili kuweza kwenda kuondoa changamoto ya maji katika Jiji letu la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili ninaomba sana kwenye mradi wetu, kuna bajeti mwaka jana tuliletewa hapa ya mradi mkubwa wa maji wa Kabangaja. Mpaka leo hatujajua ule

mradi umeishia wapi na nini ambacho kinaendelea. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, anapokuja ku-*wind up* hapa, aweze kunieleza mradi mkubwa wa Kabangaja umeishia wapi kwa maana tulielezwa wakandarasi wapo tayari wanakwenda kuzindua mradi ule na maji yanakwenda kwa wananchi wetu kuondoa kero kubwa ya wananchi wetu ya maji ili wananchi wetu waweze kupata maji na kero ya maji iweze kuondoka katika Jiji letu la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ule ulikuwa unakwenda kuondoa changamoto ya Kaskazini mwa Mji wa Mwanza, kwa maana ya kuna Kata ya Kahama, Buhongwa, Sangabuya na Kayenze ambazo zina changamoto kubwa sana ya maji. Kwa hiyo, kupitia mradi ule mkubwa wa maji wa Kabanyaja, ambao tulitangaziwa toka mwaka jana hapa. Tulikuwa tunajua changamoto ya maji Mwanza inakwenda kupungua kama siyo kuisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake watwambie, tunashukuru Serikali inafanya kazi kubwa sana, tumeletewa mabomba ya maji katika Mkoa wetu wa Mwanza, lakini kuna mabomba yapo katika Kata ya Idetemya, Tarafa ya Usagara yana zaidi ya miezi miwili hayajatandazwa. Sasa tuombe tuweze kujua tunaelezwa yatakwenda kuwekwa lini ili wananchi waweze kupata maji, kwa sababu kero kubwa ya maji inaonekana, na miundombinu bado haijatekelezwa, mama anatoa fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa na Mheshimiwa Waziri hapa fedha nyingi ambazo mama amezitoa watendaji wakafanye ile kazi, wananchi wanachohitaji ni kupata maji waweze kufanya kazi wametulia, akina mama ndio watendaji wa kubwa katika familia zetu, wanahangaika usiku na mchana wanashindwa kufanya majukumu mengine ambayo yanawahusu kwa sababu ya kero kubwa ya maji mama ameamua kulitoa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuombe watendaji wakashughulike na hilo, maji yaweze kufika majumbani ili kero kubwa ya maji iweze kutoka na wanawake tuweze kufanya majukumu mengine ya kulea familia na kufanya biashara zetu tukiwa tumetulia, siyo

tukikakaa tunawaza maji ya kwenda kuchota mbali. Tunaona mabomba tu yamewekwa yana zaidi ya miezi mitatu, miezi minne hayawekwi ili tukapata maji. Niombe sana viongozi hawa waweze kutusaidia kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa, ninaunga mkono ufungaji wa mita za malipo ya kabla ya matumizi. Tunaona kabisa tukilipa kabla ya matumizi tutalipa kile ambacho tunatumia tunakwenda kuacha na kero ya kusema… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, naomba robo dakika tu.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna kero kubwa sana ya kupata changamoto ya kulimbikiziwa bili za maji. Mimi ninaunga mkono hili la kulipa kabla kwa sababu nitalipa kile ambacho ninatumia na nyumba yetu itakwenda kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, majina ninayo mengi sana hapa, kwa hiyo, hata zile sekunde 30, leo zitakuwa hazipatikani kwa sababu tukizikusanya hizo zinamfanya mmoja achangie. Tunaendelea na wale niliokuwa nimewataja, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025.

Kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuhakikisha kwamba maji yanapatikana mijini pamoja na vijijini na ile ahadi yake ya kumtua mama ndoo kichwani inaweza kwenda kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru na kumpa pongezi kubwa na za dhati ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kweli nia yake na dhamira yake inaonesha ameamua kumtua mama ndoo kichwani na ndio maana Katibu Mkuu, ndugu yangu *Engineer* Mwajuma na kwa mwili wake tunasema sindano ndogo, lakini haishindwi kushona koti wala madera, mwanadada shupavu na makini. Tunaamini pia anaye Naibu Waziri, mama mchungaji wamepewa kazi hii na jukumu hili kama akina mama kuhakikisha wanaifikisha dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kutenga visima 900 katika nchi yetu ya Tanzania, kuamua kuja na programu hii maalum kabisa ya uchimbaji wa visima na uchimbaji wa visima hivi mfano umeanzia Mkoa wa Manyara na hususani Wilaya ya Hanang. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhehimiwa Waziri kwa sababu ninajua kumbe huwa shida inafundisha. Baada ya kupata mafuriko kule Mlima Hanang, alikuja na kukaa na sisi siku zote na ndio maana akapata hii akili ya kupata maji kwa kutumia visima vya muda mfupi na ndio maana ameweza sasa kupata ufumbuzi wa nchi nzima kwa kutoa visima 900. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi wakati anakuja kufungua programu hii pale Manyara, Wilaya ya Hanang, tulizunguka pamoja na yeye. Tumekwenda kule Gendabi, Dawar na Measkron. Tunamwomba sasa katika mradi huu, kwa sababu Wilaya ya Hanang na Mkoa wa Manyara ni sehemu ya mfano, hivyo tunamwomba ile miradi 30 ya Mkoa iweze kukamilika kwa wakati atuletee fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe sasa, kwa sababu katika Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Hanang ndipo ulipokuja kuanzia mfano wa visima hivi. Nimuombe atuletee hela kwa ajili ya Kata ya Measkron, Waama, Barjomot, Wandela pamoja na Gemunda.

Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza kazi kubwa ambayo inafanywa katika Mkoa wa Manyara, Wizara ya Maji, wameweza kukamilisha zaidi ya miradi 64 ya maji ambayo hakika inaenda kutatua kero kubwa ya wananchi, lakini pamoja na kazi hiyo kubwa imefanywa na Meneja wetu wa Mkoa na timu yako nzima kwa maana ya Mamlaka za Mji, *BAWASA*, Kiteto pamoja na Mbulu. Tunawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa kuhakikisha tunaendelea kutatua kero ya maji katika miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha tulikuwa tuna 50% tu ya maji kwa miaka mitatu lakini mama toka ameingia sasa hivi tumefika 70.2%. Hakika tunaona kabisa kero ya maji inaenda kutatuliwa katika Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri, kuna mradi mkubwa wa maji ambao unaendelea kutekelezwa, Mradi wa Maji wa Mogitu - Gehandu ukikamilika utakuwa ni suluhisho kubwa sana kwa wananchi wa Hanang, lakini siyo kwa Wana-Hanang peke yake, utavuka mipaka mpaka kwenda kutatua changamoto ya maji katika Mji wa Singida. Maeneo ambayo yatapata ufumbuzi wa haraka mradi huu ukikamilika ni pamoja na maeneo ya Mogitu, Gehandu, Gidagamowd, Warret, Sagara na Kijiji cha Moram Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakuomba uhakikishe kwamba fedha zinatoka kwa wakati ili kazi hii na dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kukamilika siyo tu kwa kujenga miradi, hapana. Tunachokihitaji ni pesa zitolewe ili wale watendaji wako waweze kuhakikisha kwamba maji yanafika kwa mwananchi na anaweza kuyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri, kuna mradi mkubwa sana, Mradi wa Bassotu, tunakuomba sana ule mradi ukikamilika utaweza kuwanufaisha na utaendelea kuwa ni msaada mkubwa sana kwa wakazi wa Wilaya ya Hanang pamoja na maeneo mengine. Mradi huu utanufaisha vijiji vya Bassoutu, Dajameda, Muungano na Wandela na tunaomba sasa mkandarasi apewe fedha ili aweze kuanza kazi hii na kuikamilisha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunakuomba sana sana Mheshimiwa Waziri, meneja wetu anafanya kazi kubwa sana, lakini tuna changamoto ya usafiri. Kwa hiyo, katika programu yako ya magari itakapokuja, basi hakikisha kwamba na sehemu ya Hanang inakuwa ni sehemu ya kwanza kupata gari hilo kwa sababu tumekuwa ni mfano wa kutekeleza miradi mingi na kusimamia fedha nyingi ambazo zinaletwa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuishukuru Serikali kwa kuendelea kuhakikisha imeendelea kutuletea miradi mingi ndani ya Mkoa wa Manyara. Ombi letu na msisitizo wetu, miradi mikubwa inaendelea kujengwa Mbulu, Babati Mji, Babati Vijijini, Simanjiro pamoja na Kiteto, tunaiomba sana Serikali kutupa na kutuidhinishia fedha hizo shilingi bilioni 19.9 ili kuweza kwenda kutatua changamoto ambayo imebaki ya usambazaji na kuhakikisha ile kauli ya mama tunaifikisha kwa vitendo. Miradi mikubwa ambayo tumeijenga, tunaifikisha kwa vitendo kwa wananchi kwa maji kutoka bombani na maji kufika kwenye majumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi katika miradi mikubwa ya kimkakati katika kuendelea kutatua changamoto ya maji kwenye Taifa letu. Hakuna asiyejua kwamba maji ni uchumi, maji ni uhai, maji ni kila kitu.

Mheshimiwa Spika, hongera sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako kwa kazi kubwa mnazozifanya na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHIKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu, nipende kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kule Chalinze, Pwani tunao mradi wa shilingi bilioni 17 ambao unaanzia Mlandizi mpaka Mboga. Mradi huu umekamilika na mwaka juzi mwezi Machi Mheshimiwa Rais alikuja kuuzindua mradi huu akiwa mwenye furaha kubwa sana, kwa sababu alikuwa anajua ndoto yake inaenda kutimia ambayo akiwa Makamu wa Rais siku zile na sasa hivi Rais kuhakikisha anawatua wanawake kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mradi huu ulidhamiria kuwanufaisha wakazi wa Mlandizi - Kibaha pamoja na Chalinze - Pwani. Kwa furaha aliyokuwa nayo Mheshimiwa Rais wetu siku ile ya uzinduzi pale pale alisema ataongeza ama atatoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya zoezi la usambazaji.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Aweso na Naibu wake kwa kazi wanayoifanya ni nzuri na ni kubwa, tangu mwaka juzi mradi umekamilika, zoezi la usambaji bado halijakamilika. Lengo letu hapa maji yasambazwe, yawafikie wananchi ili waweze kuyatumia, waweze kufurahia matunda ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anakuja kujibu atuambie watu wa Pwani ndani ya Chalinze tunataka kujua ni lini yale maji yatasambazwa ili yaweze kuwafikia wananchi hao, lakini tena Mheshimiwa Waziri ninakuomba tena ninakuomba sana, tunao mradi ambao upe kule Kibindu, mradi unaitwa Mradi wa Bwawa la Maji kwa Matumizi ya Binadamu ambao unagharimu kiasi cha shilingi milioni 969.

Mheshimiwa Spika, huu mradi unatekelezwa na *RUWASA* na ndiyo maana watu wote hapa waliosimama hapa jana na leo wanasema hebu ile *formula*, hebu ile kanuni ya mgawanyo wa fedha kati ya *RUWASA* pamoja na *DUWASA* ianze kwa uharaka sana kwa sababu *RUWASA* wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanafanya kazi kwa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, mimi niwapongeze sana *RUWASA* kule Chalinze wanafanya vizuri kwa sababu mradi huu wamefikisha asilimia 87. Kasi hii ni ndogo, tunaomba iende kwa kasi 13% ziweze kukamilika na yenyewe nitakuomba Mheshimiwa Waziri wakati unakuja hapa uweze kutueleza watu wa Kibindu - Chalinze ni lini mradi huu 13% zinaenda kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Pwani hatuna mseto, vijiji, vitongoji, kata, majimbo mpaka Taifa kura ni CCM, kura ni Mheshimiwa Dkt. Samia. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Aweso ukija hapa uje utuandalie maana sisi keshokutwa tuna jambo letu, tumebakiza muda mchache, tuna jambo letu. Kwa hiyo nitakuomba sana uje useme 13% lini unakamilisha na ni lini unaanza kusambaza ili wananchi waweze kuanza kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoizungumzia Chalinze, tupo vizuri, sisi tunakusanya shilingi bilioni 15 lakini tunatoa 60% kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pia tunawalipa Madiwani wenyewe kwa mapato yetu ya ndani, hatuna tofauti na majiji. Kama hivyo vyote havitoshi, tumejenga *round about* nzuri sana kuliko yoyote hapa nchini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu zote hizo Mheshimiwa Aweso hatutaki dosari ya ukosefu wa maji. Fanya hima hima tunahitaji maji, tunapoenda kipenga kikilia sisi maneno yetu ni machache, ndani ya masaa machache wanachukua, wanaweka waa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchache wa muda kwanza nianze kuwashukuru mashirika mawili ambayo yanafanya kazi nzuri kwangu Wilaya ya Bahi, Shirika la *Water Mission* ambao mpaka sasa wamenifanyia miradi karibu nane na ni fedha nyingi ambazo wamezitumia kutekeleza miradi katika vijiji mbalimbali.

Pili niwashukuru Shirika la *CMSR* ambao nao tunafanya nao kazi na wametekeleza miradi katika Kijiji cha Mkola, Kijiji cha Mkondai na wameendelea na maeneo mengine, kwanza niwashukuru sana sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi katika Wizara hii hoja zipo tatu; moja Wizara hii haipati fedha ya kutekeleza miradi, lakini pili, Wizara hii hailipi wakandarasi na tatu, Wizara hii miradi haikamiliki. Kwa hiyo, ni mambo hayo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la wakandarasi hasa wa ndani kutokulipwa, mimi nadhani Serikali ni lazima iangalie na isichukulie utulivu wa wakandarasi wetu, unyonge wa wakandarasi ikauchukulia kama ni jambo ambalo wanaweza kucheza nalo wanavyotaka au wanaweza kuwalipa wanavyojisikia. Mimi ninadhani ustaarabu huo, hebu tupate kama Serikali Watanzania wenzetu wanateseka, wanadaiwa kwenye mabenki na hawalipi riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakandarasi wa kigeni wanalipwa zile riba wanazoidai Serikali, lakini hawa ndugu zetu wengine hawaangaliwi na Serikali. Mimi ninachotaka kusema tusichukulie Watanzania wenzetu kwa utulivu walionao tukaona kama tunaweza kucheza kama tunavyoweza. Wizara hii haina chanzo mahususi cha fedha kama ambavyo tumetoka nyuma Wizara ya Ujenzi, *TANROADS, TARURA* wanaenda vizuri, Wizara ya Maji ipate

chanzo cha uhakika, la sivyo tutaenda hivyo hivyo na matatizo haya yataendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tunapata hela kwenye mafuta, iangaliwe namna kuwe na chanzo cha uhakika kama kitatoka kwenye mafuta basi *RUWASA* wawe na hela ya kutosha ili waweze kutekeleza miradi yao kwa sababu Wizara hii haipati fedha hata fedha tunayoitengea nyingi lakini inapata *almost* nusu ya bajeti yake, mimi nadhani Serikali jambo hili iliangalie na hili tuseme ni tatizo ambalo Wizara hii inalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana sisi kwenye Kamati tumeshauri sana na tumeshauri kweli kweli na tunaleta taarifa kwako, mimi nataka kusema sasa hivi jambo hili lichukue li-*internalize* ili uinusuru Wizara hii na ulinusuru Taifa kwamba huduma ya maji ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye miradi ambayo haijakamikia katika jimbo langu, Mradi wa Kata ya Ilindi, *RUWASA* walitoboa kisima, *TANESCO* wakapeleka umeme, kile kisima kimebaki hivyo hivyo. Wananchi wanashangaa, imekuwaje kisima kimetobolewa hatupati maji na umeme ulishapelekwa kwa hiyo ni kioja ambacho wananchi wanashangaa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kigwe mradi ule unaunganisha vijiji viwili, Vijiji vya Mapinduzi na Kigwe. Mradi huu mkandarasi alishapewa, haendelei na kazi kwa sababu hajapata fedha. Katika Kata ya Chali; Kijiji cha Chali Makulu, Chali Igongo, Chali Isanga, mkandarasi alishatekeleza mradi kwa shilingi milioni 800 hajalipwa hata senti tano, hata *advance payment* hajalipwa naye anadai na mradi umesimama. Ameshafukia bomba, shilingi milioni 800 lakini hajalipwa hata kidogo. Mradi wa Maji Kata ya Ibihwa, mradi ule mkandarasi amejitahidi kwa kiasi kikubwa naye amebidi asimame kwa sababu hajapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Mji wa Bahi maji yale ni maji ya chumvi na Serikali imekuwa inasema kila wakati kwamba italeta chanzo cha uhakika. Ninaiomba sana Serikali, mji ule hatuna maji ya uhakika na kama wanavyosema kwamba Farkwa inajengwa

na stori ya Farkwa hebu iishe na kama hamuwezi kuijenga basi msiiseme kabisa mpaka mkianza kujenga ndiyo muiseme. Kila mwaka Farkwa inajengwa, mimi ninataka niseme ninachoomba msiiseme kabisa mpaka mkianza kujenga ndiyo muiseme, lakini namna hii tumekuwa tunaisikiliza, mimi mwaka wa nne nasikiliza habari za Farkwa. Mimi naomba hebu Farkwa sasa msiitaje mpaka mkija kuanza kazi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la maji; habari ya gridi kama ambavyo wengine wanasema, maji ya kutoka Ziwa Victoria sisi tunayasubiri sana na Mji wa Dodoma unataka upate maji. Haiwezekani Jiji ambalo ndiyo Makao Makuu ya Serikali lisiwe na chanzo cha uhakika wa maji. Duniani kote majiji makubwa lazima uwe na maji ya kutosha kwa matumizi ya wananchi wako, kwa matumizi ya viwanda na hata ustawi wa mji ule na ndiyo maana bado kuna kusuasua kwa baadhi ya Taasisi za Kimataifa kuhamia kwenye mji huu kwa sababu hatuna chanzo cha uhakika cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nilitaka niliseme hili na ninataka niipongeze sana Mamlaka ya Maji hapa Dodoma, wamefanya kazi kubwa sana kutokana na wingi wa *influx* ya watu iliyoingia katika mji huu, lakini wamepambana kwa nguvu na kwa shida japokuwa hawana vyanzo vya uhakika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali waiangalie mamlaka hii, kwanza waisaidie maji ya kutoka Ziwa Victoria yaweze kufika kwa wakati ili mji huu uweze kustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallagyo Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafsi hii, kwanza na mimi pia niunge hoja mkono,

bajeti hii ya Wizara yetu ya Maji chini ya Mheshimiwa Waziri Juma Aweso.

Mheshimiwa Spika, cha pili nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kuwaletea wakina mama maji vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Solwa ni wanufaika wakubwa sana wa mradi huu wa maji wa Ziwa Victoria na moja katika mradi mkubwa sana ambapo aliwahi kuja Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango pamoja na Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso ulikuwepo pale Tinde kwenye lile tenki tulivyokwenda kulizindua, lile tenki ni kubwa sana, ni jambo la kumshukuru sana na kuishukuru Serikali yetu ya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, lina ujazo wa lita 1,150,000 lakini mradi ule mpaka sasa hivi ni vijiji viwili tu kwa maana ya Kijiji cha Jomu, Kata ya Tinde na Kijiji cha Didia ambao wanatumia maji hadi sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika *package* ya *Tinde package* ni vijiji 22 lakini nimwombe tu Mheshimiwa Waziri mpaka sasa hivi tunasubiri kibali kwa ajili ya mwendelezo wa vijiji vilivyobaki. Ni vijiji vingi, ni mradi mkubwa, ni fedha nyingi sana mmeweka Mheshimiwa Waziri. Ni suala la kumalizia tu ili wananchi katika vijiji 20 vilivyobaki waweze kupata haya maji safi na salama kwenye maeneo haya. Mimi ninakuaminia sana Mheshimiwa Aweso. Utakapokuja kujibu hoja yako hapa, hebu tupe neno la faraja kwa maana ya kwamba ni lini tunapata kibali ili vijiji hivi vianze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa visima vitano tulivyopata, kimsingi katika hivi visima vitano kwa kweli ni jambo la maana sana. Mimi katika Jimbo la Solwa katika Kata ya Bukene na katika Kata ya Usule ilikuwa *almost* zimeachwa kwa mbali sana. Sasa hivi visima vitano tumevipeleka pale na wanashukuru sana na tutaviweka kwenye Kijiji cha Ikonda, Kata ya Masengwa tutapeleka kisima kimoja, Ishororo, Igalamya na Masulula katika Kata ya Usule tunapeleka visima katika hivi vijiji pamoja na Kijiji cha Masekelo, Bukene na tuaondoa adha kubwa sana, ilikuwa

inanipa kazi kubwa sana na tunashukuru Serikali ya Mama Samia chini ya Mheshimiwa Aweso mmetupa hizi fedha kwa kweli ni mkombozi mkubwa sana katika hizi kata mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Masengwa package* ina vijiji 14, mkandarasi amefanya kazi kubwa sana mpaka sasa hivi ninavyoongea na wewe, lakini imebaki vijiji viwili kwenye Kata ya Mwamala kwa maana ya Kijiji cha Ibanza na Mwamala yenyewe, anasubiria malipo tu. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri mlipe huyu fedha zilizobaki amalizie vijiji viwili tu katika Kata ya Mwamala ili na wenyewe wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, vilevile tulileta maombi maalumu sana kwenye Kata ya Lyamidati na Kata ya Ilola. Hizi kata bado hamjatujibu vizuri, sina mashaka na wewe Mheshimiwa Waziri lakini mtupe tu majibu ya matumaini kwamba Kata ya Ilola na Kata Lyamidati kwa maana kuna vijiji vinne na kule kuna vijiji viwili vilivyobaki na yenyewe mtupe matumaini kwamba ni lini sasa angalau tuanze upembuzi yakinifu, watu wafanye upembuzi yakinifu, tulete hapa tupate fedha tuendelee na miradi katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, katika hivi vijiji na hii miradi Mheshimiwa Waziri wa Maji ukiniletea hizi fedha mpaka kufikia Desemba, 2024 au 2025 pale tunakwenda kwenye uchaguzi, nakuhakikishia Jimbo la Solwa litakuwa jimbo la kwanza Tanzania kufika asilimia kama si 105 katika vijiji 105 au 106 *out of 126* na litakuwa jambo zuri kuonesha ya mfano kwamba tunaweza, tuliweza na tunaendelea kuweza katika kuwapelekea Watanzania miradi ya maji siyo tu Jimbo la Solwa. Kama tumeweza katika jimbo la vijijini sana, jimbo la kijijini sana Solwa, tutaweza kupeleka vijiji zaidi ya 105 mwaka 2025 kufika mwezi wa sita au wa saba wakati tunaenda kwenye uchaguzi, tunashindwaje maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, mimi namwamini sana Mheshimiwa Waziri na ninamuamini Mheshimiwa Rais, kazi hii ni kubwa sana tukilinganisha adha ya maji iliyokuweko mwaka 2005, 2010 na 2015, tulikuwa tunaongea mambo tofauti sana, leo mtu katika Jimbo la Solwa, ukimwambia Solwa kuna watu wanahamia sasa

hivi kutoka maeneo mengine wanakuja kuishi Solwa kwa ajili ya miradi ya maji, yaani kwa kweli mimi sina zaidi ya shukurani na ninakuomba tu Mheshimiwa Aweso uendelee sana kuwa na moyo huo huo, ukimsaidia mama aendele kufanya kazi kwenye nchi nzima ikiwemo Jimbo langu la Solwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2005 wakati naingia Ubunge tulikuwa tunaongelea vijiji zaidi ya 25 tu ya maji, leo tunaongelea maji, sasa maji tunaongelea zaidi ya asilimia 71. Mheshimiwa Aweso akinipa kibali cha vijiji 22 na vile tukimaliza kule, tunakwenda asilimia 97, mwakani asilimia 100, tumalize kabisa, yaani inakuwa Jimbo la mfano katika Tanzania hii na kwa sababu kuu kubwa kabisa ni kwamba tumekuwa wanufaika wazuri katika mradi huu wa maji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe nakushukuru. Mheshimiwa Aweso umeandika hapo *notice* zako zifanyie kazi. Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza, samahani.

Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa hii nafasi, niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji ambayo ni Wizara nyeti kwa sababu hakuna mbadala wa maji na maji ni uhai.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kusema kweli miaka mitatu ambayo amekaa ofisini, amefanya

maajabu, ameboresha maisha ya Watanzania kwa kiwango kikubwa na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima pale Wizarani pamoja na wakuu wa taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli wameifanya na tunaona na tumeshuhudia namna gani wameendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi upatikanaji wa maji mijini uko 90% na Ilani ya Uchaguzi inasema kwamba mwaka 2025 tuwe tumefikia 95%. Pia vijijini wamefikia hatua nzuri ya 79.6% wakati Ilani ya Uchaguzi inasema 85%. Kwa kweli ni kazi nzuri imefanyika na tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri na tunamfahamu ni kijana mpole, msikivu na mchapakazi wa uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mikubwa, kwa mfano, kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria mpaka sasa hivi umefika katika Jiji la Tabora ambayo ni hatua kubwa sana. Tulikwenda kule wakati wa ziara ya Kamati, tukashangaa kuona Tabora maji ni mengi kabisa, lakini siyo Tabora tu, Shinyanga na Simiyu, kote maji ya Ziwa Victoria yamefika. Tunaipongeza Wizara kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya maji Jimboni kwangu; nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita. Nimepata mradi wa shilingi bilioni 520 kwa ajili ya Jiji la Arusha na viunga vyake, na sisi jimboni kuna vijiji vya Mbuguni, Makiba, Shambarai Burka na Kikwe, vimetengewa shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kule bomba linakopita wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri, zile fedha zimetolewa kidogo sana, juhudi ifanyike zitolewe fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza huu mradi. Pia nashukuru sana kuna mradi wa Patandi ambao unagusa kata mbili za Nkoarisambu na Akheri. Mwaka 2019 nilikuja kwako tukaondoka mguu kwa mguu mpaka kwa Mtendaji Mkuu wa *RUWASA*, baadaye ule mradi umekuja

kutekelezwa kwa shilingi bilioni 3.2. Nashukuru sana kwa mradi huo na huo mradi unanigusa kwa sababu uko katika kata yangu, nakushukuru, lakini uko kwenye *final stage*, kuna changamoto kwenye vyanzo vya maji, vinahiotaji *refinement*. Maji kule yaningia na udongo, yanakwenda kwenye matanki, mwisho yanaziba.

Kwa hiyo, naomba kwamba hatua zichukuliwe haraka haraka kwa sababu karibu tunaukabidhi. Vile vyanzo vinatakiwa virekebishwe na kuhakikisha kwamba maji ambayo yanakwenda kwenye matenki ni masafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninashukuru kwa Mradi wa Imbaseni, Maji ya Chai na Kikatiti ambao ujumla unafikia shilingi bilioni 6.1; huu mradi unakwenda mpaka Samaria. Kwa kusema ukweli, wananchi kule wana shida kubwa sana ya maji sasa hivi, mradi unaenda kwa kusuasua, nikuombe Mheshimiwa Waziri, mpeleke fedha ili mkandarasi aendelee kufanya kazi kwa sababu kuna kipindi alishindwa kuendelea na kazi akahama kwenye *site*. Utakuta wakandarasi wetu hawa wanakopa benki, sasa wanapokopa benki tunawafanya wanakuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine wa Kata ya Uwiro nyuma ya mlima ambao nao unaendelea wa shilingi bilioni nne, nadhani mpaka sasa zimetengwa shilingi bilioni mbili. Tunaomba pia fedha zitengwe za kutosha kwa sababu ule ukanda una shida sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mlima Meru una maji mengi sana, lakini maji yake hasa kwa upande wa Mashariki yana *fluoride* nyingi. Mheshimiwa Waziri nakuomba tujipange kuhakikisha kwamba tunafuata maji mengi kule mlimani hata kama yana *fluoride* kuna wahisani ambao wako tayari kutusaidia kuyatibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikutana na mmoja kutoka Korea akasema sisi tujipange, tutafute sehemu ya kujenga tenki, halafu tuchukue maji mengi kama lita milioni 24 ili waingize mashine za kutibu hatimaye wananchi wa zile Kata za Mashariki za Ngarenanyuki, Ngabobo, Reguluki, Maruvango, King'ori, Malula hadi Majengo wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingine midogo midogo tunaendelea kushukuru kama Mradi wa Kijiji cha Nkure, shilingi milioni 502 ulitekelezwa na sasa hivi wananchi wanapata maji na wananipigia simu wananiambia wanaoga mara tatu kwa siku. Wakimaliza kula wanaoga kwa sababu maji ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu Mradi wa Patandi walipoufungulia tu mabomba yalianza kupasuka kwa sababu kuna miundombinu ambayo hawajaibadilisha. Kwa hiyo, nakukumbusha kwamba uwaambie wabadilishe miundombinu yote ili maji yasiendelee kupotea, kwa sababu upotevu wa maji ndilo tatizo kubwa ambalo linatusumbua Wizara ya Maji... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nasikia kengele ya pili imeshalia.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukrani. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nashukuru kwa ushirikiano ninaoupata kutoka kwa wananchi wa Urambo na familia yangu ambao unanipa nguvu ya kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Urambo nikiulizwa shida ya kwanza Urambo iwe usiku wa manane au asubuhi nitasema ni maji, halafu ndiyo zinafuata shida zingine, pengine upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, masuala ya

umeme na mengineyo kama barabara, lakini la kwanza ni shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msambazo wa maji Urambo ni 24%. Nimeona hapa wenzangu wanatamba hapa sijui asilimia ngapi, mimi ni 24. Sasa hii ndiyo inadhihirisha kabisa kwamba shida ya maji ni kubwa, lakini ni kwa sababu mbalimbali ikiwemo pia na asili ya miamba na kadhalika, lakini shida kubwa ya Urambo ni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu kwa kutambua kwamba shida ya kwanza ya Urambo ni maji na ndiyo maana katuletea miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo upatikanaji wa maji kutoka *Lake Victoria* kwa kupitia ile miji 28, pia uchimbaji wa Bwawa la Kalemela ambalo litasaidia kusambaza maji kwa vijiji 17 lakini pia na huu msaada mkubwa ambao tumeupata sasa hivi ambao tumeambiwa tutapata maji katika vijiji vitano ikiwamo Mpigwa, Kasisi, Kapirula, Mwinyi na Chekereni. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Rais, nchi yetu ni kubwa, kwa hiyo, anapotuletea sisi miradi mikubwa kama hii tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzuri wake Mheshimiwa Dkt. Samia naye akamteua Mheshimiwa Waziri mchapakazi. Hongera sana Mheshimiwa Aweso, *Engineer* Mwajuma na watendaji wote walioko katika Wizara yako, wakiwemo pia watendaji wetu wa *RUWASA* na *TUWASA* Tabora; *Engineer* Kapufi, Mayunga na hata wa kwangu Ngedei aliyeko Urambo wanafanya kazi kubwa. Mheshimiwa kazi mnaifanya, hongera. Ulinifurahisha zaidi ulipokuja wewe mwenyewe kuja kuangalia jinsi ambavyo miradi inaendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa shida ni kubwa, mimi kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya wananchi wa Urambo, naomba sasa mfuko wa maji uje. Bwawa lile limeanza kuchimbwa, lakini fedha hakuna. Tunajua kwamba lile bwawa litagharibu shilingi bilioni 5.9 maana yake ni karibu shilingi bilioni sita, maji hayawezi kupatikana kama fedha hazitapelekwa. Kwa heshima na taadhima naiomba Serikali ilete fedha za Mfuko wa

Maji ili zisaidie uchimbaji wa lile Bwawa la Kalemela. *(Makofi)* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mimi mweyewe sijui kama ulishaona, naweza kukutumia kwenye mtandao, kila wakati nakwenda kuchungulia yale mabomba yanayoleta maji kutoka *Lake Victoria,* najua mvua ilichelewesha, lakini sasa hivi mvua imesimama, naamini mitambo itakwenda kule, kwa sababu kila siku kupiga picha kwenye mabomba haisaidii. Tusaidie maji yafike halafu wewe mwenyewe uje ufungue Urambo siku yenyewe tufurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana ule Mradi wa *Lake Victoria* isiwe hadithi tu tunaomba sasa ikamilike ili na sisi tufaidike kutokana na matatizo makubwa ya maji tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhaika kama nilivyosema hii miradi miwili ya kimkakati, la kwanza maji kutoka *Lake Victoria* tunakusihi huu mradi ukamilike na Bwawa la Kalemela ambalo kama nilivyosema hapo awali, litasaidia vijiji 17, tunaomba fedha ziletwe ili tuweze kukamilisha hilo na hivi vijiji sina wasiwasi, naamini kabisa utaleta fedha ili hivyo vijiji vitano vikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Urambo wana imani na Serikali yao na kama nilivyosema pia wana imani na wewe mwenyewe na utendaji kazi wako. Sasa tunaomba basi haya maji siku yenyewe, ukisimama hapa hebu tupe matumaini kwamba wananchi wa Urambo tulieni huko maji yanakuja tarehe fulani. Je, unaweza ukasimama ukasema hivyo? Ukatoa kauli ya Serikali kwamba ifikapo angalau mwezi fulani ninyi mtapata maji kutoka *Lake Victoria* ili na sisi tufurahie maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kabla maji yenyewe hayajafika tunaomba basi na mtandao wenyewe, yakishafika pale yanakwenda wapi. Tunajua yatakwenda kilometa 12 pande zote mbili, lakini msambazo wenyewe ule, tunaomba na maandalizi yaanze kufanyika. Tusingoje mpaka maji yakaja halafu ndiyo tukaanza kuweka msambazo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba sana hata maandalizi ya msambazo yaani jinsi maji yatakavyosambazwa kwenda sehemu mbalimbali basi yawe yamefikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba niishukuru tena Serikali, lakini sina haja ya kurudia shida yetu kubwa, maji ndiyo uhai na ndiyo tunayoyategemea kutoka kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo kwa kweli sina la zaidi ya kusema naipongeza Serikali yetu, nakupongeza na wewe Mheshimiwa Waziri ambaye utahakikisha kwamba maji yanafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli ametuheshimisha sana sisi Watanzania na ametuheshimisha sana sisi wanawake, kwa hiyo, kwa heshima aliyotupatia, sisi Watanzania wote tutamlinda na tutahakikisha kwamba kura zake zote zinapatikana kwa wanawake, wanaume, watoto na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wetu Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri sana, nimpongeze Mheshimiwa Maryprisca, tumefanya naye kazi sana katika Kamati yetu na Mheshimiwa Kundo, tunaamini kabisa muunganiko huo sasa utaleta kasi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa hakufanya kosa kumpandisha Katibu Mkuu wetu *Engineer* Mwajuma, lakini pia kumteua *Engineer* Agnes. Kwa kweli, mimi nasema kwamba pamoja na watendaji wote nawapongeza sana. Sasa upele umepata wakunaji na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba Wana-Mbeya wakulinde kwa sababu umetuheshimisha kuwa Spika wa Mabunge ya Dunia, ikiwezekana wakulinde na wakuheshimishe kwa heshima uliyotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijawatendea haki kama sitawapongeza Mtendaji Mkuu wa *RUWASA* - *Engineer* Kivegalo na Meneja wa *RUWASA* Iringa - *Engineer* Joyce, wamekuwa msaada sana katika utekelezaji wa miradi yetu ya maji. Pia Mkurugenzi wa *IRUWASA* - *Engineer* Pallangyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *IRUWASA* imekuwa mamlaka ya kwanza nchini kwa huduma bora za maji mara mbili mfululizo na ya pili kwa maji na usafi wa mazingira kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, ametuheshimiwa sana mkoa wetu wa Iringa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa una vijiji 360, lakini vijiji 303 tayari vimepatiwa maji safi na salama, vijiji 57 tu ndivyo ambavyo bado havijapata maji. Kwa hiyo, tunaamini kwa ile programu ambayo imewekwa ya vijiji 900, vijiji 25 vitapunguza kabisa vijiji vyetu katika mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyo vijiji ambavyo vumeshaanza kuwa na miradi ya maji kama Ifua, Wotalisoli, Kimara, Wambingeto, Mtandika, Ikula, Kihesa, Mgagao, Mkaranga, Ng'ang'ange, Igowole, Mgololo, Mkumbinyi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana kabisa na Kamati yetu kutoridhishwa na Serikali kupunguza bajeti ya maji kwa kiasi cha shilingi 137,714,253,000, sawasawa na asilimia 18.4. Kwa kweli mimi nawaomba kabisa na Waheshimiwa Wabunge wengi

wamechangia, siyo haki na siyo halali bajeti ya maji kupunguzwa na ikiwezekana basi ibaki kama ilivyokuwa ili kazi hii ya kumtua ndoo mwanamke kichwani iweze kufanyika vizuri zaidi na wanawake wote waweze kutuliwa ndoo kichwani na vijiji 2,000 ambavyo bado viweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu itoe tamko kuhusu zile taasisi ambazo zinadaiwa na Wizara ya Maji, basi ziweze kulipa madeni yake kwa sababu mpaka kufikia Desemba, 23, madeni ni shilingi bilioni 26 na mwaka huu bado hatujaweka idadi yake itakuwa shilingi ngapi na ikiwezekana basi hizi taasisi ziwekewe mita kama za LUKU, maana yake bado zinadaiwa na zilipe madeni yote ili miradi iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya wakandarasi; yaani malipo ya wakandarasi hayaendi kwa wakati, ni kwa sababu hiyo kwamba mnapunguza bajeti ya maji na vilevile madeni hayalipiki, sasa mnategemea Wizara ifanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile wakandarasi wetu wa ndani tunakuwa hatuwajengei uwezo, kwa sababu wanatakiwa tuwajengee uwezo waweze kufanya vizuri zaidi. Miradi mingi inapokuwa haikamilika kwa wakati, gharama za miradi zinakuwa zinaongezeka. Kwa hiyo, ninaomba hili lichukuliwe kwa umakini zaidi kuhakikisha kwamba wakandarasi wanalipwa malipo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza sana Katibu Mkuu wetu kwa Programu ya Wiki ya Maji, mwaka huu aliheshimisha wanawake na katika Mkoa wetu wa Iringa, uchimbaji wa Kisima cha Mtandika, kwa sababu pale Mtandika wananchi walikuwa wanatumia maji ya Mto Lukosi, walikuwa wanapata shida sana, wengine wamekuwa walemavu na wengine wamepoteza maisha. Kwa hiyo, tunakushukuru sana wa hii Programu ya Wiki ya Maji kwamba kila mwanamke atafute mradi na apeleke ili kuheshimisha Wiki ya Maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi letu pale Mtandika tayari kisima kimeshachibwa, kwa hiyo, tukipata tenki la lita 100,000 utakuwa umesaidia kijiji kizima... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Taletale na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, yeye ambaye ametupa uzima kwa siku ya leo na kuwepo katika Bunge hili, kutekeleza majukumu yetu ya kawaida ya kuwakilisha wananchi na kuhakikisha kwamba Taifa letu linasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisiache kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na jinsi ambavyo anaendelea kuliongoza Taifa letu kwa umahiri mkubwa na tunaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwamba suala la maji ni suala muhimu sana katika maisha ya binadamu na katika jambo ambalo tunatakiwa tulitazame sana sasa ni suala la kuondokana na kilio cha maji mara kwa mara. Katika kipindi hiki ambacho tunaelekea tunakokujua suala hili linaweza likaja kutuletea matatizo makubwa kwa sababu hatujalitilia maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ni kwa sababu gani? Kama tumekwenda kupunguza bajeti ya maji ina maana malengo yetu

yale ambayo tumetegemea kuyafikia hatutoweza kuyafikia kwa kiwango ambacho kinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa wakandarasi waliopo kazini; katika jimbo langu la Arumeru Magharibi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso kwa sababu kuna mradi mmoja ambao ulianzishwa na Mheshimiwa Rais, ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Magufuli. Mradi huu unaenda, lakini unakwenda taratibu mno. Changamoto iliyopo kwenye mradi huu ulianzishwa kwa sababu wananchi wa Oldonyosambu na vijiji tisa ambavyo ni Vijiji vya Lemong'o, Lemanda, Oldonyosambu, Engutukoit, Ol-sinoni Kati na Oldonyowas. Vijiji hivi vinaathiriwa sana na *fluoride* kwa sababu maji yanayopatikana ni *fried. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanapinda miguu, wananchi wanavimba vichwa, wananchi wanapinda migongo, ukifika kule utaona huruma. Mheshimiwa Waziri nikuombe wewe mwenyewe umefika katika mradi huu, umeona wananchi wanavyoteseka. Makamu wa Rais amepita pale wananchi wamemzuia, ametoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri mradi huu wa *fluoride* wa Oldonyosambu wa vijiji tisa kwa kweli wale wananchi wanateseka na wewe ni shahidi, nimekulilia mara nyingi, mpaka sasa nasema labda nije ofisini kwako nipige magoti, nitembee, nitambae kwa magoti pale ofisini ili muweze kunielewa kwamba wale wananchi wanataka kunitoa roho na ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri suala hili alichukulie kwa kiwango cha uzito wa hali ya juu na Naibu Waziri wako pamoja na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuna mradi wa Olmulo; mradi huu unahudumia vijiji karibu tisa mpaka kijiji kimoja cha Simanjiro kwa Mheshimiwa Sendeka. Wananchi wote hao kwa ukanda huo hali siyo nzuri, mkandarasi alikuwepo *site* amepewa huo mradi, amekaa kwa muda, lakini sasa hivi hayuko *site* tena kwa kipindi cha miezi minne na ni kwa sababu hakulipwa

fedha kwa wakati na ni kwa sababu ya uhaba wa fedha. Kwa hiyo, naomba hili suala la mradi huu pia wa Olmulo katika Kata ya Oljoro ambayo inaenda kupitia Kata ya Laroi mpaka Simanjiro nao uangaliwe Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi unaohudumia kata inayotoa maji na yanayokwenda katika Jiji la Arusha ni Kata ya Kimnya, Kata ya Kimnya kupitia Kata ya Tarakwa kupitia Kijiji cha Siwandeti na Kiranyi yenyewe hayo maeneo yote yana *population* kubwa yaani ina watu wengi mno. Sasa wale wananchi wa ukanda huo hawapati maji. Mheshimiwa Waziri, nikuombe nimezungumza na wewe ukaniambaia tuchukue hatua ya dharura ukasema basi utatutafutia shilingi milioni 500 ili hatua ya dharura kabla tukisubiri mradi mkubwa. Basi utusaidie hiyo shilingi milioni 500 ipatikane ili wale wananchi wa Kimnya wapate maji, wananchi wa Siwandeti wapate maji na wananchi wa Tarakwa wapate maji, kwa sababu kwa kweli hilo eneo lina watu wengi sana. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, sana, sana tunaelekea kubaya na hilo jimbo unalielewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mradi wa Kata ya Kiutu; tumeleta andiko kwa ajili ya kuomba Kata ya Kiutu ipatiwe mradi wa maji, lakini kwa bahati mbaya sana hatukuweza kufanikiwa kupata fedha. Suala la Kata ya Bangata na vijiji vyake vya Midawe, Sasi na Bangata yenyewe bado ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kuhusu suala la *prepaid meters;* hizi *meter* ni muhimu sana zikifungwa hasa kwenye taasisi za Serikali kwa sababu hawalipi maji na ndiyo maana hata *RUWASA*, *AUSA* hawawezi kujiendesha katika kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana hizo mita mzifunge kwenye hizo taasisi kwa sababu mtakata mzizi wa fitina. Mkifunga hizo mita mtakusanya pesa nyingi sana na kama hawalipi basi watabaki bila maji, kwa sababu wanaona kwamba ni Serikali sasa hawalipi maji. Naomba sana hizi mita zifungwe katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nimwombe Mheshimiwa Waziri haya niliyoyasema hebu ukifika leo mbele ya Siwa hiyo hapo utuambie sisi wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi ni lini miradi hiyo itakamilika hasa huu mradi wa *fluoride* na miradi mingine hiyo midogo midogo niliyoitaja na mikubwa, kwa sababu kwa kweli hali ni mbaya na ni tete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu ya muda niombe kushukuru sana viongozi wangu wote wa *RUWASA* Mkoa, *Engineer* Makaidi na wengine wote ambao wanafanya kazi nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Haji Makame Mlenge ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, *Rabbish rahli sadri wa yassirli amri wah lul uqdatan min lisaani, yaf kahu kauli*.

Mheshimiwa Spika, nimesema nianze na dua kwa ajili ya kuiombea Morogoro Kusini Mashariki, lakini kwa ajili ya kumwombea Mheshimiwa Rais na kukuombea wewe pia kwenye kila tunachokiongea kiwe chepesi, ulimi wangu ufike kwa Mheshimiwa Rais na ufike vizuri kwa kaka yangu na ndugu yangu Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme Wizara ya Maji sasa hivi ina raha sana, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Wizara ya Maji leo hii ametuletea Katibu Mkuu mwanamama, mwepesi, mwelewa, *Hajat* mtarajiwa; ametuletea Naibu Katibu Mkuu, mwanamama, mwepesi, mchungaji, lakini pale mbele kuna Waziri sijui huyu ni Sheikh. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niipongeze Serikali kwa kutuletea mradi mkubwa wa Morong'anya, mradi ambao leo hii sisi wakazi wa Tomondo tumesahau kabisa shida ya maji, wakazi wa Mikese tunakwenda kusahau shida ya maji. Vilevile niipongeze Wizara kwa kutuletea mradi wa maji wa shilingi bilioni nne kwenye kata

yetu ya Mkambarani, lakini pia nikuombe kwenye hili hapa, leo hii sisi wakazi wa Tegetero ambao ndio wenye ule Mradi wa Morong'anya ambao unatokea kwetu, Mheshimiwa Waziri ulikuja na ukatoa maagizo kwamba wakazi wa Tegetero tupate maji mpaka leo hii imekuwa historia, hatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, mimi sitaki nimwambie twende wote Tegetero kwa kufika ulishafika naomba upeleke pesa ili Wana-Tegetero wapate maji. Kwa kupitia huu Mradi wa Morong'anya leo hii Mikese ina maji, lakini kuna changamoto. Nimwombe Mheshimiwa Waziri azungumze vizuri na wataalam wake, Kata ya Mikese ni kata yenye watu wengi sana. Kwa hiyo, kwenye utaratibu wa kuyagawa haya maji yanayotoka Morong'anya twende tukaangalie jinsi ya wakazi wa Mikese ili wapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna changamoto ya mvua, imekwenda kuharibu miundombinu kule juu kiasi cha kwamba mpaka sasa watu wa Mikese hawapati maji. Mheshimiwa Waziri jiulize, wengine wana nyota kama za kwako, wana wake wawili wawili wanakoga saa ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliongee hili kwa huzuni sana, kwenye Kata ya Mkambarani hii kata ametuletea mradi wa maji wa shilingi bilioni nne, lakini ni kama umesimama, hatuelewi shida ni Mkandarasi, hatuelewi shida ni ninyi hamjapeleka mchele pale na mchele ni pesa, hawajapeleka pesa pale. Sasa mimi niombe, hii miradi isiyopelekewa pesa sisi tunakuwa tunapata changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye kata yetu ambayo kuna shida na ndiyo mlango wa maji kuelekea Mkoa wa Dar es Salaam, Kata na Tarafa nzima ya Ngerengere. Nitoe mfano kwenye Kata ya Tununguo, tuna maji mengi kwenye Kata ya Tununguo, lakini ninavyozungumza kwamba tuna maji mengi kwa sababu tuna Mto Mvua pale, tunaishia tu kuliwa na mamba, lakini wananchi wa Kata ya Tununguo hawajawahi kuona maji ya bomba tangu Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasifia Mradi wa Morong'anya umesaidia zaidi ya vijiji 24 upande wa Tarafa ya Mkuyuni, lakini Tarafa ya Mikese inapata mradi kidogo, Tarafa ya Mikese imepata huu mradi wa Kata ya Mkambarani sawa, Kata na Tarafa nzima ya Ngerengere haina maji.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili nitaomba jambo moja na nitamwomba Mheshimiwa Waziri mimi na wewe twende kwenye Tarafa ya Ngerengere, Wanangerengere wana shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa ule Mradi wa Kidunda, leo hii Kidunda tuna uhakika kwamba wananchi wa Dar es Salaam watapata maji, lakini wale ndugu zetu wa *DAWASA* hawalipi madeni pale kwetu. Kwa hiyo, tuna watu ambao tunawafugia maji halafu wanashindwa kutufikiria. Mheshimiwa Waziri leo hii mimi nikikupeleka Ngerengere nikakuchotea maji kwenye bomba huwezi kunywa wewe na huwezi kunywa kwa sababu ni maji ya chumvi isiyopita shingoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe kikubwa hawa watendaji wetu kwa mfano tu niseme kitu kidogo, mtendaji wetu anayehusika na maji wa Wilaya, mimi nilinunua *Land Rover* yangu mpya nikaipa Wizara ya Maji pale mkoani kwangu ili watembee. Gari imekufa, *DMO* wangu hana gari, anaomba gari kwa Mbunge ambaye sasa hivi gari yangu iko juu ya mawe. Nikiitazama ile gari kama natazama sura ya Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe ndugu yangu na kaka yangu, ninamuheshimu sana na anajua kwamba wanasema; "Mwembe wa uwani, nyani hatambi" kwako mimi sitambi sana. Mheshimiwa Aweso nikwambie wale watu wanataka kupewa pesa, wale watu wanataka kusaidiwa kwenye utaratibu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini hili lina umuhimu sana kwa ndugu yangu Mheshimiwa Aweso na Wizara kwa ujumla, nimeona bajeti yako wakati unasoma jana, watu wanataka kuomba eti pesa ipungue, jamani ninyi wasomi mpaka

mnatuangusha sasa hivi, bila maji kuna nchi kweli! Watu tunapambana eti wasomi mmekaa, mmepiga mahesabu huko Wizara ya Maji ipunguziwe pesa kweli, tutafika sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mheshimiwa Rais kumtua mama ndoo kichwani, dhamira ya Mheshimiwa Rais kutusaidia sisi watu wa chini huku. Kama leo hii mnakaa na mnapiga mahesabu yenu eti Wizara ya Maji ipunguziwe pesa, jamani. Mheshimiwa Aweso amekuja hapa nywele mpaka hapa, leo hii anapata kiwalaza kwa sababu ya vitu kama hivi. Haiwezekani tukae chini, wasomi mnakaa mnakutana kabisa eti mnawaza Wizara ya Maji ipunguziwe pesa, hii dhalili kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kutekeleza miradi ya maji nchini kwa kutoa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Waziri wa Maji, mwanangu Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Kundo kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia nawapongeza watendaji wote wa Wizara ya Maji bila kumsahau Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Mpanda, Rehema Nelson ambaye anakaimu kwa kazi nzuri anazozifanya sasa pale Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mpanda una matatizo ya maji na maji yamekuwa yakitoka kwa ratiba kwa miaka yote. Tunayo maji kutoka *Ikorongo One*, *Ikorongo Two* pamoja na Konuge, lakini

maji hayo hayatoshi. Tuna mradi wa maji ya miji 28 tunashukuru Serikali imetoa pesa pale takribani shilingi bilioni 22 tunasema ahsante sana kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa maji na mradi huo unaendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna wananchi ambao walipisha ule mradi katika eneo lile la Bwawa la Milala takribani wananchi 520 wana madai yao. Mheshimiwa Waziri Aweso nilikuwa naomba ushirikiane na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili muweze kuwalipa wananchi hao kwa sababu wamepisha huu mradi wa miji 28.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mkoa wetu wa Katavi suluhisho kubwa la maji ni kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri tunaomba uweze kulichukulia hili kwa uzito, uweke *consultant* ili waweze kufanya *research* zao na maji yaweze kuvutwa kutoka Ziwa Tanganyika ili yaweze kusaidia Mkoa wetu wa Katavi pamoja na Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Kigoma na vijiji vinavyopita kwenye mkoa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kutumia pia nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Tanganyika ambao wamepatwa na janga la mafuriko kule kwenye Kata ya Karema, Kata ya Ikola, Kata ya Kapalamsenga, Isengule pamoja na vijiji vya pembezoni wamepata matatizo ya mafuriko, maji yamejaa kwa sababu wako pembezoni mwa Ziwa Tanganyika na nyumba zao zimebebwa na maji. Serikali sasa hivi imewapimia viwanja vingine kwenye eneo lingine ambalo liko juu kama mlimani.

Mheshimiwa Spika, eneo hilo halina maji, halina miundombinu ya maji. Ninaomba pesa zilizoombwa kwenye Wizara ya Maji ziweze kuwapatia kama sijakosea ni takribani shilingi 3,000,600,000; ninaomba sana na niko chini ya miguu yako Mheshimiwa Waziri na mwanangu uwape kwa sababu wananchi wale wanateseka, hawana mahali pa kukaa wameweka tu maturubai, maana yake miundombinu yote ya maji kwenye kata hizo nilizozitaja pamoja na vijiji imemezwa na maji, Ziwa Tanganyika limejaa.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa mama mmoja natoka Mkoa wa Katavi tunapenda sana kazi zako na wewe ni msikivu tunaomba hili suala ulichukulie kwa uzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni ulipaji wa wakandarasi ambao wanafanya kazi za maji kwenye mkoa wetu wa Katavi, lakini pia na sehemu nyingine waweze kulipwa kwa wepesi ili wafanye vizuri zile kazi za maji, kwa maana yake mtu anapochukua *tender* kwenye Wizara ya Maji anategemea afanye kazi ili aweze kulipwa. Ninaomba wawe wanaharakishwa kufanyiwa malipo yao ili waweze kutekeleza kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, mkoa wetu wa Katavi katika sensa ya mwaka jana watu wameongezeka mara mbili, baada ya kuongezeka mara mbili takribani wakazi wa mji ule wa Mpanda lakini pamoja na Mkoa wa Katavi wameongezeka siyo kama wakazi wa miaka ya nyuma na ndiyo maana tunauhitaji sana wa maji kwenye mkoa wetu wa Katavi na tunauhitaji sana, sana wa kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunakwenda kujenga gridi ya maji kama ulivyosema mwanangu kwenye ripoti yako. kutakuwa na gridi ya maji ya Kitaifa ambayo kuna maji kutoka Mkoa wa Katavi, Ziwa Tanganyika yatakwenda kuihudumia hii mikoa mingine, lakini pia gridi ya maji nyingine itatoka Ziwa Victoria ambayo ndiyo maji yamekuja mpaka Tabora nafikiri na mito mingine kutoka Ruvuma. Baadaye, takribani tunategemea baada ya miaka kumi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, amina.

Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa bajeti hii ya Wizara ya Maji. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai kufika hapa tukiwa wazima. Aidha, nimshukuru sana na nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utendaji wake mzuri na nimtie moyo, nimwambie asishughulike na wale ambao wanamsema vibaya ndani ya mitandao, yeye apige kazi, Watanzania wanaona kazi ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niendelee kuipongeza Wizara kupitia Waziri wetu Mheshimiwa Aweso. Wizara hii inafanya kazi kubwa sana, Wizara hii inastahiki kupongezwa na Wizara hii, Waziri huwa ana msemo anasema; "Wizara hii ilikuwa ni Wizara ya kero, sasa ni Wizara ya faraja." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo naomba nianze na maneno yafuatayo; maji ni uhai, maji ni Uchumi na maji ni mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeanza maneno haya lengo langu kuu kuonyesha ni nini umuhimu wa maji. Bila maji hakuna uhai, bila maji hakuna uchumi na bila maji mazingira hayapo. Kwa hiyo, unarudi pale kwamba hakuna uhai. Kwa hiyo, maji ni muhimu sana, maneno haya ni mazito sana kama utayatafakari na nayatolea mfano kuonesha uzito wa maneno haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge hapa tukikosa maji kwa siku moja tu Bungeni humu hakutakuwa na mtu, tutashindwa sote kuja hapa ndani ya Bunge kuonesha kwamba maji ni muhimu hatuwezi tukakosa maji angalau kwa siku moja na viumbe vyote hai vinahitaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msisitizo huu lengo langu kubwa kusema kwamba tunaiomba Serikali iongeze bajeti ya maji, bajeti ya maji

haikidhi. Mwenyezi Mungu amejaalia Wizara hii kupata Waziri kaka yangu Mheshimiwa Aweso, anapiga kazi kubwa sana, anafanya kazi usiku na mchana, ameifanya Wizara hii iwe ni Wizara ambayo inasikilizwa na anasikilizwa kwa sababu wafanyakazi wote amewaweka pamoja, wapo tayari usiku na mchana kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nirejee msemo ambao yeye mwenyewe amesema siku ya semina ya Bunge zima kupitia Wizara ya Maji amesema hivi; "Bila nyenzo hutoki."

Mheshimiwa Spika, maneno haya aliyasema Mheshimiwa Waziri siku ile na mimi nikayaandika na nikataka niyarejee leo, lakini maneno haya sikurejeshei wewe, nairejeshea Serikali kuona kwamba bila ya kukupa nyenzo hata kama una nguvu kiasi gani huwezi kufika pale ambapo tunapakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kunipeleka kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira. Sisi wanakamati hatuna shaka na Mheshimiwa Waziri kabisa, wala watendaji wake lakini tuna shaka na bajeti hii ambayo amepewa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yam waka 2020/2025 imeelekeza kwamba kwa vijijini tufikie 85% ya maji, hivi sasa ipo asilimia 79 pointi kadhaa na mijini kufikia 95% na hivi sasa ipo 90%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina wasiwasi sana kwamba kiwango hiki hakitafika kwa bajeti hii tukiwa tumebakisha mwaka mmoja. Mwaka huu ni wa kupiga mbio na kumtuma Mheshimiwa Waziri afanye kazi kubwa ya kufanya miradi yote iliyokuwepo ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe ushauru wangu, lakini pia ni ushauri wa Kamati; kwanza Serikali ione inalipa madeni ya wakandarasi na hii itapendeza kama madeni haya yatalipwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024 ili kuipa nguvu Wizara hii ya kufanya kazi ile ambayo imebakia lakini pia kufanya kazi mpya ili

kuendana na ile dhima ambayo anadaiwa au inadaiwa Wizara hii ya kufikisha 85% kwa shamba, lakini 95% kwa mijini.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili na hili ni la kwako Mheshimiwa Waziri, iangalie namna nzuri ya kupunguza bei hasa katika maeneo ya vijijini ya wale ambayo wanapelekewa maji. Mara nyingi inatokea kwamba maji hayafiki ndani ya nyumba si kwa sababu wananchi hawayataki, ni kwa sababu ya uwezo wa kufikisha ndani ya majumba yao. Kwa hiyo ningeliomba ukatafute utaratibu maalum ambao utawawezesha walio wengi kupata maji ndani ya majumba yao ili kuonesha kwamba tunapata maji bila shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la tatu au mapendekezo ya tatu Wizara ione namna nzuri ya kuzuia upotevu wa maji. Hili jambo umelisisitiza hata wewe mwenyewe kwenye semina na ukasema kwamba jambo hili utalichukulia mkazo naomba ulichukulie mkazo zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Spika, Ester Amos Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherahani, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mwanangu nisikilize kwenye jambo linalohusu Bunda Mjini.

Mheshimiwa Spika, tuna miradi pale Bunda Mjini ambayo ikikamilika ule mradi mkubwa utakuwa na maana, tunaomba pesa mamlaka yetu bado changa, inajikongoja, ina mkurugenzi mwanamke anachapa kazi sana haya yote hatoyafanikisha msipompa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza, Mradi wa Kutibu Maji Taka wa Butakale ni wa shilingi bilioni 1.7 mmetoa shilingi milioni 400 tunahitaji pesa ili huu mradi ukamilike. Mradi mwingine ni mradi unahitaji shilingi bilioni 1.4 ni mradi wa bomba kubwa sijui tumeelewana mwanangu kutoka Migungani hadi Kaswaka kule kwenye tenki mlimani shilingi bilioni 1.4 na hapa ukitupa tutaondoa aibu ya Bunda kuwa wa tatu kwenye upotevu wa maji ambayo mradi tumetumia 45% tu hiyo 45% ndiyo inayochangia kwenye kupotea, karibu shilingi milioni 700 hasara kwenye upotevu wa maji tunaomba shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, naendelea, mradi mwingine wa shilingi milioni 600 huu ni kupeleka maji Chuo cha Kisangwa, kusambaza mabomba kilometa saba, tunahitaji shilingi milioni 600 ili huu mradi maji yapatikane. Mradi mwingine ni Balili - Kunzugu shilingi milioni 733 tunaomba hizo pesa, wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwenye kata zote 14 wapate maji safi na salama, umesikiliza mwanangu naendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea, tatizo la upotevu wa maji nchi hii limekuwa kubwa sana lazima mfanye utafiti wa kutosha lazima tujue kiini. Nilikuwa napitia ripoti ya CAG hapa kwenye mamlaka 12 upotevu wa maji shilingi bilioni 9.9 haiwezekani, kwenye mita za ujazo milioni 8.7 maji yanamwagika tu ambazo hizi hasara tungezishughulikia leo hii shilingi bilioni tisa tungesambaza miradi ya maji kwenye majimbo mangapi?

Mheshimiwa Spika, lazima tugundue tatizo la upotevu wa maji. Kama watu wanajiunganishia kiholela, kama uzembe, kama miundombinu imechakaa, lazima tuweke mikakati ya kuhakikisha tunakomboa hizi pesa mabazo zinapotea bila sababu. *EWURA* wametoa kiwango cha maji imezidi inaendelea kuzidi, hili lazima ulifanie utafiti wa kina ili tuache maji kupotea kabla hayamfikia mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, na nitoe mfano Mamlaka ya Rombo maji yaliyopotea hasara shilingi bilioni tano, Handeni shilingi bilioni 2.1, Mamlaka ya Mji wa Bunda shilingi milioni 788, Maswa shilingi milioni 666, Turiani shilingi milioni 648, hizi ni halmashauri chache tu

nimetolea mfano. Mambo kama haya hatuwezi kuyavumilia unapewa bajeti ndogo lakini lazima wataalamu wafanye kazi kuangalia kutatua chanzo cha upotevu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ni aibu kuzungumzia tunapunguza bajeti kwenye Wizara ya Maji kweli, kweli, zaidi ya shilingi bilioni 100 halafu tunataka tatizo la maji liishe sina shaka na uwezo wako wewe na watendaji wako, tunataka pesa itoke ili wananchi na akina mama wa nchi hii tuwatue ndoo maji kichwani. Hatuwezi kuwatua ndoo maji kichwani kwa kupunguza bajeti ya maji. Tunataka tuongeze bajeti ya maji ili wamama waondokane na usumufu wa kutembea umbali mrefu kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka jana nilizungumza hapa kuhusiana na taasisi za Serikali kutumia maji hawalipi, akasimama Mheshimiwa Waziri wa Fedha akasema ametoa maelekezo watalipa, leo taasisi za Serikali zinadaiwa shilingi bilioni 26, wananchi wa kawaida kule wakitumia maji wanakatiwa, kwa nini msiwakatie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge nisikilizeni, JWTZ wanadaiwa bilioni 12 yaani wanatumia weee mpaka shilingi bilioni 12 hawalipi, Magereza shilingi bilioni sita, Polisi shilingi bilioni 5.374, Serikali za Mitaa shilingi bilioni 1.5, hospitali za mikoa shilingi milioni 635, Ikulu Ndogo shilingi milioni 102, Mifugo shilingi milioni 44, kweli?

Mheshimiwa Spika, sasa hizi mamlaka zitaanzishaje miradi mingine? Ninyi mnatumia maji, hamlipi, mwaka jana mmeji-*commit* hapa. Juzi kule Mbweni kuna mtu tu alichimba mitaro mabomba yakakatika, *DAWASA* wakaja wakarekebisha ndiyo hizi hela mkiwalipa wanafanya hayo. Leo mamlaka zinashindwa kujiendesha, mmekalia shilingi bilioni 26 zao mnatumia maji ya kupika chai ofisini, watu huko wanaoga kweli, kweli hivi mnadhania ni raha hapa sisi tuseme vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinatumia maji hayalipi?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha yupo, Mawaziri wote mpo hapa halafu wananchi wanakatiwa maji kiholela huko

wakitumia maji na wepesi kwenda kudai bili halafu mnataka Mheshimiwa Aweso afanye nini, mna shilingi bilioni 26 zake, mnampunguzia Bajeti, halafu hiyo ndoto ya kumtua mama ndoo kichwani inatoka wapi? Lipeni madeni, yaani huku Wizara ya Maji mdaiwe, wafanyakazi walie kikokotoo, walimu wanalalamika, tutaendaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge wanaofuata wote watachangia kwa dakika tano kwa yale niliyokuwa nimeyasema kabla hatujaanza uchangiaji.

Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa sababu ya uchache wa muda kwanza kabisa binafsi nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini mimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, lakini nikushukuru sana ndugu yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa maono makubwa pamoja na timu yako ya Wizara mliyoyaleta kwa Mheshimiwa Rais ambapo sasa kazi kubwa kwa upande wa kumtua mwanamama ndoo kichwani inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, nimezunguka maeneo mengi sana kwenye Kamati, lakini tumefika maeneo mbali mbali changamoto kubwa ya wananchi wetu ni upanuzi wa miradi. Upanuzi wa miradi ndiyo kilio kikubwa kwa wananchi wetu, tumefika Songea, kijiji cha Marungu kuna mradi wa shilingi bilioni 1.2 wananchi wale wengi wanalalamika upanuzi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lalamiko lingine la wananchi miradi hii yote inayotekelezwa inazungukwa na wananchi wetu wafugaji na ndiyo walinzi wakubwa wa miradi hii. Sasa kilio chao wafugaji ni kuomba kwa sababu miradi ya maji inapopita hawakumbuki kutengenezewa eneo la kunyweshea mifugo yao, ni eneo ambalo wafugaji wengi wanalalamika, niendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri hili eneo likumbukeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanahangaika, wanazunguka, wanatembea mchana, wanazunguka maeneo mbalimbali, sasa mnapowatengenezea vimbauti katika maeneo yao wao wanasema hawana shida kulipia maji, hawana shida kabisa, lakini sasa kama hawajatengenezewa kale kaeneo nikuombe Mheshimiwa Waziri kwamba wafugaji wetu muwakumbuke.

Mheshimiwa Spika, mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa upande wa Ushetu. Wananchi wa Ushetu wamelalamika siku nyingi, wananchi wa Ushetu wamelia siku nyingi, walikuwa na changamoto kubwa sana ya maji hasa mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambayo ilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Ushetu na ndiyo lilikuwa ni jimbo pekee ambalo lilikuwa limesahaulika katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jumaa Aweso nikupongeze sana wewe binafsi na timu yako yote na ma-*engineer* wako wote, lakini pia nimpongeze sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kukubali kukuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huu, mradi ambao itakuwa ni suluhisho sana kwa wananchi wa Ushetu. Najua kuna maeneo ambayo pia yamepata maji, mafano mradi wa Igwamanoni ambao uligharimu zaidi ya shilingi milioni 400 unafaidisha wananchi wa Iramba na pale Igwamanoni peke yake.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia Kijiji cha Mwamanyili hakina maji, Kijiji cha Kipangu hakina maji, Kijiji cha Nyakashadala hakina maji, eneo hili linazungukwa na wananchi ambao ni wengi sana bado wanateseka maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unakuta sawa mradi wa maji upo na umekamilika lakini hebu kwa sababu ya makusanyo ya fedha yanayochangiwa kwenye

maeneo yale ambayo tunatoza hebu tuzielekeze kwenye maeneo husika kwenda kupanua mradi wa maji.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Sabasabini ambao umegharimu shilingi bilioni 1.2, nikushuruku sana Mheshimiwa Waziri umekamilika, lakini wananchi wanaozunguka vijiji vile wote bado hawajafaidika na maji. Tuna mradi ambao upo pale Nyamilangano na Mradi wa Busenda pale ambao ulikuja Mheshimiwa Aweso nikushukuru sana ambao ulikuwa ujengwe kwa shilingi milioni 500 lakini niwashukuru sana ma-*engineer* wa Mkoa wa Shinyanga *Regional Manager* wa *RUWASA,* watu hawa walitumia shilingi milioni 300 lakini mradi ulikuwa utumie shilingi milioni 500 na *point*.

Mheshimiwa Spika, tayari walitumia shilingi milioni 300 ina maana zilibaki zaidi ya shilingi milioni 100 na nashukuru Mheshimiwa Waziri ulihaidi kwamba Kitongoji cha Imambo A na Imambo B kihudumiwe kwa fedha hizi shilingi milioni 100 zilizobaki, kazi Mheshimiwa Waziri inaendelea wananchi wa Ushetu wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niendelee kuiomba Serikali iongezeeni fedha Wizara ya Maji kwa sababu maji ndiyo roho ya nchi yetu ya Tanzania, bila maji kama walivyosema Wabunge wenzangu hatuwezi kufanya kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa wanazozifanya na fedha ndogo wanazopewa, lakini bado wanazisimamia vizuri sana na timu yake. Sisi tumezunguka maeneo mengi, tumepitia miradi mingi sana, ma-*engineer* wako wote, ma-*RM* katika mikoa yote nchini wanafanya kazi ya kuisimamia fedha pamoja na kwamba ni kidogo lakini bado inasimamiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mimi niendelee kuiomba Wizara ya Fedha, wamwongezee fedha Mheshimiwa Jumaa Aweso, huyu kijana kwa kweli umri bado ni mdogo, lakini kulingana na kuuzima kichwa sana fedha apate wapi, anaonekana kama sasa anaenda kuzeeka, mwongezeeni fedha Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru sana kulingana na hali ya muda, lakini naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kutekeleza miradi ya maji kama ambavyo yeye ni mwanamke na anataka wanawake wa Tanzania wamalize tatizo la maji, lakini Mheshimiwa Rais alivyo mnyenyekevu ndivyo Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake na...

*(Hapa kuna Mbunge alipita kati ya Mzungumzaji na Spika)*

**SPIKA:** Mheshimiwa umemuona anayechangia yupo wapi? Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alivyo mnyenyekevu ndivyo Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake nao ni wanyenyekevu vilevile, kwa sababu tumeshuhudia kila ukienda kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Katibu Mkuu kwa Taasisi *RUWASA* uNasikilizwa vizuri na unashauriwa kwa hiyo nawapongeza sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ambayo imesimama ambayo hata mikataba yake imeisha, lakini ni wa sababu ya kukosa fedha na kuikamilisha hiyo miradi. Jimbo la Magu lina Mradi wa Nyang'anga Iseni ambao upo kwa 77%; Jimbo la Magu una Mradi wa Rugee Kigangama upo 44%; Jimbo la Magu lina Mradi wa Misungwi Rumegi 80% miradi hii inahitaji fedha ya kwenda kukamilisha. Hebu niombe mimi Wizara siwezi kuiomba sana, naiomba Wizara ya Fedha kwa sababu tunaamini Wizara ya Maji imekwisha kupeleka maombi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara ya Fedha iipe Wizara ya Maji fedha ili iweze kutekeleza hii miradi kwa sababu hata hivyo wakandarasi wameshindwa kuendelea wanaingia gharama

kubwa za *interest* kwa sababu ya kutolipwa kwa wakati. Kwa kweli kama Wizara ya Fedha haitapeleka fedha Wizara ya Maji bado miradi hii itakuwa imezama na hapo sasa sisi ambao tupo kwenye Kamati ya *PAC, value for money* hatuioni kwenye miradi hii. Hebu ziende fedha ili angalau miradi hii iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo mradi mkubwa wa Kisesa - Bujora ambao Waziri wewe uliagiza ukiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwamba anzeni kujenga tenki. Tenki linajengwa kubwa la shilingi milioni tano, tatizo kubwa ni ule mradi wa usambazaji mabomba, kwa kweli nikuombe tu umetuletea mama anaitwa Nelly yule Mkurugenzi wa *MWAUWASA* ni mzuri kuliko maelezo, anakwenda *site* na kusimamia, kwa kweli una watumishi wazuri wanaokuelewa. Niombe sasa kwa sababu *tender* imekwisha kutangazwa na ipo kwenye hatua za manunuzi, hebu usukume haraka ili mradi wananchi hawa wa Kisesa - Bujora waweze kuona mradi wao unakamilika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 nilikuwa na swali la msingi katika Mradi wa Langi – Lutale – Langi, Serikali iliji-*commit* hapa ikasema itatenga fedha za kutosha kugharamia kuanza kutekelezwa mradi ule kwa sababu usanifu tayari umeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, nashangaa na kusikitika kwamba shilingi milioni 294 ndizo zilizotengwa kati ya shilingi bilioni 30. Sasa Serikali huwa inatudanganya inapokuwepo hapa kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali hapa wananchi kule wanasikiliza.

Mheshimiwa Spika, sasa nikuombe tu Mheshimiwa Waziri kama hutatenga fedha hizi angalau hata shilingi bilioni tano za kuanza maana yake kule wananchi wa Jimbo la Magu wataona kwamba Mheshimiwa Waziri umeondoa fedha hizi, mradi ule usitekelezwe wakati wewe ni kijana ambaye tunaomba sana ikiwezekana Mheshimiwa Rais umalize naye mpaka mwaka 2030 ili miradi hii iweze kutekelezwa kikamilifu kwa sababu umenza kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka sasa hivi ni Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri sana Serikali, tunapojibiwa hapa maswali yaendane na kauli za Serikali ili kuwasidia wananchi mawazo yao, kwa kweli sisi tunasikitika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la madeni; kama Mfuko wa Maji ungekuwa unakwenda kila mwezi Wizarani na kila mwezi wanalipwa wakandarasi miradi hii ingekuwa imekamilika. Nikuombe sana kwa kweli wewe na wataalamu wako hata ukienda *RUWASA*, Mkurugenzi wa *RUWASA* amesimama na wasaidizi wake. Kwa kweli Wizara ya Maji imejipanga vizuri na wewe tunakuombea pamoja na Naibu wako na Katibu Mkuu ambaye kwa kweli ana muda mfupi na hii ni bajeti yake ya kwanza, na hili mimi nilikuwa nasema ili niunge mkono…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti kuu Wizara hii iongezwe pesa, tusikubali kupitisha bajeti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru wewe, kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumshukuru Waziri wa Maji, Naibu Waziri na watendaji wote wakuu wa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali naomba nifikishe shukurani kwa Mheshimiwa Rais. Wananchi wa Buhigwe, Kata ya Buhigwe, Kijiji cha Kavomo, Mlela na Bwega wanashukuru sana kwa mradi wa shilingi bilioni 1.6, mradi umekamilika, huduma zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Migongo, Kata ya Kilelema wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaishukuru Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Aweso kwa mradi wa maji wa shilingi bilioni moja umekamilika kwa 100% na huduma zinaendelea. Aidha, wanakijiji wa Kijiji cha Kilelema, Kata ya Kilelema walipata ufadhili wa *World Division* mradi wa shilingi milioni 353 nao umekamilika, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kushukuru ni kuomba, ninaomba pamoja na kwamba tayari bajeti imekwisha taja miradi minne hapa, ninaomba ujenzi wa Mradi wa Maji wa Rusaba wa shilingi bilioni moja, ujenzi wa Mradi wa Kijiji cha Nyaruboza shilingi bilioni moja, Mradi wa Maji wa Mnanira, Nyakimwe, Mkatanga, Msagala, Kitambuka, Kibande na Bweraka wenye thamani ya shilingi bilioni 8.2 ambao umepangiwa shilingi bilioni moja. Hii fedha ni ndogo naomba iongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile upanuzi wa Mradi wa Maji wa Migongo kwenda Kilelema ambao kwenye bajeti tumepewa shilingi milioni 141, mradi huu jumla shilingi 3,390,000,000 fedha hizi zilizotengwa ziweze kutekeleza miradi hii zipatikane kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia miradi ya jimbo langu naomba nitoe ushauri kwa Wizara ya Maji; kwanza niwapongeze kwa mchakato ambao umefikiwa sasa wa kumpata mshauri mwelekezi kwa ajili ya mradi mkubwa ambao unaenda kutatua tatizo na changamoto ya maji katika Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma ambao tayari wamekwishafikia hatua ya kumpata mshauri mwelekezi ambapo maji yatachukuliwa katika Ziwa Tanganyika kuja kwenye mikoa hiyo na hatimaye kuja Mkoa wa Tabora na kuja kwenye mikoa ya kati kwa ajili ya kutengeneza Mradi wa Gridi ya Maji ya Taifa, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashauri Wizara ya Maji itafute vyanzo ambavyo vitakuwa ni imara kwa ajili ya kuweza kukamilisha hii miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja; ninaungana kabisa na ushauri na maoni ya kamati na pia ningependekeza kwenye Mradi wa *SGR* kuna shilingi 100 inayokatwa pale ingepunguzwa shilingi 50 ije kwenye miradi ya maji ili iongeze pato tuweze kutekeleza miradi hii ya maji. Maji ni uhai, maji ni maendeleo, maji ni kilimo, maji ni viwanda, bila maji ya uhakika hatuwezi kuwa na nishati, maji ni usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba na ninapendekeza hiyo fedha iliyopungua shilingi bilioni 137.6 ya bajeti, tunaomba irudishwe pale. Ni vema tuendelee na bajeti ile iliyopita kuliko kupunguzwa kwa sababu kuna madeni mengi ya nyuma na bado kuna miradi mingine mipya ambayo bado haijatekelezwa na bado ninashauri tena Wizara ijipange kukamilisha mradi wa kutengeneza Gridi ya Taifa na kuhakikisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa, Kidunda na kuhakikisha mito na vyanzo vingine vyenye uhakika wa maji kutengeneza maji yatakayotengeneza Gridi ya Taifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai lakini pia na afya njema niliyonayo, lakini niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na nia yake ya dhati ya kuwatua wakina mama ndoo kichwani, kwani miradi mingi anaendelea kutekeleza ili kuhakikisha maji yanapatikana kwa urahisi na kwa umbali ulio karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru mdogo wangu Mheshimiwa Jumaa Aweso, kaka yangu Mheshimiwa Kundo, lakini pia na Mheshimiwa MaryPrisca Mahundi, kiukweli wamefanya kazi nzuri sana kwenye hii Wizara, lakini yote kwa yote niendelea

kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuchagulia mwanamama makini sana mdogo wangu Mwajuma Waziri kama Katibu Mkuu Wizara ya Maji. *Engineer* Mwajuma mimi ni *schoolmate,* lakini ni wa *kulugo* kabisa na wanasema, siku zote mzigo mzito mpe Mnyamwezi na huyu Mnyamwezi amepewa mzigo mzito na naamini kabisa atautendea kazi na mimi leo kwa hii heshima aliyotupa Mheshimiwa Rais watu wa Tabora sitashika shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nianze kuongea suala la maji hususan kwa Jimbo langu la Ulyankulu. Jimbo langu la Ulyankulu kijiografia ni jimbo ambalo maji kutoka chini ya ardhi ni tabu sana kupatikana, lakini mwarobaini wa maji kwenye Jimbo la Ulyankulu ni maji kutoka kwenye mabwawa.

Mheshimiwa Spika, kuna Bwawa langu la Ichemba, bwawa hili likijengwa na likakamilika litakwenda kuhudumia wananchi takribani kata tisa na vijiji 28, lakini kwa masikitiko makubwa bwawa hili liko kwenye Ilani ya Uchaguzi yam waka 2015/2020 ikapita *dash,* mwaka 2020/2025 na lenyewe hili bwawa limo, lakini umebakia mwaka mmoja tufike mwaka 2025 hakuna dalili ya hili bwawa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana mpaka inafikia mahali nataka nijihisi kana kwamba sisi wananchi wa Jimbo la Ulyankulu kwa sababu kulikuwa na wakimbizi labda ukimbizi wetu kwa kipindi hicho tunaendelea kutengwa, lakini sitaki kuamini hilo. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana bwawa hili litengewe fedha, fedha ilitengwa, lakini mpaka dakika hii halijahudumiwa chochote. Mkandarasi amesaini mkataba na ameomba takribani shilingi milioni 571 tu, lakini mpaka dakika hii hazijakwenda.

Mheshimiwa Spika, sijapanga kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, lakini kama hutoniambia hizi fedha zinatoka lini ili wananchi wangu wamwone mkandarasi yuko *site* na maji yatoke na sisi tutumie maji kama *RUWASA* wanavyosema maji bombani, tuyapate maji bombani. Sasa hivi wananchi wangu wanatembea umbali mrefu sana kufuata maji. Mheshimiwa Waziri nikuombe tutengee fedha ili hili bwawa lianze utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipende kushukuru hivi visima vitano vya kila jimbo, kuna kisima ambacho tunataka kujenga Kaswa, Kijiji cha Taba, Kijiji cha Mwendakulima, Ulanga na Mgelela, nikuombe visiwe kama vile visima vya kwanza, vimechimbwa visima vizuri na ile mitambo ambayo ametuletea Mama Samia, lakini vile visima havitoi maji. Kwa hiyo, tusiwe tunawadanganya wananchi kwamba waone magari tu yanarandaranda kule vijijini, yanatuchimbia maji, lakini maji hayatoki. Tuombe sasa, kwa sababu mmesema hivi ni *fast track* na kweli viwe ni *fast track,* vichimbwe kwa muda mfupi na vianze kutoa maji wayaone na isiishie tu kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa Waziri Aweso wewe ni kijana shababi kabisa na unasema anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo yake. Mimi najua mihemo ya watu wa Ulyankulu, Ulyankulu tunataabika sana, watu wanataka waboreshe hata ndoa zao. Sasa hivi ndoa zina migogoro mikubwa sababu ya maji. Watu wanaamka asubuhi kwenda kufuata maji, hawapati hata haki yao ya ndoa ya asubuhi. Mheshimiwa Waziri nikuombe tupelekee maji watu tunataka tuwakumbatie wanaume wetu asubuhi. Nikuombe hizi blaablaa za kuwa kila siku unasema sijui nini nini, hatutaki tunataka fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niombe kwenye jimbo langu tulikuwa tumetengewa shilingi bilioni tano, lakini fedha zilizopelekwa kutoka kwenye Mfuko wa Maji ni shilingi bilioni 2.3 lakini bajeti inayoombwa mwaka huu ni shilingi bilioni 2.63, tunaona namna gani bajeti yetu inavyozidi kupungua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, Mheshimiwa.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, tuangalie sisi watu wa Ulyankulu siyo wakimbizi tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema, kengelea ya pili imeshagonga.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitangulie tu kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikitusaidia kufuatia janga la mafuriko katika Wilaya yetu ya Kilwa, janga ambalo limepelekea watu wetu nane kupoteza maisha katika vijiji vya Chumo, Nandete, Mitole, Miguruwe, Njinjo, Nahama na Njia Nne na katika misaada ambayo inakuja ningeomba Serikali isisahau kutuletea mbegu za mazao ambayo yanaweza kukua kwa muda mfupi ili tuweze kukabiliana na changamoto ya baa la njaa.

Mheshimiwa Spika, nitangulie kukupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri inayofanyika katika Wizara yako ya Maji na inaonekana kwa vitendo, lakini niseme tu kwamba tunashukuru sisi Wana-Kilwa Kaskazini kwa sababu kuna miradi kadhaa imetekelezwa katika Vijiji vya Kipindimbi, Somanga, Mingumbi, Chumo, Chapita na Marendego. Pia naomba nikukumbushe Mradi wa Kinjumbi unaotekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Maji umekwama kwa miaka mitatu sasa, ninaomba katika kipindi cha mwaka huu wa fedha unaokuja kabla ya mwaka 2025 mradi huu uweze kutekelezwa na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri tarehe 6 Oktoba, 2021 yapata miaka miwili na nusu sasa alishuhudia Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini alifika sehemu inaitwa Nasaya, alifika sehemu inaitwa Masaninga na kule alikuta umati wa wananchi ukiwa umebeba ndoo za maji wakiashiria uwepo wa uhaba wa maji na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba huduma ya maji itapelekwa kule haraka sana, lakini katika hali ya kusikitisha hadi sasa maji hayajapatikana. Mheshimiwa Waziri hili jambo ni *sensitive* sana nanimekupigia mara kadhaa, naomba huu mradi utekelezwe na visima vichimbwe na mtandao wa maji uwekwe Nasaya na

Masaninga, na nitaomba maelezo namna gani mnakwenda kutekeleza huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna mradi wa vijiji vitano, tunashukuru Serikali imepanga kutekeleza mradi huu katika Vijiji vya Nandete, Pungutini, Kibata, Mwengei pamoja na Kitongoji cha Nambunju katika Kijiji cha Zinga Kibaoni, lakini rai yangu niombe kama alivyotangulia kuzungumza mzungumzaji aliyepita kwamba utekelezaji ukafanyike kweli kweli na ndani ya wakati ili tunapofika mwezi Disemba mambo yawe yamekaa sawasawa na twende kifua mbele kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na ule uchaguzi mkuu ujao mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kutoa pendekezo katika eneo hili kwa kuwa kwenye miji mikubwa kama Arusha, Mwanza, Tanga na Dar es Salaam ipo miradi mikubwa ya mabilioni ambayo inazalisha maji na *excess* nilifikiri kule msipeleke hivi visima vitano, hivi tuongezeeni sisi wenye vijiji vingi badala yake kule tawanyeni mtandao wa maji kwa sababu katika maeneo mengi hii miradi inazalisha maji ya kutosha, kama kule Arusha wanazalisha lita milioni 200 kwa siku wanatumia lita milioni 120 tu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** ...wana *excess* ya zaidi ya lita milioni 80.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema nashukuru, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza, binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa na uwekezaji mkubwa kwenye Wizara hii ya Maji. Tumeona tumeshuhudia maeneo mbalimbali ile miradi ambayo ilikuwa imsimama kwa muda mrefu imeanza kutoa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na timu yako nzima, mmekuwa mnafanya kazi nzuri, mmetembea nchi hii nzima katika utatuzi wa miradi ya maji katika maeneo yetu, nakupongeza sana. Pia nawapongeza watumishi wako walioko ndani ya Mkoa wa Tabora, lakini pia ndani ya Wilaya yetu ya Igunga Meneja wetu Ndugu Muraza pamoja na Meneja wa Mkoa, Ndugu Kapufi kwa kuendelea kufanya kazi nzuri, hongereni sana watumishi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu na pongezi nimewasikiliza Wabunge wengi, sina mapya ambayo ninaweza nikayachangia, lakini ninachoweza kusema haya mengine yako ndani ya uwezo wako.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumeona bajeti ya Wizara ya Maji mwaka jana ilikuwa zaidi ya shilingi bilioni 756, mwaka huu imeshuka na kurudi shilingi bilioni 627, kwa hiyo, kuna upungufu wa bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi kule unakoenda huwa unashuhudia akina mama wanavyoshangalia wanapoona maji yamepatikana katika maeneo yao, wanabeba miti, wanagalagala chini, hiyo ni hali ya kuonesha wanafuraha maji wameyaona. Hebu fikiria wale ambao hawajapata maji wanahali gani na wahanga wakubwa wa maji ni akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wewe hapo ni mwana mama umekaa kwenye kiti chako, hebu nikuombe ufanye jambo hii bajeti badala ya kupungua kushuka kwenye bilioni nikuombe utengeneze mazingira hii bajeti iweze kurudi angalau ifanane na ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaporudisha hii fedha itaweza kwenda kusaidia kulipa madeni kwa wakandarasi wanaodai, lakini pia itaenda kuongeza mtandao wa maji katika maeneo yetu na hili nikwambie ndani ya Wilaya yetu ya Igunga, Jimbo letu la Manonga kule kwenye Kata ya Igweka kuna watu zaidi ya 22,000 hawana maji, hawana maji vijiji vitano, Kata ya Igoweko hawajawahi kuona maji, Kata ya Yuswaya hawana maji, Kata ya Tambarare hawana maji na Kata ya Sungizwi hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuja Mheshimiwa Rais pale na nikamwambia Mheshimiwa Aweso hizi kata zipate maji, lakini katika ile Kata ya Ntobo kwenye Kijiji cha Ntobo pamoja na Mwamloli hawana maji. Tunaomba hii bajeti iongezwe ili haya maeneo mengine yaweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, pia tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa vijiji 900 sasa karibu maeneo nchi nzima tutapata visima 900 na sisi kwenye Wilaya yetu tutapata kwenye kijiji kimoja cha Igoweko, Kijiji cha Uswaya, Kijiji cha Tambarare, Kijiji cha Igondela, Kijiji cha Igumo pamoja na Mpogolo. Nashukuru sana kwa visima hivi vitano, lakini pia nimwombe Mheshimiwa Waziri, Mkoa wetu wa Tabora ni mkubwa sana, ni mkubwa una *square meter* 76,000 ukilinganisha na Mkoa wa Geita wenye *square meter* 14,000 kilometa za mraba zile, unaingia mara tano. Hebu mnapotupa gari moja, Mkoa wa Geita gari moja, Tabora gari moja, ukubwa wa eneo hamzingatii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyokwambia leo toka mmetupatia lile gari Wilaya ya Igunga halijawahi kukanyaga. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri ongeza magari, tupe magari mawili au matatu lingine likae Igunga, lingine likae Tabora na lingine likae huko hata Uyui. Nakuomba sana uongeze gari ili visima viweze kuchimbwa kwa kasi, vinginevyo hili gari litafika Igunga mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa itakuwa haina maana, nakuomba hili gari lifike mapema ili wananchi waweze kuona matunda ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwainua

wananchi katika kuhakikisha kwamba wanapata, lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri tumepata mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Ziba kwenda Nsimbo wa zaidi ya shilingi bilioni 500. Mwaka jana hukukamilika, mmehamishia mwaka unaofuata changamoto ni nini? Changamoto mmetuambia mliwachukua wataalam mkawapeleka kwenye mafunzo hali iliyopelekea mradi kutokuanza kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, mnawachukua wataalamu mnawapeleka kwenye mafunzo, watu wanakosa maji. Hili jambo lisijirudie wakati mwingine, tunaomba wananchi wapate maji kwa wakati. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa George Natany Malima ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Nami nimpongeze Waziri na timu yako yote kwa kazi nzuri mnayoifanya, wakiwepo wale makamanda wako kule Kilimanjaro, *Engineer* Kija Limbe, Munishi na Msangi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Rais wetu kwa kutupatia shilingi milioni 500 ambazo zilikwenda kutekeleza mradi katika Kata ya Kimochi, tunashukuru sana. Katika hii kata kuna matenki mawili ambayo yamejengwa kwenye Kijiji cha Lyakombila, tunashukuru. Hata hivyo, pale kwenye *intake* kuna bomba za inchi tatu, kwa hiyo, maji hayatoshi. Vijiji vya Mdawi, Shia na Sango karibu watu 14,000 hawajapata maji. Kwa hiyo, kusema ukweli tunaomba

msaada kwa sababu kata hii ni kubwa na ina watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa zawadi ya Rais ya vile visima vitano na hivi tumeshaongea na ma-*engineer* wako tunajua tunavyokwenda kuyaweka.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa na muhimu utahusu Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji *(National Water Grid)*. Hili ni jambo muhimu sana kwenye Taifa letu na katika hotuba ya Waziri ameonesha kwamba miaka kumi ijayo au 11 kutakuwa na upungufu wa maji kutokana na mabadilikoa ya tabia nchi na matumizi mabaya ya vyanzo vya maji, lakini pia ametupa takwimu ambazo wametoa wataalamu kwamba tutakuwa tunatumia mita za ujazo 883 badala ya 2,105 ambazo ziko sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa kuna tatizo, inaonesha kwamba miaka kumi ijayo kutakuwa na shida kubwa ya maji na hii imeshaanza kujionesha kwa sababu kwenye maeneo mengi hapa nchini sasa hivi Waziri amejitahidi amejenga miundombinu ya maji, lakini kuna maeneo tunapata maji kwa mgao, maeneo mengine maji hakuna. Kwa hiyo, naomba kifanyike kitu ambacho kitasaidia kutatua hili tatizo kwa sababu tusipofanya hivyo tutakuwa hatujalitendea haki Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, mimi ninaishauri Serikali ije na mpango kabambe wa dharura wa kutengeneza *National Water Masterplan,* badala ya ile mikoa mitatu ambayo mmeitaja kwenye ripoti yako Mheshimiwa Waziri kwamba ni Dodoma, Njombe na Rukwa, hapana, kwa sababu ni tatizo la kitaifa, twende kwenye mikoa yote, tushirikishe mikoa yote, tujue vyanzo vya maji viko wapi kwa kutumia teknolojia nzuri kabisa, tujue maji yatapatikana wapi, ubora wake, kama yatapatikana, tujue mahitaji halisi ya maji, tujue makisio ya siku zijazo na tuje na mkakati wa kutunza vyanzo vya maji ili hii shida inayokuja miaka kumi ijayo tuanze kuishughulikia sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili kwa Serikali ni kwamba iishirikishe jamii kwenye kutengeneza hii *National Water Masterplan* ili jamii iwe sehemu ya hii ya hiyo na wasiwe wakatuletea fujo za kusema kwamba hiki ni chanzo changu, hapa Serikali msiguse. Hata hivyo, tukiwashirikisha kwanzia mwanzoni itakuwa ni jambo la kheri na tutafanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa tatu, naomba Serikali ije na maoteo ya fedha, yaani miaka kumi ijayo tumeshajua kuna shida ya maji. Sasa huku mnapunguza bajeti ya Wizara ya Maji, naona kuna kitu hakipo vizuri. Tuje na maoteo ya fedha zitakazokidhi matakwa na ushauri utakaotokana na hii *National Water Masterplan.* Piga, ua, bila maji hakuna maisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naunga mkono hii hoja, nilikuwa na mambo mengi sana ya kusema, lakini kwa sababu ya muda naunga mkono hoja. Naomba utakapokuja kuhitimisha hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, asiponiridhisha kuhusu hii *issue* ya *National Water Masterplan,* Mheshimiwa Aweso tutazinguana. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niweze kuchangia kwenye hii Wizara muhimu sana katika nchi yetu na nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa niseme kwa uwazi kabisa kwamba katika jambo ambalo sitaliunga mkono na siliungi mkono kabisa ni suala la Wizara hii kupunguziwa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna vijiji 40 havina maji mpaka leo. Tumekubalina hapa na tume-*set* kwamba kufikia mwakani angalau vijiji vifikie 85%, lakini kwa mwendo huu ninahofu kwamba jimbo hili halitafikia hizi 85%. Kwa hiyo, nikuombe na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wakati wa Bajeti Kuu tusikubali kuipitisha ikiwa Wizara hii ya Maji haitaongezewa fedha. Niombe sana Wizara hii iongezewe fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, niipongeze Serikali sasa hivi katika Wilaya yangu, katika Jimbo langu tuna miradi tisa yenye thamani ya shilingi bilioni 1.1 inaendelea kutekelezwa na hii ikikamilika maana yake angalau sasa asilimia kadhaa zitaongezeka katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi iko ya muda mrefu haijakamilika, Mheshimiwa Aweso unakumbuka Mradi wa Maji Ruagala, ukiwa Naibu Waziri ulifika pale wananchi waliziba barabara, wakalala kukulilia upeleke maji, mpaka leo miradi ile uko Waziri haijakamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, upo mradi mmoja unatoa maji na ule wa Mabuni unatoa maji, lakini ile mingine haitoi maji vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe tuhakikishe hii miradi itoe maji katika kipindi hiki kwa sababu unakumbuka toka ukiwa Naibu Waziri miradi hii ilikuwa haitoi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna madeni yanadaiwa katika miradi hii. Sasa huku tunapunguza bajeti, huku madeni yanadaiwa, Hapana na haikubaliki, tuombe sana bajeti ya Wizara hii ibaki angalau kama ile ya mwaka jana ili madeni yazidi kulipwa, lakini na miradi mipya itekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa miradi ile ya vijiji vitano na mimi nashukuru katika jimbo langu tunaenda kujenga mradi Kiwombi, Litorongi, Kihangi Mahuka, Kindimba Chini na Manzega, maeneo haya yalikuwa na mahitaji makubwa ya maji. Sehemu nyingine tuna vituo vya afya, sehemu nyingine kuna mahitaji, kuna zahanati, lakini mpaka leo maji wanayachukua

kwa kuchota kwenye visima, lakini kupitia hii miradi ya vijiji vitano najua wanaenda kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kama walivyosema wenzangu basi mradi huu uharakishwe ili watu hawa waanze kupata maji, majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa na mengi siwezi kujenga hoja mpya hapa, muda wenyewe hautoshi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi nzuri ambayo anaifanya pamoja na bajeti yake kuwa ndogo.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja yangu kwamba katika Wilaya yangu ya Mpwapwa, Jimbo la Mpwapwa tuna miradi mingi kama mitano; Mradi wa Kisokwe, Idola-Mazae, Mradi wa Kata ya Lupeta - Makutupa, Nzomvu/Inzomvu, Mpwapwa Mjini – Ving'hawe – Mang'hangu, kuna mradi wa maji katika Kijiji cha Igujuani na kuna mradi wa maji katika Shule ya Sekondari ya Berege, yote hii haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba sana kwa bajeti hii inayokuja kamilisha kwanza miradi yote ambayo haijakamilika kabla ya kuanza miradi mipya, kwa sababu miradi mipya itakapokuja maana yake hii ya nyuma au ya zamani haitakamilika. Kule wananchi wanaona miradi imeanzishwa

halafu wakandarasi wameondoka, hakuna kitu kinaendelea, lakini ni kwa sababu wakandarasi halipwi fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru kwamba Mheshimiwa Rais kwa wazo alikuja nalo la kutoa vijiji vitano kila jimbo na sisi kule Mpwapwa kuna Vijiji vya Namba Thelathini, kuna Ngaramilo, kuna Ising'u, kuna Mlimani na Kijiji cha Mgoma, tunaomba sana vijiji hivi vipatiwe maji haraka kwa maana tulishatangaza sana halafu baadaye itafika mahali matokeo hayataonekana na utekelezaji utachukua muda mrefu. Mheshimiwa Waziri, naomba sana uchimbaji wa vijiji hivi vitano au visima hivi vitano basi ufanyike mapema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kusema ni kwamba niiombe Serikali bajeti ya maji ni muhimu sana, maji ni kila kitu. Bajeti iongezwe hii ya shilingi bilioni 627 ni ndogo, kama ile ya mwaka jana iliyokuwa kubwa kuliko hii imeleta shida kubwa mpaka sasa hivi miradi yote haijatekelezeka, halafu sasa imepungua, hii itakuwa ni tatizo kubwa sana. Naiomba Serikali iongeze bajeti, izidi hata ile ya mwaka jana ili miradi hii ambayo imetapakaa nchi nzima iweze kukamilika, wananchi wetu wanapata shida sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii ipo kwenye maeneo yao, lakini haitekelezeki na unapouliza unaambiwa mkandarasi hajalipwa fedha. Sasa kama wapo wengi hawajalipwa fedha halafu bajeti imepungua, tunategemea hii miradi itakamilika kwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana Serikali imsaidie Mheshimiwa Waziri, bajeti iongezeke, alipe wakandarsi wakamilishe miradi yote ambayo haijakamilika na usianze miradi mipya kama hii ya zamani haijakamilika, ikamilike kwanza halafu ndiyo tuendelee mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Mama wa Taifa amethibitisha kwa vitendo kauli ya kazi iendelee. Ukienda katika Bwawa la Mwalimu Nyerere utamkuta, Kigongo – Busisi utamkuta, *SGR* pale utamkuta, lakini amefunga kazi ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kuendeleza katika maeneo mbalimbali. Mama hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Tarime Vijijini nimeingia madarakai nikakuta 35.5% ya maji na hivi sasa ninavyozungumza ni 73.3% na miradi ambayo imepangwa kwenye bajeti ya mwaka huu ikikamilika tutakuwa na 82.6%. Mama Samia 2025 kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile visima vitano ambavyo vitaena Kata ya Mbogi, Getenga, Pemba kule Nyabisaga, Bumela, Kitenga, Ganyange, Nyakalema pia Mama Samia ataonekana katika maeneo hayo na 2025 Mama Samia aendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mama Samia ametusaidia sana katika Wilaya za Rorya na Tarime kwa kupeleka Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Kulikuwa na maneno mengi kwamba, maji yako pale Ziwa Victoria karibu na kwetu, lakini maji yamekwenda mpaka Tabora. Leo hii napozungumza maji yatanyweka Rorya, Tarime Mjini yatakwenda mpaka Sirari, Mbogi - Nyasincha, yatakuja mpaka Komaswa – Nyamongo, Mogabiri – Nyamwaga, Muriba, Susuni – Bumela na kule Mwema. Mama Samia 2025 kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo maombi muhimu sana katika eneo hili, tunavyo vijiji 88, vijiji 62 vina miradi ya maji, vijiji 26 havina miradi ya maji kabisa na vitongoji zaidi ya 300 havina maji katika Jimbo la Tarime Vijijini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri

aangalie katika maeneo haya angalau wapate maji ya kutosha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia nilileta ombi hapa kwamba Mradi wa Maji kule Magoto, Kata ya Nyakonga, Mradi wa Maji kule Itiro Kata ya Itiro, yale maji ni maji mserereko, ni maji machafu wakati wa mvua. Tunaomba tuwekewe chujio ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Mkoa wa Mara tumefikia 72% ya maji. Naomba niseme yafuatayo, Mheshimiwa Aweso amekuwa akipokea simu za Wabunge na kujibu kwa wakati; Mheshimiwa Aweso amefanya ziara kule Sirari akiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na maagizo waliyotoa kwenda Mbogi na Pemba, Mheshimiwa Waziri watu wako wamefika na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso amekuwa akijibu majibu sahihi na wabunge wote wamesema hapa kwamba kila akitamka anatenda. Mheshimiwa Aweso, Mheshimiwa Rais amekupa nafasi kubwa na umeitendea kazi, walisema Maprofesa kutoka Mlimani, naomba niwambie pia kuwa na wewe ni kijana wa *UDSM*, kijana wa *chemistry* umefanya kazi nzuri ni balozi mwema kwa wale ambao siyo wasomi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza kwa watu wa Pangani, wewe kwenye jimbo lako usisumbuliwe ili ulete maji kwenye nchi ya Tanzania na upite bila kupingwa. Mheshimiwa Rais, kijana kama huyu akifanya kazi nzuri itatugharimu nini kumpa pongezi kwa Azimio la Bunge kwamba Aweso ameafanya kazi nzuri sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mimi ninapendekeza, Wabunge wote wamesimama wamesema kila mahali kuna jambo linafanyika ila kuna upungufu wa fedha. Ninapendekeza kwako tuwe na Azimio la Bunge, Bajeti Kuu ikija hapa Mheshimiwa Aweso aongezewe fedha za maji ili miradi viporo ikamilike. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka niwambie kwamba hatuwezi kuchangia kuwa fedha ni ndogo halafu tukakaa kimya. Tuweke azimio kwamba fedha ya bajeti ya Wizara ya Maji isipunguzwe, wapunguze kwingine lakini kwenye maji waongeze fedha ili miradi ya maji iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, maji ni afya na maji ni usalama. Kila mtu anataka maji kwenye maeneo yake. Waheshimiwa Wabunge, tuongeze fedha na tuazimie kuongeza fedha ya bajeti ya ile. Waziri wa Fedha humu simuoni, ajipange huko aliko ajipange, fedha iongezeke, Mheshimiwa Aweso achape kazi, Wizara ichape kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, kule Tarime Vijijini Meneja wangu wa Maji wa Wilaya na Mkoa usiwaguse.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa sharti la kuazimia bajeti ya fedha iongezeke. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii uliyonipa.

Mheshimiwa Spika, sikutaka kupongeza, lakini kwa mipango mizuri ya uanzishaji wa Gridi ya Taifa ya Maji, kwa uboreshaji na ufanisi ulioletwa wa *CBWSOs*, kwa utekelezaji wa miradi ya *P4R* na ubunifu wa hati fungani, nataka nichukue nafasi hii ya mimi kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso, pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri sana wanayoendelea kuifanya kwenye hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hizi pongezi na shukrani kwa kipekee zimuendee Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia vizuri sana agenda ya maji hapa nchini na pia kwa namna ambavyo anahakikisha kuwa maendeleo yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa changamoto hii ya muda naomba niseme machache kati ya 14 na bahati nzuri nimekwishamwandikia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, moja ni Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Simiyu; tunashukuru sana mradi huu mwisho leo, mradi huu wa shilingi bilioni 444 umeanza, wananchi wa Mkoa wa Simiyu ambao utajengwa kwa Wilaya zote tano ikiwemo Meatu na Jimbo Kisesa, tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nikiri kabisa nikiwa Naibu Waziri, Ofisi yake mradi huu ndiyo ulianza na maandiko yalianzia pale. kwa hiyo, aliusimamia mradi huu kutoka pale akiwa Makamu wa Rais wakati na mpaka leo hii amekwenda kuutekeleza na sisi wasaidizi wake enzi hizo tulihakikisha kuwa mradi huu unakamilika.

Mheshimiwa Spika, hapa tu nataka niseme kidogo, kwa wale Mawaziri ambao baadaye wakiona wameshindwa kujibu maswali yetu wanasema ooh unajua ana jambo lake, nataka tuwaambie tu kwamba, hatuna jambo lolote tuna jambo moja tu la Watanzania kupata maendeleo na hakuna hiyama yoyote. Vilevile, huko wanakopeleka majungu wajue kwamba wengine ndiko tumekulia kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa Makamu wa Rais na leo ndiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi nimekaa pale kwa miaka mitatu na nilitoka pale kwa kuvikwa nishani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakosa hata nianzie wapi, niseme suala la fedha. Tumesema hapa fedha za maendeleo zimepunguzwa

kwa 18%, fedha hizo zisipunguzwe badala yake fedha za maji ziongezwe mpaka shilingi trilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili hatuna mzaha nalo, hauwezi ukapunguza fedha za maji wakati mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umekwishakamilika, huwezi ukapunguza fedha za maji wakati hata kwenye *TRAB* na *TRAT* tuna shilingi trilioni 10.5 mpaka sasa hivi zile kodi zipo. Hata tungekusanya asilimia 57 tu tungekuwa na shilingi trilioni 5.7, huwezi ukapunguza fedha za maji, ukapeleka fedha kwenye ruzuku ya mbolea ambayo wananchi wanapata asilimia 25 tu, huwezi ukapunguza fedha za maji wakati wananchi asilimia 57 tunaruhusu maji machafu kwenda kwenye mazingira, huwezi ukaruhusu kupunguza fedha za maji wakati sasa hivi wakandarasi wetu wanatudai zaidi ya shilingi bilioni 400, halafu unaipunguza bajeti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi ukapunguza bajeti ya maji katika changamoto nyingi kiasi hicho ikiwemo hata upotevu wa maji, kwa mfano pale Kigoma, Mamlaka ya Kigoma inapoteza maji asilimia 65. Tunachofanya pale tunatengeneza upotevu wa maji na wala hatutengenezi mahitaji ya maji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa unaweza ukapunguza bajeti hiyo ukiwa una mgogoro mkubwa hivyo wa maji hapa nchini? Unaweza ukapunguza bajeti hiyo ikiwa Rais wako tena mwanamke akiwa amewaahidi akina mama wote kuwafikishia maji, halafu wewe unakwenda kupunguza maji?

Mheshimiwa Spika, mambo haya sikutegemea kwamba tuna Tume ya Mipango halafu inakwenda kutuletea mipango ya hovyo ya namna hii? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, unapunguza fedha za maji unazipeleka wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imekwishagonga, ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, tunaomba shilingi trilioni 1.5 kwa ajili ya maji na siyo kuzipunguza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa upendeleo mkubwa ambao ametupatia wananchi wa Jimbo la Bukene kwa kutupatia mradi wa kielelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza Jimbo la Bukene tunapata mradi mkubwa wa kuyapeleka maji ya Ziwa Victoria Bukene kutoka Nzega ambao ni mradi wa shilingi bilioni 29. Huu ni mradi mkubwa sana kwa sababu ni mradi mmoja tu wa sekta moja ya maji, kwa hiyo, shilingi bilioni 29 ni fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mradi ndio unakwenda kuwa suluhisho la matatizo ya maji katika Jimbo la Bukene. Tumekuwa na matatizo sana ya kupata maji chini ya ardhi, tukichimba visima, visima vingi kwanza havina maji na ambavyo vina maji wakati wa kiangazi vyote huwa vinakauka. Sasa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria unakwenda kuwa suluhisho kwa sababu sasa tunatakuwa na uhakika wa kupata maji muda wote, iwe masika au iwe kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mradi huu unakwenda kutupatia maji kwenye vijiji 20 na vitongoji zaidi ya 100. Kwa hiyo, inakwenda kuwa suluhisho na hii awamu ya kwanza mradi huu utakapopita kwenye Kata za Shigamba, Itobo, Uduka, Mwamala, Kasela na Bukene na baada ya hapo sasa awamu ya pili utakuwa ni kuyatoa haya maji hapo yalipofika na kuyapeleka

sasa kwenye kata zilizobaki za Mogwa, Mbutu, Mbambari, Semembela, Kamahalanga na Isagenhe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao haturidhishwi na bajeti ya maji kupungua. Kwa kweli umuhimu wa maji sina haja ya kuueleza kwa sababu watu wote wameshaueleza, lakini kuna tatizo lingine pia pamoja na bajeti ya maji kupungua, lakini hata hiyo bajeti iliyopangwa maeneo mengi haiendi kikamilifu kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nzega huu mwaka ambao unaisha mwezi ujao tulitarajia kupata shilingi bilioni 10 za maji lakini mpaka sasa ambako umebaki mwezi mmoja tumepata shilingi bilioni tano tu na sioni uwezekano wa mwezi mmoja kupata shilingi bilioni tano zilizobaki. Kwa hiyo, kuna tatizo lingine pamoja na bajeti kupungua, lakini kuna hili tatizo pia hata hiyo iliyopangwa pia mwaka unafika fedha hazijapelekwa.

Kwa hiyo, ushauri wangu kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine ni kwamba maji ni muhimu mno na fedha zote zinazopangwa kwa ajili ya maji zinapaswa ziende asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha mchana huu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, vilevile niombe kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri na watendaji wote kwenye Wizara hii, hongereni sana na mnachapa kazi, lakini baada ya kuwapa hongera hizo na nawapeni pole kwa sababu najua mnafanya

kazi kwenye mazingira magumu sana kwa sababu ninajua shida kuwa ya Wizara hii ni rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwenye Wilaya yangu ya Liwale, wilaya ambayo ina vijiji 76 tumebakiza vijiji 11 vijiji ambavyo havina kabisa mradi wa maji. Vijiji vilivyobaki ni Kijiji cha Nahoro, Mkungunyu, Mahonga, Nanjegeja, Chikugu, Mtawango, Lubaba, Liwale B, Lilombe, Turuki na Tuungane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi 11 havina miradi kabisa ya maji, tena Turuki ndio mahali ambapo tumechimba vile visima vitatu ambavyo vinakwenda kulisha Mji wa Liwale. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana ifikapo mwaka 2025 kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi vijiji hivi 11 vipate maji safi na salama na nashukuru katika vijiji vile vitano ambavyo Mheshimiwa Rais ametupa kama zawadi ni miongoni mwa vijiji hivi 11. Kwa hiyo basi, vitabakia vijiji sita naomba sana ifikapo mwaka 2025 vijiji hivi sita vipate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyo vijiji vipatavyo 14, vijiji hivi vimepata maji kwenye vioski kwa maana kijiji kizima wanapata maji sehemu moja. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uone namna ya kuyafikisha maji haya angalau kwenye vijiji vile vipate angalau vilula viwili au hata vitatu. Vijiji hivi ni Kijiji cha Kipelele, Mihumo, Darajani, Kimambi, Mbuli, Kigwema, Luwele, Mtawatawa, Mkundi, Ngongowele, Mikunya, Makinda, Nambinda, Nyera na Mbuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi ina maana kwamba ili upate maji wanapata sehemu moja, kijiji kizima waende sehemu moja kwa hiyo foleni ni kubwa sana. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tupate angalau vilula viwili/vitatu angalau kila kijiji ili watu hawa wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye takwimu ya Mheshimiwa Waziri aliposoma hapa tumefikisha asilimia 90 maji mjini na asilimia 79 maji vijijini, mimi kwangu ni tofauti. Mimi mjini nina asilimia 56 na

vijijini ni asilimia 72 hapa muone ni namna gani pale Liwale Mjini palivyo shida ya maji na shukuru juzi hapa tumepata shilingi milioni 400 na jana nimepigiwa simu na *engineer* wangu pale wilayani anasema kwamba wameshaanza kufanya manunuzi kwa hizi shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana, tunavyoiomba Serikali kutuongezea fedha kwa maana ya kwenda kutekeleza miradi hii, maji ya Liwale Mjini ni shida kubwa sana na hapa nimpongeze sana Meneja wangu wa *RUWASA* pale wilayani anaitwa Ndugu Ruhumbika, anafanya kazi nzuri, pamoja na mazingira haya magumu Ruhumbika anafanya kazi nzuri wakisaidiana na kijana wetu pale Zuberi Mtepetala ambaye yeye yuko pale kwa ajili ya maji mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi najua kinachokutesa wewe Mheshimiwa Aweso ni rasilimali fedha, lakini vilevile na kauli ya Mheshimiwa Rais alisema ukimzingua, anakuzingua na ndio hicho kinachokuahangaisha sana kutafuta fedha huku na huku. Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe sana utekeleza hii miradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa sababu ya muda napenda nitoe taarifa kwamba katika Wilaya yangu ya Muleba, Mkoa wa Kagera miradi ya maji ipo mizuri sana, nashukuru na kukupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kuna mambo mawili; moja bajeti imepungua kwa shilingi bilioni 137 tunashukuru kwa kutunga mkono lakini la pili kuna ushauri wa Kamati kwamba wakandarasi wote wanaodai takribani zaidi ya shilingi bilioni 300 walipwe kabla

ya mwezi Juni, ni mambo mawili tunayaomba; shilingi bilioni 300+ wanazodai walipwe kabla ya mwezi Juni na *Insha Allah* maombi ya walio wengi ni sauti ya Mungu hiyo shilingi bilioni 137 tuongezewe. Kwa nini mimi naomba shilingi bilioni 137 ziongezwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna mradi wa Muleba Magharibi, kuanzia Kasharunga kwenda Kiteme, kwenda Burungura, kwenda Ngenge, kwenda Rutoro, hawa watu ndio wana *water stress* unaposikia *water stress* hawa ndio watu wana *water stress*. Tunawaombea hizo shilingi bilioni 137 tuweze kupata maji namna ile lakini huwezi kuamini katika Ziwa Victoria katika kata zangu tano za Ziwa Victoria Wilaya ya Muleba kuna uhaba wa maji, watu hawana maji ukisikia watu wanakufa kwa kipindupindu ni katikaki ya Ziwa Victoria, ndio maana mimi na mimi nimeungana na Kamati naungana na Waheshimiwa Wabunge kwamba shilingi bilioni 137 zipatikane kusudi Mheshimiwa Aweso mimi ndio najua mihemo ya mgonjwa, unisaidie visiwani watu wasife kwa kiu ndani ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Wizara mlivyotupangia miradi ya maji. Nakushukuru sana Mradi wa Kagoma umeongeza pesa kupeleka maji Nsisha, kupeleka maji Bigaga, kupeleka maji Manyora nakubaliana na wewe uhakikishe kwamba mradi huo unakwenda, lakini nikupongeze kwa Zawadi ya Mama. Zawadi ya Mama vile visima vitano uwaelezee Waheshimiwa Wabunge kwamba maji yatapatikana kabla ya mwezi wa kumi, watu wa Rutoro, watu wa Misambya, watu wa Chebuweke, watu wa Kilamba hiyo zawadi ya mama, mimi ninaileta moja kwa moja lakini tunaitaka zawadi hiyo mwezi wa tisa maji yawe yameshamwagika na watu waweze kushuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo Chuo cha Maji; Chuo cha Maji tumewahi kuwashauri tunaomba mzalishe mafundi zaidi kwa ajili ya ku-*manage* miradi hii, lakini mafundi zaidi kusudi waende kwenye nchi za Afrika zilizotuzunguka kuna uhaba wa mkubwa wa mafundi. Sasa tufundishe vijana wetu hawa wenye shida ya ajira kusudi waweze kwenda katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hili suala la *water stress*. Naungana na mapendekezo ya Kamati kwamba tuweze kutengeneza mtandao wa maji, lakini tulikuwa tunapendekeza kwenye taarifa zetu ya kutengeneza *mini-lake* yaani mabwawa makubwa siyo mabwawa ya shilingi bilioni 35, mabwawa makubwa kusudi haya maji yanayokuja yakatuletea *El-Nino* na kuharibu makazi ya watu tuweze kutengeneza maziwa makubwa yaweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa na mimi fursa ya kuongea machache juu ya maji. Nashukuru Wizara mnafanya kazi vizuri na mimi naungana na Wabunge wenzangu kuomba Serikali hii shilingi bilioni 137 mpewe. Maji ni uhai, maji ni afya na tunaipata wapi? Napendekeza pendekezo lingine tuna pesa inayotokana na *fuel levy* ambayo inakwenda kugharamia masuala ya barabara, reli, *REA* na maji na najua Wizara mnapata shilingi 50 kwenye huo mgao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukapata pesa ya kutosha kutoka kwenye huo mgao. Napendekeza naona Mwanasheria Mkuu yuko hapa, ile sheria iletwe hapa Bungeni haraka sana iwezekanavyo badala ya shilingi 50 maji wapewe shilingi 150 tunaweza tukapata pesa ya kutosha kutoka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili; kwenye mfuko huo napendekeza tuweke utaratibu mzuri na kimsingi napendekeza tu-*borrow a reef* kutoka *Road Fund* mgawanyo wa zile pesa uwekwe chini ya kanuni ambayo inajulikana na pesa nyingi ipelekwe *RUWASA* kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo narudi jimboni. Waziri Aweso ulikuja Muleba, tulikukaribisha vizuri, lakini ulitoa

*commitment* pale nimeangalia kwenye bajeti hujaweka mradi wa Yangiro - Ijumbi na uliutamka wewe pale Buganguzi. Nakuomba utaapopata hili shilingi bilioni 137 ambayo tunakuombea kwa nguvu zetu zote na nina hakika mama anatusikia utakapopata hizi pesa hakikisha huu Mradi wa Yangiro - Ijumbi ambao uliutamka wewe mwenyewe pale Buganguzi uingizwe kwenye hii bajeti.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa miradi ambayo inaendelea kutekelezwa Wilaya ya Muleba mmefanya kazi kubwa na nzuri, tunaomba sasa hii miradi ikamilishwe ili wananchi wa Muleba wakafurahie maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ili kuleta ufanisi kwenye miradi ya maji haya mabomba ambayo yanatumika kwenye miradi ya maji *actually* yanatumia zaidi ya asilimia 60, naomba Wizara iweke utaratibu wa kuagiza mabomba haya moja kwa moja kutoka kwa *manufacturers* ili kupunguza gharama za miradi hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga hoja mkono na shilingi bilioni 137 tuwapatie na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Protas Daud, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia na kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya hususani kule kwetu Manyoni tuna miradi mingi sana ya maji lakini nimshukuru ndugu yangu Aweso na timu yako, Katibu Mkuu mtani wangu Mnyamwezi mzigo mzito umepewa Mnyamwezi kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini na *DG* wa *RUWASA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia maeneo manne; eneo la kwanza kuhusu madeni, *in short* maji ni siasa, kama

hatutawekeza kwenye maji maana yake *we are in trouble* tunaenda kupata shida.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Wizara ya Maji inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 200 na wakandarasi wa ndani. Ningemwomba Waziri wa Fedha kabla hajatuletea bajeti yake hapa ya fedha ahakikishe amewalipa hawa wakandarasi zaidi ya shilingi bilioni 200 *otherwise* mimi nitakuwa wa kwanza kushika shilingi ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi namwahidi Waziri wa Fedha kama hatawalipa wakandarasi shilingi bilioni 200 ambazo anatakiwa awapekee Wizara ya Maji kwa kweli bajeti yake mimi nitakuwa wa kwanza na bahati nzuri mimi tunatoka mkoa mmoja kwa hiyo leo nitamsaliti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili; ningeshauri kuhusu *restructuring* ya *fuel levy,* wenzangu wameongea. Dkt. Kikoyo umeni-*preempt* umeongea. Ukiangalia tumeshafanya mambo mengi upande wa *REA*, upande wa barabara tumefanya mambo mengi, lakini nimesema siasa ipo kwenye maji, huko vijijini ukienda wananchi wanalalamika kuhusu maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye ile *fuel levy* ningeshauri tuipandishe kutoka shilingi 50 angalau iende shilingi 100, shilingi 120 kwa sababu kule kwingine tumeshafanya mambo mengi, hii itampa unafuu Waziri wa Maji atafanya mambo makubwa, tutampa unafuu Rais wetu mwakani tuna uchaguzi, mwaka huu tuna uchaguzi ni miradi mingi sana ya maji bado inachechemea. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kuhusu usimamizi wa Mfuko wa Maji. Wengi wamechangia kuhusu Mfuko wa Maji na nimpongeze sana *CEO* wa Mfuko wa Maji anafanya kazi nzuri, lakini sanjari na la kuongeza fedha kutoka shilingi 50 kila lita mpaka zaidi ya shilingi 100 ningeshauri vilevile tutumie mfano wenzetu wa *Road Fund* ambako wameweka *formula* kwamba tuna *RUWASA,* tuna mabonde, sijui tuna Wizara na kadhalika. Tuweke *formula* kwa mfano tunaweza tukasema *RUWASA*

wapewe 50% ya hela inayotoka *National Water Fund*, labda hawa wapewe asilimia ngapi, lakini ningependekeza kwa sababu ya mahitaji mengi yapo vijijini, nashauri angalau *RUWASA* wapewe zaidi ya 70% ya hela iende vijijini. Siasa ya maji ipo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu hii miradi yetu, wakandarasi wengi sana wa ndani wanadai, mimi pale Manyoni nina Mradi wa Kitinku-Lusilile.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ukija pale kwetu wewe wanakuona kama mfalme wewe na Mheshimiwa Rais, ule mradi ulikaa zaidi ya miaka 15 umeshindikana, lakini umeshaukomboa mkandarasi yule amesha-*commit* hela yake zaidi ya shilingi bilioni nne, anatudai sisi, mwezi uliopita niiuliza swali Bungeni hapa Mheshimiwa Waziri uliahidi mwezi wa tano maji yatatoka Kintinku. Sasa nikuombe Waziri lakini nimeshasema Waziri wa Fedha najua wewe huna shida, shida ipo hujapewe hela, Waziri wa Fedha atupe shilingi bilioni 200 katika hizo shilingi bilioni 200 na ninajua shilingi bilioni nne ipo ya mkandarasi wangu alipwe ili mama aje azindue ule mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant Daud Protas atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, ajiandae

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maji katika bajeti ya mwaka 2025/2025.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kumpongeza Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya lakini kumpongeza Menejimenti yote ya Maji akiwemo dada yetu Mwajuma, Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo machache sana, jambo la kwanza tuna miradi kule ambayo inaendelea na katika bajeti yake ya Waziri hapa nimeiona wamesema kwanza ni kukamilisha miradi inayoendelea, lakini katika Jimbo la Igalula mradi ambao kwangu unaenda kuandika historia ni mradi wa utanuzi wa bomba la Ziwa Victoria kutoka Ibela Mirundi kuja Kigwa na kwenda Goweko - Igalula na Nsololo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana hapa Mheshimiwa Waziri kidogo kwenye bajeti yake hatukuweza kuelewana na nikamlaumu sana nikasema mmetuahidi maji ya kutoka mwezi Desemba, 2022 lakini mpaka mwezi wa sita mwaka jana maji yalikuwa hayajatoka. Alichukua hatua za haraka na kwenda kumfukuza mkandarasi na leo nimshukuru Mheshimiwa Waziri sasa wakandarasi wanakwenda mchakamchaka, kwa sababu ulisimama imara, lakini nilisimama zaidi mimi imara kwa sababu niliongea humu Bungeni, kama nisingeongea nadhani ule mradi ungekuwa umesuasua.

Mheshimiwa Spika, leo mkandarasi wa ulazaji wa bomba kutoka Ibela Mirundi kuja Kigwa yuko *site,* lakini kuna mkandarasi wa ujenzi wa matenki mawili; moja la lita milioni moja na lingine la laki tano, lakini na yule msambazaji wa bomba kwenda kwa wananchi naye yuko *site,* nikushukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nina mradi wa uchimbaji wa bwawa, Mheshimiwa Rais ameleta vifaa na hivyo vifaa miongoni mwa waliokuja katika Mkoa wa Tabora bwawa la kwanza ambalo mnalichimba ni linalotoka katika jimbo langu ambalo ni Bwawa la Kizengi. Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri pale Bwawa la Kizengi mimi nikuombe, kusanya nguvu, peleka kwa pamoja. Pale umeniletea shilingi milioni 300 ukaniletea shilingi milioni 150 leo ukienda pale lile bwawa utaenda kuwafunga watumishi wako wa wilaya na mkoa kwa sababu utaona kama hawajafanya kazi na fedha zimeisha, lakini ukiangalia kiuhalisia kazi imefanyika, lakini hakuna kitu chochote kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukienda pale majani yamejaa na mitambo yako wamekwisha ondoa kwa sababu hakuna fedha. Nakuomba, kwa kuwa mimi ndiyo nilipewa mfano wa majaribio wa hiyo mitambo kama inafanya kazi ukaleta jimboni kwangu, naomba ukamalize lile Bwawa la Kizengi ili liweze kuleta tija kwa wananchi wa Kata ya Kizengi, Miswaki, Loya, Miyenze na Rutende. Wananchi wale watapata maji kwa lile bwawa na ile 85% kwa wananchi wa vijijini nitaweza kuifikia kwa sababu ya hilo bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo Mheshimiwa Waziri, leo nataka nikupongeze yale niliyoyasema kwenye bajeti ya mwaka jana umeyafanyia kwa kiasi kikubwa, nakushukuru sana na namshukuru Mheshimiwa Rais, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na kwa sababu ya ufinyu wa muda naomba nijikite zaidi jimboni.

Mheshimiwa Spika, nilianza kuzungumza utaratibu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kama suluhisho la Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa na mikoa mitatu yote inayozunguka Ziwa Tanganyika. Jambo hili nilianza kulizungumza nikiwa Mbunge wa Viti Maalum 14 Januari, 2016, leo nazungumza tena na nakushukuru uliniona naongea na simu hapa ukanistahi tu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaangalia Bunge wananambia muulize Waziri jambo ambalo tumekuwa tunakuagiza kila wakati, utaratibu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, tunazungumza tunajua kwamba kuna mkakati wa muda mrefu na mkakati wa muda mfupi. Serikali siyo kwamba haijafanya chochote kwenye jimbo langu, kuna miradi

mabalimbali inaendelea, lakini ili kuondoa migogoro kati ya mimi Mbunge na watumishi suluhisho ni maji kutoka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro na kutokuwaamini watumishi, kutengeneza migogoro kati ya wananchi na hawa watu wanaohusika na maji suluhisho ni kutoa maji Ziwa Tanganyika. Ni kwa nini nasema kuondoa migogoro? Mheshimiwa Waziri unajua, umetoa fedha ya dharura, umetupa tena fedha shilingi milioni 400 juzi tu hapa, lakini mpaka sasa ninavyozungumza upatikanaji wa maji kwa mujibu wa wataalamu wako ni 52% lakini wananchi wanasema ukituuliza sisi tutakwambia ni 15%. Unaona utofauti wake? ni kwa sababu maji hawayaoni, hawawezi kusoma wanataka wayaone maji kwa vitendo nyumbani kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nazungumza hapa tunajua kuna habari ya ilani, mimi sina shida na ilani na wewe unajua unatakiwa utekeleze ilani. Kama ilani inasema vijijini iwe 85% tuko mwaka gani huu? Tunaenda kwenye mwaka wa uchaguzi. Kama Nkasi ni 52% unayoizungumza unafikiri huu utaratibu ambao tunakwenda nao, halafu leo hapa mimi Mbunge nikae niseme nakubali eti bajeti ya Wizara ya Maji ipunguzwe, hili jambo haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mipango hii inayopangwa, najua tuna vipaumbele, kama kuna miradi mbalimbali inaendelea hapa nchini ni mradi gani ambao leo utashindwa kuzungumzia maji? Ukikosa ugali, utakula wali; ukikosa wali, utakula ndizi; ukikosa ndizi utakula viazi, lakini ukikosa maji huwezi kunywa soda, soda ni soda na maji ni maji. Ili pongezi hizi ndani ya Bunge unazoziona kwa Waziri ziendelee ni lazima awezeshwe kibajeti. Hawezi kutumia muujiza wowote tofauti na kupewa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge letu tumekuwa tunafanya maamuzi mbalimbali hasa yale ambayo yanahusu maslahi ya wananchi. Jambo hili Bunge lako Tukufu lazima tulisimamie bajeti ya maji iongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaposhangaa bajeti kupunguzwa unajiuliza je, imetekelezwa kwa 100%? Jibu ni hapana. Hakuna madai kwenye Wizara hii? Madai ya wakandarasi ni kibao. Miradi inatekelezwaje kama wakandarasi hawajalipwa?

Mheshimiwa Spika, unaanza kujiuliza kwa hali ya kawaida, hivi walifikiri nini kupunguza bajeti ya maji? Ni kweli walitazama kwamba hakuna mahitaji kwenye nchi hii au walikaa tu kwamba hii bajeti ya maji tuipunguze? Haiwezekani. Ili kwenda huko, upotevu wa maji pamoja na kwamba upatikanaji wa maji ni 52% upotevu wa maji peke yake ni aibu kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, unajua tumeingia mikataba mingapi kwa ajili ya makubaliano ya upotevu wa maji, lakini nchi yetu kama tunaamini upotevu wa maji ni kiasi hiki basi kipaumbele kwenye Wizara yako ni kwenda kukarabati miundombinu ambayo imechakaa kwa sababu kwenye upotevu wa maji inawezekana ni kwenye miundombinu au wizi. Kwa hiyo, kuna shida kwenye usimamizi.

Mheshimiwa Spika, nimeona Wabunge wengi wanazungumza kuhusu kuongeza kutoka kwenye shilingi 50 kwenda shilingi 100. Nakubali lakini lazima tuangalie hao wananchi wana mzigo mkubwa sana, tuone utaratibu maalum utakaofanyika kwenye kwenda kuongeza hiyo fedha tusije kwenda kuathiri wananchi wa chini kabisa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na muda siyo rafiki kwa kweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe atafuatiwa na Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na kwa kuwa muda siyo rafiki nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amefanya mapinduzi

makubwa katika sekta ya maji na namna ambavyo ameendelea kumtua ndoo mwanamke, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu kwamba Bajeti ya Maji iliyotengwa kwa mwaka huu ni bajeti ndogo sana ukilinganisha na Bajeti ya Maji kwa mwaka uliopita ambayo imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 128. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu maji ni maisha na maji ni maendeleo, kwa hiyo basi bajeti hii iongezwe ili miradi ambayo haijakamilika hasa katika mkoa wangu wa Singida iweze kukamilika kwa wakati na wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Mradi wa Maji Kintinku - Lusilile. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge Dkt. Chaya amekuwa akiupigia kelele sana mradi huu, lakini bila ya mafanikio mradi huu bado haujakamilika kwa kuwa ni mradi wa muda mrefu sana. Kaka yangu Mheshimiwa Aweso, nakuomba wewe ni msikivu mradi huu wa maji sasa hivi ukamilike na kwa kuwa umefikia 90% basi naiomba sana Serikali iweze kutoa fedha zilizobaki kwa mkandarasi ili huu mradi uweze kukamilika kwa sababu wananchi wa Kintinku - Lusilile wameteseka kwa muda mrefu sana kwa kukosa majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini upo Mradi wa Maji Nyahaa, hapa pia nielezee masikitiko yangu, mradi huu wa maji umekamilika, sitaki kusema kwamba umekamilika, kwa sababu umegharimu fedha nyingi, lakini mradi huu hautoi huduma ya maji. Mradi huu uko Kata ya Mpambala, Mkalama, wananchi wa Kata hii wanateseka sana na wanawake wanatembea kwa umbali mrefu na ukizingatia kata hii haina miundombinu mizuri ya barabara, hivyo wananchi wanateseka sana hasa wanawake wa Kata ya Mpambala katika Jimbo la Mkalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utakapokuja ku-*wind up* hapa utuambie ni kwa nini mradi huu umegharimu fedha nyingi za walipa kodi, lakini hautoi maji. Wameteseka toka mwaka 2014. Naomba suala hili liangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza sana watendaji wa *RUWASA* katika Mkoa wangu wa Singida wakiongozwa na Ndugu Lucas Saidi, wanafanya kazi nzuri sana na iliyotukuka, lakini wana changamoto kubwa ya ukosefu wa magari. Jiografia ya Mkoa wa Singida ina changamoto kubwa sana, unaweza kutoka Kijiji kimoja kwenda kijiji kingine ni kilometa 270.

Sasa kwa namna hiyo naiomba sana Serikali iangalie uwezekano wa upatikanaji wa magari katika Wilaya zangu za Mkalama, Singida Vijijini, Iramba, Manyoni pamoja na Ikungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Andrea Mathew Kondo, Mtoa hoja ajiandae, Kundo, samahani.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kuahirisha Mjadala, Kanuni ya 79.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kundo hebu keti kidogo, ehee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba niirejee Kanuni.

**SPIKA:** Wewe endelea kuelezea hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba Kanuni ya 79 inazungumza kwamba Mbunge anayependa mjadala unaoendelea uahirishwe anaweza akatoa hoja kufanya hivyo.

**SPIKA:** Wewe endelea na hoja yako Kanuni ninayo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tuko kwenye kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji Fungu la 49. Tumesikia michango ya Wabunge mbalimbali ambayo ina mantiki kabisa ikizungumzia namna ambavyo Wizara hii imepewa pungufu ya

bajeti ya shilingi bilioni 137 pungufu ya bajeti iliyopewa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, ukisoma maelezo ya Kamati yetu ya Bunge yameeleza maeneo 15 muhimu ambayo ni changamoto kutokana na upungufu wa bajeti husika. Ukisoma ukurasa wa 29, 30 na 31 maeneo 15 muhimu, miongoni mwao ni madeni ya wakandarasi na vitu vingine vingi. Sasa kwa nini nimesema hivi?

Mheshimiwa Spika, Waziri na Naibu Waziri wakishahitimisha na sisi tukishapiga kura na kupitisha maana yake ni kwamba Wizara ya Maji bajeti yake itakuwa ndiyo hiyo ambayo tumeipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna namna tutapitisha leo, pamoja na kwamba tunampenda sana kijana wetu tukaja tukamwambia Mwigulu huko baadae abadilishe. Sasa naomba iahirishwe mpaka lini? Kwa sababu nina *room* hiyo ya kupendekeza. Leo ni Ijumaa, tumeshajadili imefika tu kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ya Bajeti inakutana kila siku katika kipindi hiki cha Bunge, waende wakae na Wizara ya Fedha, siku ya Jumatatu kabla hatujaanza kujadili bajeti nyingine tuambiwe shilingi bilioni 137 zinapatikana wapi ili kuweza kujazia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge ndiyo tunaopitisha bajeti. Serikali inatuletea mapendekezo, haina mantiki... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima malizia hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilikuwa nishapa mizuka nilikuwa nataka kuchangia. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Naona unaanza kuchangia, malizia hoja yako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya nilikuwa naomba huu mjadala uahirishwe kwa muda mpaka

siku ya Jumatatu ili Wizara ya Fedha ikakae na Kamati ya Bajeti, iangalie maeneo ambayo itachambua chambua yako mengi, Mpina na Wabunge wameyasema mengi ili fedha ipatikane.

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa tuketi. Mlikuwa mnanisaidia kuhesabu eeh?

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Halima Mdee hapa kutumia Kanuni yetu ya 79 inayomruhusu Mbunge kusimama na kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na ametueleza ni sababu gani anayotaka mjadala uahirishwe. *(Kicheko)*

Nadhani sote tumemsikia kwa hiyo sina haja ya kuzirejea hizo lakini sehemu moja tu Mheshimiwa Halima Mdee anasema, tukishafika mahali ambapo Mheshimiwa Waziri atapewa nafasi ya kuhitimisha hoja yake tukaingia kwenye Kamati ya Matumizi, tukifanya maamuzi hakutakuwa na nafasi tena ya kufanya mabadiliko ambayo Wabunge wengi wameyazungumzia.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 124 inazungumzia kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali kusomwa Bungeni. Ili nifupishe muda wa maneno nitawasomea kanuni ya 124(1), (2) na (3).

Waheshimiwa Wabunge, fasili ya kwanza; "Baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa makadirio ya Wizara zote ndani ya siku sita kabla ya hotuba ya bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata."

Fasili ya pili, "Katika kipindi cha kufanya majumuisho kwa mujibu wa fasili ya kwanza, Bunge litaendelea na shughuli zake

nyingine kama zitakavyokuwa zimepangwa na Spika baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi."

Fasili ya tatu, "Wakati Serikali ikifanya majumuisho kwa mujibu wa fasili ya kwanza Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa nafasi nafasi zao watakuwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti."

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii aliyoileta Mheshimiwa Halima hapa ukiisoma Kanuni ya 124 tukishamaliza Bajeti za Kisekta za Wizara zote tunakaa sasa sisi kama Bunge na Serikali kwa maana ya Kamati yetu ya Bajeti tunakaa na upande wa Serikali na kipindi hicho Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge wanakuwa ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti.

Kwa hiyo, hoja zote zilizojadiliwa hapa ndani ambazo mmezungumza na Mawaziri wamezichukua, lakini pia hoja zote zilizoletwa kwenye vile vitabu ambavyo Kamati zetu zimeleta hapa ndani kipindi hicho cha siku sita ndicho ambacho tunapata nafasi ya kufanya hayo marekebisho. Sehemu pekee ambapo hatutaruhusiwa kufanya marekebisho, nilikuwa najaribu kuangalia hapa ni Kanuni ipi, ahaa Kanuni ya 125 ni baada ya Bajeti Kuu ya Serikali ikishasomwa hapa ndani, wakati wa ule mjadala hatupendekezi mabadiliko. Hata hivyo ukipendekeza mabadiliko maana yake wewe ulete hela zitatoka wapi, siyo kwamba unakatazwa kabisa. Unaruhusiwa ukileta hoja kwamba hili tunapoondoa basi na wewe unaleta tuweke lipi kwa sababu Serikali inakuwa imeshasema sasa kwamba inakuwa imeshataja ule ukomo wa bajeti yake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo Mheshimiwa Mbunge hoja yake iko sahihi kwa maana ya kwamba Wabunge wamejadili sana hoja hiyo, lakini kwa maana ya kusema kwamba tukipitisha hapa basi hakuna nafasi tena ya Bunge kuitazama bajeti hii ya Wizara ya Maji kwa mujibu wa Kanuni ya 124 nafasi hiyo ipo wakati wa zile siku sita na kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Maji na wale Wajumbe wengine wa Kamati bila shaka wamesikia hoja za Wabunge na hapa tutakapohitimisha leo tutaiagiza Kamati ya Bajeti kile kinachopaswa kufanywa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu, ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nianze na mchango wangu kuhusu utaratibu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika ambalo ndilo suluhisho la kumaliza changamoto ya maji Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma. Mradi huu kwa umuhimu wake unatakiwa kufanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, aidha Mfuko wa Maji hauna pesa za kutosha, naishauri Serikali itafute vyanzo vingine ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Pia Wizara iwalipe wakandarasi hasa wazawa ili wamalize kazi zao kwa wakati na waendelee kuaminiwa na wasivunjike moyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri bajeti ya Wizara ya Maji iongezwe kwani kuna mahitaji mengi ili kutatua changamoto za maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na uvunaji wa maji hasa kwenye maeneo yenye mvua nyingi kama Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Nkasi tunahitaji gari kwa watumishi, wanahangaika sana kutimiza majukumu yao.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi wote wa Wizara wakiwemo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote. Pia nawashukuru kwa kukamilika kwa mradi wa Chankorongo unaopeleka maji Mji Mdogo wa Katoro, naishauri Serikali sasa iendelee kutoa pesa kwa ajili ya usambazaji ili kuongeza mtandao na wanufaika wa mradi. Kutokana na wingi wa wananchi (takribani 300,000 kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022) eneo hili inabidi liongezewe vyanzo ili kuimarisha upatikanaji wa maji kwenye mji huu mdogo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Busanda lina kata 22, hivyo tunaomba miradi ya visima na mtandao wa usambazaji kwenye kata zote 22. Ikumbukwe Jimbo la Busanda kuna uchimbaji wa madini hivyo uchenjuaji wa madini kwa kutumia *mercury* (zebaki) na *cyanide,* ni changamoto kubwa kwa upatikanaji maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, visima vyote vilivyochimbwa miaka iliyopita viwezeshwe kwa kupata umeme ili usambazaji uwe rahisi na wa tija.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kuwa maji ni uhai na maji ni uchumi pia. Bila maji safi na salama hatutakuwa na Taifa lenye watu wenye afya bali tutatumia gharama kubwa kutibia wananchi wote wanaopata maambukizi ya magonjwa mbalimbali yatokanayo matumizi ya maji yasiyo safi wala salama na magonjwa hayo ni kama kichocho, kuhara, homa ya matumbo *(typhoid)*. Bila maji ya uhakika shughuli mbalimbali za maendeleo zitakwama, kwa mfano uzalishaji wa umeme, shughuli za ujenzi, kilimo, ufugaji na hata viwandani. Hivyo maji ni moja ya kichocheo muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nyingi kwa kweli ambazo zinafanya na Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha inamtua mama ndoo kichwani, lakini bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma ya maji hasa maeneo ya vijijini. Takwimu zinazotolewa na Serikali za kuonesha kwa wastani asilimia ambazo huduma za maji zimefika vijijini na mijini, lakini ukweli ni kuwa bado maeneo mengi hayajafikiwa na maji kwa kuzingatia sera yetu ya maji, kwa mfano ni takwimu ya kuwa vijiji vimefikiwa 9,737 kati ya 12,318. Hapa kwa haraka haraka utaona

kuwa huduma imeshafikishwa kwa asilimia kubwa ilhali ni tofauti kabisa maana unakuta huduma hii kwenye kijiji husika imegusa sehemu ndogo tu tena ya kitongoji kimoja kwenye kijiji husika huku ikiacha vitongoji vingi bila huduma hii na hivyo kufanya asilimia za upatikanaji kwa huduma za maji kiuhalisia kuwa chini ya asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuboresha huduma ya maji safi hasa vijijini, tuna jukumu la kuhakikisha tunaongeza vyanzo vya mapato kwenye Mfuko wa Maji ambao unahudumia maeneo matatu ambayo ni mabonde, maji mijini na maji vijijini. Kwa sasa mfuko huu unachangiwa na tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta. Naungana na maoni ya Kamati ambayo imeshauri ongezeko la tozo kwa kila lita moja ya mafuta kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100. Hizi zitasaidia kuboresha huduma za maji vijijini ambapo tumeona utekelezaji wake unasuasua na kupelekea wakandarasi kutolipwa kwa wakati na kupelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi hata kama haina riba kwa kuwa wakandarasi wengi wanatekeleza miradi ya maji vijijini ni wakandarasi wazawa ambao hata wakicheleweshewa malipo huongeza muda wa kukamilisha miradi bila riba. Hili si tu linaathiri ufanisi wa wakandarasi bali miradi inakosa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi nashauri Bunge lako Tukufu tuazimie kuongeza tozo hadi shilingi 100 kwa kila lita moja ya mafuta, lakini pia Mfuko wa Maji uige jinsi ambavyo Mfuko wa Barabara unagawa yale mapato ya tozo kwenda *TARURA* na *TANROADS* ambapo 30% kwenda *TARURA* na 70% kwenda *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mfuko wa Maji uboreshe kanuni zake za uendeshaji kwa kuhakikisha unaweka mgawanyo wa asilimia kwenye mabonde *(RUWASA and UWASA),* kwa mfano 60% iende *RUWASA*, 20% iende maji mijini na 20% iende kwenye mabonde.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wazawa wanapitia madhira makubwa sana kwa kutolipwa kwa wakati hata pale unakuta *certificate* imeshatolewa. Tukumbuke wakandarasi

wazawa hawana riba kwenye miradi/mikataba yao hata pale wanapocheleweshewa malipo kama vile ambavyo wakandarasi wageni wakicheleweshewa tu malipo kwenye miradi inakuwa ina-*generate* riba.

Mheshimiwa Spika, vilevile nipongeze matumizi ya *pre-paid meter,* hii itasaidia sana kupunguza malalamiko ya kubambikiwa *bill* ya maji, lakini pia kumpa unafuu mtumiaji kwa kulipia maji kwa kadri anavyotumia. Lakini pia itasaidia kwa wadaiwa sugu ambao wengi wao ni taasisi za Serikali ambazo zinadaiwa mabilioni ya fedha kwa muda mrefu na kupelekea mamlaka za maji kushindwa kujiendesha. Hivyo *pre-paid meters* zitasaidia sana na kuwa mwarobaini kwa taasisi ambazo zimekuwa hazilipii *bill* zao za maji maana sasa watatakiwa kulipia kabla ya kutumia kama vile wanavyofanya kwenye umeme. Hii itasaidia kuongeza mapato kwenye mamlaka zetu za maji na hivyo kuweza kujiendesha vyema.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuishauri Serikali juu ya upotevu mkubwa wa maji ambao hufanywa kwa njia mbalimbali kama vile wizi wa maji kwa kuchepusha *line* na kutumia maji bila kupita kwenye *meter,* kutokana na uchakavu wa miundombinu, kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu kama ujenzi wa barabara na ujenzi wa nyumba ambapo huchimba misingi ambayo huaribu miundombinu hata kama siyo chakavu sambamba na majanga mbalimbali kama vile mafuriko, mmomonyoko wa udongo na kadhalika. Natambua Serikali sasa inafunga mtambo wa kutambua *leakages* mbalimbali ili ziweze kutatuliwa kwa wakati na kudhibiti upotevu mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kusisitiza ukamilishaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria wa Rorya - Tarime ambao umeanza, lakini utekelezaji wake kasi siyo ya kuridhisha, hivyo ningependa kujua lini wananchi wa Rorya na Tarime watarajie kupata huduma ya maji kutoka Ziwa Victoria. Vilevile wakati tunasubiri mradi huu nilishafikisha ombi langu la kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi na wanafunzi wa Sekondari ya Tagota iliyopo Kata ya Kenyamanyori, Sekondari ya Nyandoto iliyopo Kata ya Nyandoto na Sekondari ya Nkongore iliyopo Kata ya Ketare, hizi zote zipo

Halmashauri ya Mji wa Tarime ambapo wanafunzi na wananchi wanatembea umbali mrefu kutafuta maji kitu ambacho kinaathiri muda wao wa kujisomea na kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime nilifikisha ombi la kupatiwa kisima kwenye Kitongoji cha Songambele kilichopo Kijiji cha Nyabirongo, Kata ya Susuni ambapo kuna soko na zahanati pamoja na Kijiji cha Kiongera chenye zahanati na shule ya msingi.

Mheshimiwa Spika, tukipata hivi visima pamoja na vile vitano vya kila jimbo vitasaidia sana kama *short time solution* wakati tunasubiri maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, suala la upotevu wa maji mijini na vijijini linaendelea kwa kasi kwa sababu watu wengi hawaelewi kama kuvuja maji kwa matone kidogo kidogo ni upotevu mkubwa na husababisha *bill* za maji zinakuwa kubwa sana. Wananchi waelimishwe juu ya utengenezaji mabomba mara tu yanapoharibika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuvuna maji ni muhimu sana nalo likatolewa uelewa. Chalinze waliweza kuvuna maji kila nyumba wakati huo maji yalikuwa ni shida sana. Hebu halmashauri zione namna ya kuwezesha wananchi waweze kuvuna maji kwa maeneo yenye shida ya maji wakati wa kiangazi. Elimu itolewe na pia mabwawa yajengwe kule kwenye maji kama *block farm* Tabora kwa matumizi ya mashamba na mifugo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, moja, tunaomba shule zote za Serikali zipewe maji kwa bei ya chini au *flat rate* ya shilingi 100,000 mpaka shilingi 200,000 kwa mwezi na shule za binafsi shilingi 200,000 hadi shilingi 300,000 kwa mwezi. Labda kwa zile zinazotumia maji chini ya hela hiyo. Fedha hizo ziongezwe kila mtu mwenye bili ya maji atoe shilingi 1,000 au shilingi 500 kwa vijijini, kila mwezi kuchangia bili hizo za maji kwenye shule.

Mheshimiwa Spika, pili, sehemu zozote zinazoweza kujengwa au kuchimbwa mabwawa hata kama ni madogo yachimbwe ili kuongeza matumizi ya maji yanayopotea nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, tatu, sehemu nyingi za vijijini au maeneo ya mijini yenye sura za vijiji, wachimbiwe visima kama inawezekana kupata maji hayo kuliko kupeleka maji ya bomba kutoka mbali wakati watu wanaoishi huko na wanaohitaji hayo maji wako wachache.

Mheshimiwa Spika, nne, ninashukuru kwa maji zaidi ya 97% yaliyosambazwa katika Jimbo la Iringa Mjini na kwa mipango mizuri ya kufikia 100%; pamoja na kupunguza bei ya bili za maji ndani ya Jimbo la Iringa. Tunaomba mradi wa maji ya Mtitu utekelezwe, na mradi wa mtandao wa maji taka, pia ukamilike. Ahsanteni sana.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha anamtua ndoo kichwani mama wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumpogeza Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja Naibu Waziri wake, bila kumsahau Katibu Mkuu pamoja na timu yote ya watalam kwani wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kumshukuru Rais kwa kutupatia miradi ya maji katika Jimbo la Lushoto. Pia tunashukuru kwa kupewa kwa kila jimbo visima vitano katika kila jimbo.

Mheshimiwa Spika, kama waswahili wanavyosema kuwa kushukuru ni kuomba tena, Jimbo la Lushoto lina vyanzo vingi vya maji hasa ya msererreko, kwa minajili hiyo, kuna chanzo cha maji ambacho kipo kwenye Msitu wa Magamba maeneo ya Heluli Mtaa Namba Tisa na wataalam wameshafika maeneo hayo, na usanifu umeshafanyika, tunachosubiri kwa sasa ni mradi kupewa pesa ili uanze, na mradi huu ukikamilika utaweza kuhudumia zaidi

ya kata 13 kati ya kata 15; kwa hiyo mradi huu ukikamalika utakuwa umemaliza kabisa tatizo la maji katika Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Spika, kata zitakazopitiwa na mradi ni hizi zifuatazo; Magamba, Migambo, Kwai, Malibwi, Kwekanga, Mbwei, Mlola, Makanya, Lushoto, Ubiri, Gare, Kwemashai na Ngulwi. Hizi ndiyo kata zitakazopitiwa na mradi pamoja na vijiji vyetu. Kwenye mradi huu tunaomba tuangaliwe kwa jicho la pekee ili tuweze kupewa pesa na mradi huu uweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, pia Jimbo la Lushoto ni la milima na mabonde, kwa hiyo kuna haja ya kujenga mabwawa katika maeneo haya yafuatayo kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko pamoja na mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa pamoja na ardhi yenye rutuba kutosombwa kwenda mabondeni. Maeneo hayo ni pamoja na Boheloi, Ubiri, Kwabonda, Yogoi, Kimunyu, Kwai Kizungu, Ntambwe, Ngindoi, Mavongo, Mzilagembei, Mhezi, Mgambo, Mazashai Mtae, Hondelo, Mdando na Kwemshazi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Wizara kwa kuja na mita za *pre-paid,* kwani zitakuwa ni suluhisho hasa kwa watu wasiokuwa waaminifu hasa katika kubambika bili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso (Mb) kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025. Ni hotuba nzuri iliyojaa mafanikio na mipango mizuri ya kutatua changamoto zilizoko kwenye sekta ya maji na matokeo tumeanza kuyaona. Hongera sana.

Pia niipongeze Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa taarifa yake nzuri ambayo imefanya uchambuzi na kufafanua mambo mengi kwa kina ambayo yanatusaidia sana Waheshimiwa Wabunge kutoa michango yetu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kuanza kutekeleza mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi Mkoani Simiyu *(Simiyu Climate Resilience Project-SCRP)* katika wilaya tano za Mkoa wa Simiyu ambazo ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu ambao unatarajia kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 444.6.

Mheshimiwa Spika, kwa wasiojua historia, mradi huu uliasisiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2016 chini ya uongozi wa Makamu wa Rais wa wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unatokana na msukumo wake tangu andiko la mradi na sisi wasaidizi wake tulihakikisha ajenda hii hairudi nyuma wakati huo mimi Mpina nikiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na leo tunashuhudia mradi mkubwa wa mabadiliko ya tabia nchi umeanza kutekelezwa. Ahsante sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yako isiyoyumba ya kutekeleza mradi huu tangu ukiwa Makamu hadi Rais wa nchi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Wilaya za Mkoa wa Simiyu ambao wameathiriwa sana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo uhaba wa vyanzo vya maji ya kunywa, uhaba wa maji kwa ajili ya kilimo, mifugo na shughuli zingine za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Serikali kuanza kwa kasi utekelezaji wa mkakati wa kuwa na Gridi ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito na mabwawa kwa ajili ya kupeleka maji katika maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika, Wizara ianze utekekezaji wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kupeleka maji katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi, kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mkoa wa Mtwara, Mto Rufiji kwenda Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani na Lindi na Ziwa Nyasa kwenda Mkoa wa Ruvuma, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji taka yanayorudishwa kwenye mazingira; kuna changamoto kubwa katika usimamizi na

uondoshaji wa majitaka kwenda kwenye mazingira, majitaka yanapaswa kutibiwa na kufikia viwango vya kuruhusiwa kwenda kwenye mazingira. Ili kutekeleza jukumu hilo ni lazima katika maeneo ya makazi, viwanda, migodi na kadhalika pawepo na miundombinu ya kutibu majitaka *(wastewater treatment facilities)* kama mabwawa ya majitaka *(Waste Stabilization Ponds-WSPs)*, mitambo ya kutibu majitaka *(Effluent Treatment Plant-ETP)* na kadhalika kabla ya kuruhusu majitaka hayo kwenda kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mingi ni michakavu na haifanyi kazi sawasawa na maeneo mengine hayana kabisa miundombinu ya majitaka. Aidha, imebainika kuwa 57.8% ya mifumo ya majitaka haikidhi viwango vya ubora wa majitaka kwa ajili ya kurudishwa kwenye mazingira. Pia mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 12 hazijaanza kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya usafi wa mazingira ili kuweza kutoa huduma ya ukusanyaji na utupaji wa majitaka.

Mheshimiwa Spika, kama kuna mifumo dhaifu kiasi hiki ya usimamizi wa ubora wa majitaka tutalinda vipi usalama wa vyanzo vyetu vya maji, tutakwepaje magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kansa na magonjwa mengine ya kuhara na kuhara damu, vifo vya binadamu na mifugo. Waziri wa Maji, Waziri wa Mazingira na *NEMC* mko wapi haya yanatokea katika migodi, viwanda na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mgodi wa *North Mara* ulikuwa na mabwawa ya majitaka yenye kemikali *(Tailings Storage Facilities-TSFs)* ambayo kwenye kitako chache hayakuwa na kinga ya kuzuia majitaka kupenya ardhini *(liners)* na hivyo kuruhusu kwenda kwenye mazingira na vyanzo vya maji. Hadi sasa hatujaarifiwa kama mgodi huo umesharekebisha kasoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upotevu wa maji kabla ya kufika kwa wateja *(Non-Revenue Water-NRW);* mamlaka nyingi za majisafi na usafi wa mazingira zimekuwa zikiripoti upotevu mkubwa wa maji kabla ya kuwafikia wateja na kuleta hasara

kubwa kwa mamlaka na wananchi kukosa maji. Hivi sasa hasara ya upotevu wa maji katika mamlaka imefikia shilingi bilioni 162.25 katika mwaka wa fedha 2022/2023 na viwango vya upotevu vinavyoripotiwa ni zaidi ya 20% inayoruhusiwa na *EWURA*. Baadhi ya mamlaka zina upotevu mkubwa wa maji kati ya 41% hadi 65%, hapa tunafanya kazi ya kuzalisha maji au kupoteza maji?

Mheshimiwa Spika, wananchi katika maeneo ya Kigoma, Ngara, Mtwara, Arusha, Korogwe, Karatu, Dar es Salaam, Kyela, Kasumulu na kadhalika wanateseka kwa migao na katakata ya maji isiyoisha huku wakitozwa tozo kubwa kufidia hasara. Waziri umeruhusu vipi mambo haya?

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya madeni ya wazabuni na wakandarasi yamefikia shilingi bilioni 400, kuchelewa kulipwa wakandarasi hao kunaongeza gharama za ujenzi kutokana na riba, mradi kuchelewa na wakandarasi kufilisika hasa wakandarasi wa ndani ya nchi. Leo tunatenga shilingi bilioni 558.115 kwa ajili ya maendeleo huku Wizara ikiwa inadaiwa na wakandarasi shilingi bilioni 400, wakati huo pia tukitangaza miradi mipya lukuki, hivi kweli tuna nia ya dhati kupeleka maji kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, wilayani kwangu Meatu madai ya wakandarasi wadogo ni zaidi ya shilingi bilioni 1.5 ambapo wamekuwa wakipigwa danadana kila leo kulipwa malipo yao. Wakandarasi (makampuni) na familia zao zimefilisika huku miradi ilishajengwa na kukamilika na inatumiwa na wananchi, huu ni ukatili wa hali ya juu kwa wananchi wetu. Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake aniambie fedha za wakandarasi waliojenga Miradi ya Maji ya Itinje, Lubiga, Bukundi, Mwamalole na Sakasaka zinalipwa lini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa uzalishaji maji; baadhi ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zinazalisha maji kidogo ikilinganishwa na uwezo wa miundombinu *(underutilization of installed infrastructure capacity)* hali inayosababisha migao na katakata ya maji kwa wananchi na kuleta usumbufu mkubwa wa kutafuta maji, kwa mfano Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi inazalisha maji katika

mita za ujazo asilimia nane tu ya uwezo wake kwa siku, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ambayo ina chanzo cha uhakika cha Ziwa Victoria ina upungufu wa kuzalisha maji katika mita za ujazo 24% ya uwezo wake, Waziri atuambie nini kinasababisha hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za maendeleo, katika mwaka wa fedha 2024/2025 fedha za maendeleo zimepungua kwa 18.4% ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 katika mwaka huo wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 558.115 zimetengwa kugharamia miradi ya maendeleo zikiwa ni pungufu kwa shilingi bilioni 137.7 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka jana. Programu, mipango na mikakati iliyowasilishwa na Waziri wa Maji haiwezi kutekelezwa kwa utengaji wa fedha wa namna hii. Waziri amewasilisha miradi mipya mingi, malimbikizo ya madeni zaidi ya shilingi bilioni 400, mamlaka za maji kushindwa kuzalisha maji kulingana na mahitaji, kukosekana kwa miundombinu ya majitaka na upotevu mkubwa wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu, migao na katakata ya maji isiyoisha halafu tunafika kwenye kutenga fedha tunapunguza fedha za maji.

Waheshimiwa Wabunge, tusikubali kupunguza fedha za maji na badala yake ziongezwe zaidi ili kukabiliana na changamoto za maji tulizonazo nchini. Hauwezi kupunguza fedha za maji wakati mradi wa mkubwa wa kimkakati wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umekamilika uliokuwa tunatumia takribani shilingi trilioni 1.5 kila mwaka. Hauwezi kupunguza fedha za maji na kupeleka fedha kwenye ruzuku ya mbolea shilingi bilioni 150 ambapo wanapata wakulima 25% tu, fedha za ruzuku ya mbolea zipelekwe kwenye maji na mbolea tutumie mfumo wa *BPS* ambao utaleta unafuu zaidi wa bei kwa wakulima kuliko hata mpango wa mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kupunguza bajeti ya Maji huku kuna fedha zimeshikiliwa kwenye mapingamizi katika Mahakama za *TRAB* na *TRAT* zaidi ya shilingi trilioni 10.5 na bila sababu za msingi. Hata tukishinda kwa 57% ni sawa na shilingi trilioni 5.7.

Mheshimiwa Spika, nashauri bajeti ya Wizara ya Maji isipungue na badala yake tuongeze fedha hadi shilingi trilioni 1.5 ili kukabiliana na changamoto za maji tulizonazo nchini. Vyanzo vya fedha tunavyo, miradi tunayo, Waziri wa Maji mchapakazi, mnyenyekevu na mwadilifu tunaye, hatuwezi kushindwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tutume salamu kwa wananchi na dunia nzima kuwa tuna Rais mwanamke aliyeamua kwa dhati kutatua changamoto za maji na kuleta faraja na furaha kwa akina mama wenzake wanaoteseka na shida ya maji usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, pia ushindi tulioupata katika Programu ya *P4R* ambapo Tanzania imeshika nafasi ya kwanza kati ya nchi zaidi ya 50 duniani kufanya vizuri katika utekelezaji wa programu hiyo na Benki ya Dunia kuamua kuiongozea nchi yetu fedha za utekelezaji kutoka dola za Marekani milioni 350 hadi dola za Marekani milioni 654. Haya ni mafanikio makubwa ya kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya hati fungani ya kijani; huu ni ubunifu mzuri kwa Wizara kuanza kutekelezwa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ambapo itasaidia kupanua wigo wa mapato na upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya upanuzi, usambazaji maji na ukarabati wa miundombinu ya maji, na hivyo kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za maji kwa wananchi na kuipunguzia mzigo Serikali.

Mheshimiwa Spika, jaribio lililofanywa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga *(Tanga UWASA)* la kuuza hati fungani za kijani na kufanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 54.72 sawa na 103% ya lengo linatia matumaini. Tunataka Mawaziri wabunifu kama wewe Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Spika, rai yangu; utoaji wa hati fungani hizi ufanyike kwa uangalifu na usimamiwe kwa karibu ili mapato yanayopatikana yatumike kwa shughuli zilizopangwa pamoja na kurejesha mikopo. Wizara ihakikishe kuwa mamlaka zingine za maji nchini zianze kutoa hati fungani kama hii ya *Tanga UWASA*.

Kuhusu usimamizi wa vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii *(CBWSOs);* hatujasahau miradi ya ngazi ya jamii ilivyokuwa na changamoto nyingi katika uendeshaji, ikiwemo kushindwa kufanya matengenezo kwa wakati, miradi mingi kusimama kutoa huduma kwa sababu ndogo ndogo, upotevu wa mapato, mizozo na migogoro isiyoisha ya jumuiya ya watumiaji maji.

Mheshimiwa Spika, jitihada zilizochukuliwa na Wizara kupitia *RUWASA* ya kusajili *CBWSOs* 1,382 na kuajiri wataalam wapatao 5,342 katika kada za ufundi, uhasibu pamoja na kada saidizi ambayo imeboresha hali ya uendeshaji na utoaji wa huduma ya maji vijijini, tunashuhudia miradi mingi iliyokuwa imesimama imeanza kufanya kazi, hali ya upotevu wa mapato imepungua na hata ukaguzi wa *CAG* katika jumuiya 133 zilizokaguliwa 98% zilipata hati safi.

Mheshimiwa Spika, nimeshindwa kujizuia kukupongeza tena Mheshimiwa Waziri Aweso kwa mageuzi makubwa unayofanya kwenye Wizara ya Maji, wito wangu muundo wa *RUWASA* ngazi ya wilaya uwe na timu ya wataalam ambao kazi yao itakuwa ni kukagua miradi ya *CBWSOs* mara kwa mara na kuhudhuria vikao vya kila robo mwaka ili kuzijua changamoto na kuzitatua kwa wakati na kuhakikishia wananchi wanapata maji muda wote na bila kisingizio chochote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maji Jimbo la Kisesa; miradi ya maji iliyokamilika na inayoendelea kujengwa katika Jimbo la Kisesa yenye thamani ya shilingi bilioni nane, Mradi wa Maji Mwaukoli, upanuzi wa Mradi Mwandoya, Mradi wa Mwandu Itinje, Mradi wa Inonelwa, ujenzi wa Mradi wa Maji Semu-Mbalagane na Mwabuma-Mwashata. Katika miradi ya maji ambayo imekamilika wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji vizuri huku wakisubiri kwa hamu kukamilika kwa miradi inayojengwa. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kisesa niipongeze sana Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, madeni ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, hadi kufikia

Juni, 2023 yalikuwa yamefikiwa shilingi bilioni 136.17 huku uwezo wa kukusanya madeni hayo ukiwa mdogo sana na madeni haya kwa sehemu kubwa zinadaiwa taasisi za Serikali, kwa mfano *DAWASA* hulimbikiza madeni ya wastani wa shilingi bilioni 11.3 kila mwaka, nini sababu ya ulegevu huu kwa mamlaka hadi madeni yamekuwa kwa kiwango hicho na kuongezeka kila mwaka?

Kuhusu ushuru wa maji na upangaji wa viwango; kumekuwepo na malalamiko ya wananchi kuhusu viwango vya ushuru na tozo zinazotozwa na vyombo vya *CBWSOs* kuwa viwango hivyo ni vikubwa kiasi cha wananchi kushindwa kumudu gharama, sehemu zingine ndoo moja ya lita 20 inatozwa hadi shilingi 200 kiasi ambacho wananchi wengi wanashindwa kumudu gharama hizo na kulazimika kuendelea kutumia maji ya kuchota mtoni na kwenye visima vya asili. Pia bei zinatofautiana kila *CBWSOs,* kwa nini *RUWASA* mmeruhusu haya? Kwa nini kusiwepo na kanuni ya fedha ya pamoja itakayoweka viwango sawa nchi nzima na kuondoa urasimu uliopo sasa *(Unified Financial Regulations)*. Miradi ya *CBWSOs* ni ya wananchi, ni lazima bei ziwe ndogo ambazo hadi mwananchi wa chini ataweza kumudu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuondoa matumizi ya nishati ya dizeli kwenye skimu za maji vijijini; miradi mingi ya maji vijijini bado inatumia nishati ya mafuta ya dizeli na hivyo kupelekea gharama za uendeshaji kuwa kubwa, ninajua Wizara kupitia *RUWASA* ilishaanza kutekeleza mradi wa kuondoa matumizi ya nishati ya dizeli kwenye skimu za maji na kuweka matumizi ya umeme wa gridi na umeme wa jua, najua kuna mpango unaotekelezwa na Wizara kupitia programu ya *Accelerating Solar Water Pumping via Innovative Financing-ASWPIF* inayohusisha *RUWASA*, Benki ya Dunia na *TIB.*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kisesa mradi katika Kata ya Sakasaka bado unatumia nishati ya mafuta, ninaomba kwa kuwa fedha zipo kesho mradi huu ubadilishwe uanze kutumia nishati ya umeme ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wa gharama wananchi wa Kata ya Sakasaka. Lakini pia miradi ya Sakasaka na Lubiga ilishasimama kutoa huduma bila sababu za msingi.

Kuhusu ucheleweshaji katika kutoa huduma kwa wateja; kumekuwepo na ucheleweshaji wa kuunganisha wateja wapya siku nane hadi 408 kinyume na mkataba wa huduma kwa wateja inayohitaji muunganisho mpya wa maji kufanywa ndani ya siku saba tangu tarehe ya maombi. Hali hii inasababishwa na uhaba wa vifaa hasa mabomba na mita mpya za maji. Ucheleweshaji huu unachelewesha huduma kwa wananchi. Pia kuna ucheleweshaji wa kutatua malalamiko ya wateja ndani ya mamlaka ambayo inachukua siku nane mpaka 129 kinyume na mkataba ambao unataka ndani ya siku tano kutatua changamoto. Kwa nini kwa muda mrefu Wizara imeshindwa kuweka mfumo mzuri wa utatuzi wa changamoto hii?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**SPIKA:** Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Mtoa Hoja ajiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napeda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake kwangu na kwa upendeleo usiopimika kwa kunijaalia afya njema hadi kufikia siku ya leo. Pili, natumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini tena na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maji katika Wizara mbayo yeye ni muasisi wa kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani hii nitailipa kwa mambo yafuatayo, kwanza kwa kuchapa kazi; pili, kwa uadilifu na kwa unyenyekevu mkubwa na kwa maarifa yangu na akili yangu yote na nguvu zangu zote, na nitashauri na tutafanya maamuzi kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, Naibu Waziri Mkuu Dkt. Doto Mashaka Biteko pamoja

na Serikali nzima kwa usimamizi wao na kwa miongozo yao ya kutufanya sisi tufanye kazi ambayo inaenda kulenga maslahi ya Taifa. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati na Wabunge wote kwa kutuwezesha na kwa kutushauri na kwa kutupatia yale ambayo yanaenda kulenga kuimarisha sekta yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jumaa Hamidu Aweso; amekuwa ni kaka, kiongozi, mlezi na mtu ambaye hataki kutuacha nyuma wasaidizi wake. Mheshimiwa Waziri nakuahidi mimi siyo Waziri ni Naibu Waziri ambaye nimeletwa kwa ajili ya kukusaidia kazi pamoja na kwamba wewe una-*slogan* yako ya kusema kwamba; "Sote ni Mawaziri." Mimi ni Naibu Waziri nafahamu kimo changu na najua wajibu wangu wa kuhakikisha kwamba naenda kukusaidia kazi ili kuhakikisha kwamba tunafikia malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, dada yangu *Engineer* Mwajuma, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, pamoja na ma-*RM* wote, ma-*MD* wote na ma-*DM* wote, pamoja na madereva wetu na masekretari wote ambao wanatusaidia kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinaendelea kuwa rahisi zaidi katika kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kusahau wananchi wangu wa Jimbo la Bariadi ambao leo wamewakilishwa na Waheshimiwa Madiwani pale, nawashukuru sana kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano mzuri kwa kufanya kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisahau kumshukuru sana mke wangu kipenzi, Grace Kundo, naona leo yuko hapa, nakushukuru sana mke wangu kwa kuendelea kuwa msaidizi mzuri na kunifanya nitimize majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, natoa pongezi hizi kwa sababu ni Rais mwenye maono na ajenda, ni Rais ambaye ana nia ya dhati ya kuwatumikia Watanzania, ni Rais ambaye ana maamuzi na kusimamia anachokiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais alibeba ajenda yake ya kumtua mama ndoo kichwani na ajenda hiyo ndiyo iliyosababisha kuleta msukumo kuja kupitia Sheria ya Huduma za Maji ambayo ndiyo ilipelekea kuhakikisha kwamba tunakuwa na *RUWASA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kile *RUWASA* haikuwepo, lakini vilevile upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa ni asilimia 64. Sasa leo hii tunapoongelea, tunaongea kwamba kuna vijiji takribani 9,737 vimepata maji kati ya vijiji 12,318. Haya ni mafanikio makubwa sana ambayo ni sawasawa na asilimia 79.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuhakikisha kwamba miradi yetu inakamilika na kati ya miradi ambayo *RUWASA* iliikuta ilikuwa imesimama, kati ya miradi 177, mpaka sasa kwa usimamizi madhubuti wa Waziri wetu Mheshimiwa Jumaa Aweso na watendaji wa Wizara, tayari miradi 164 imeshakwamuliwa na tayari inafanya kazi. Haya ni mapinduzi makubwa sana katika sekta ya maji. Tunapopima matokeo, tunatazama tumetoka wapi, tuko wapi na tunaelekea wapi. Hapa tunapoongea mpaka sasa tunaona kabisa kwamba pamoja na kwamba changamoto bado zipo, lakini tunaamini kabisa uelekeo wa Serikali yetu ni sahihi kwa ajili ya Watanzania kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua, maji ni usalama, maji ni kilimo, maji ni mifugo, maji ni siasa na maji ni uchumi. Kwa kuzingatia hayo, sisi Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa Watanzania kupata maji safi na salama kwani tunaamini kwamba kwa kuwapatia maji safi na salama wataendelea kuwa na usalama, kufanya kilimo, mifugo na uvuvi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ambalo nataka nitoe ufafanuzi kidogo, nalo ni kuhusu visima 900 ambavyo Mheshimiwa Waziri alivitaja katika hotuba yake ya jana. Visima hivi vina kazi tatu, kazi ya kwanza ni kujenga tenki, kazi ya pili ni kusambaza mabomba na kazi ya tatu ni kuhakikisha kwamba tunafikisha mtandao wa maji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Wabunge na Watanzania kwa ujumla, sisi Wizara ya Maji tumejipanga, miradi hii itakamilika ndani ya miezi sita kuanzia hapa tunapoongea n ani kwa sababu fedha zipo na Serikali tumejipanga, uwezo huo tunao, maarifa hayo tunayo na nia ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata hayo maji, tunayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, wanaporudi katika majimbo yao, wakatusaidie kubainisha maeneo ambayo wanajua kwamba ni kipaumbele katika siasa zao na sisi tutakuja kuhakikisha kwamba tunaweka visima na maji yanatoka katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala la malipo ya kabla ya matumizi *(pre-paid water meters)*. Haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, sisi Wizara ya Maji tunayapokea na kwenda kuyatekeleza, hatutayajadili, lakini tunashukuru sana kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa sababu imelenga katika kuimarisha mambo ambayo yatakuwa yanajitokeza. Kwa kuweka *pre-paid water meters*, tunaenda kutatua matatizo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni matumizi mabaya ya maji; kwa kutumia *meter* ambazo tunazo sasa ambazo ni *mechanical meters* zinasababisha upotevu wa maji na kadhalika. Sasa tunaenda kutumia *smart pre-paid meters* ambazo zitatusaidia kuhakikisha kwamba matumizi mabaya ya maji tunaenda kuyadhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, malalamiko ya wananchi ya kubambikiwa bili; Mheshimiwa Rais aliongea, sisi tunalichukua kwenda kuhakikisha kwamba hakutakuwa na Mtanzania, baada

ya kuweka *pre-paid meters* ambaye atalalamika kwamba amebambikiwa bili ya maji ambayo haiendani na uhalisia wa matumizi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni malimbikizo ya madeni; na hapa Waheshimiwa Wabunge wameongelea hata taasisi za Serikali zipo. Ni kweli kabisa tunakiri na changamoto hiyo tunaifahamu. Kama Mheshimiwa Waziri anavyosema, hakuna *striker* anayeogopa beki, hiyo ni changamoto na sisi tunaichukua na kwa kutumia *pre-paid water meters* hatutakuwa na mgogoro na taasisi yoyote ya Serikali kwa sababu kila mtu atakuwa anajipimia kile ambacho anataka kukitumia, kwa hiyo tunaenda kutatua hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni wananchi kulalamika kutoshirikishwa katika usomaji wa mita. Tukishaweka *pre-paid meters* hatutahitaji mtu yeyote aranderande katika familia za watu kwa ajili ya kusoma mita. Huu ni mwarobaini na suluhisho la mambo yote haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika *human resource management*, tukishaweka *pre-paid meters* hawa watu ambao walikuwa wanaenda kusoma mita tutawapeleka katika majukumu mengine na kuhakikisha kwamba wanaenda kuleta tija katika maeneo mengine ambayo tutawapangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo tutatatua kwa ku-*install pre-paid meters* ni jambo la upotevu wa maji. Katika upotevu wa maji kuna mambo mengi, kuna mambo ambayo yanatokana na *mechanical installment* na mambo ambayo tumesema kwamba ni maji yamepotea, lakini hayajawa *charged*. Maana yake ni kwamba kuna taasisi imetumia maji, lakini hatujawa-*charge*, hayo yote tunahesabu kama upotevu wa maji.

Kwa hiyo, unaweza kukuta kwamba sehemu nyingine unaambiwa upotevu wa maji ni asilimia 45 unafikiri ni yale ambayo yanavuja peke yake, hapana. Kuna maeneo mengine ambayo tunatoa maji kama huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaamini kwamba, bajeti hii inapopita inaenda kwanza kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais za kuendelea kumtua mama ndoo kichwani, lakini kumpatia maji safi na salama, na vilevile tutaendelea kwenda kulinda vyanzo vyetu vya maji. Sambamba na hayo tunaenda kutengeneza mipango mikakati ambayo inaenda kutusaidia kwenda ku-*manage* mafuriko yaani maji mengi, lakini vilevile kujiandaa na kipindi ambacho kutakuwa na ukame, tutatoa wapi maji?*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba sasa haya maji mengi tunayatengenezea utaratibu wakati tukiwa na maji kidogo ili Watanzania wasiwe na upungufu wa maji yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba…

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, gurudumu ndio linaanza kutembea na gari ndiyo linatiwa petroli sasa, na ndiyo tunaanza kufanya kazi. Sisi Wizara ya Maji, nikimsaidia Mheshimiwa Waziri, nimeletwa hapa kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri, na…

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo tumesema kwamba visima hivyo 900 lazima vikamilike ndani ya miezi sita. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba na Waheshimiwa Wabunge wakubali kupitisha bajeti yetu ili tukaanze utekelezaji mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji, aje ahitimishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, moyo usiokuwa na shukrani hukausha yaliyo mema yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nikushukuru wewe binafsi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya kwa kuweza kuisimamia bajeti yetu tangu jana na leo na tumepata michango mingi, zaidi ya 60, ya Waheshimiwa Wabunge. Tunakushukuru sana na Mwenyezi Mungu akufanyie wepesi sana katika majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Kiswaga, kipenzi cha Wana-Kalenga, Makamu Mwenyekiti wetu wa Kamati Mama Anna Lupembe na Wajumbe wa Kamati yetu, kwa kazi kubwa na nzuri ya kuishauri Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya na pongezi zote ambazo zimetolewa ni kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na Kamati yetu, Kamati yetu ipewe maua mengi sana, ahsanteni sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, mmetupa pongezi nyingi sana hasa juu ya utekelezaji wa miradi ya maji na mmeonesha sekta ilipotoka, ilipo na wapi inapoenda, ahsanteni sana, lakini pongezi zote ambazo mmetupatia sisi Wizara ya Maji pamoja na mimi Waziri wa Maji zote zimwendee Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi zote ambazo mmetupa sisi viongozi wa Wizara hii ya Maji, ziende kwa watendaji wetu wote wa Wizara yetu ya Maji. Kwa kweli wamekubali kufanya kazi na kazi yenye kuonekana na nataka niwaahidi watendaji wote wa Wizara ya Maji, mimi pamoja na Naibu wangu, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Kundo, hatutakuwa kikwazo na tutatoa mazingira rafiki kabisa kuhakikisha kwamba mnatimiza majukumu yenu na kuhakikisha dhamira ya kumtua mwanamama ndoo kichwani ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, inatimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu, nimpongeze sana Naibu Waziri, *Engineer* Kundo. *Engineer* Kundo ameingia ndani ya Wizara ya Maji kwa muda mfupi sana, lakini amekuwa msaada mkubwa sana katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mimi ninakushukuru sana na tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba tunafanya kazi usiku na mchana, dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, iweze kutekelezeka. Leo umepata bahati ya kuja na mkeo yuko pale juu, nataka kumwambia shemeji yangu, ana mume bora, ana mume kiongozi. Nimwombe sana aendelea kumpa utulivu katika kuhakikisha kwamba mambo yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mdogo wangu huyu Kundo nimemzidi kidogo, mimi nimeona nijipe wawili, ndiyo maana unaniona kabisa nina kiaraza. Kwa namna ya kipekee niishukuru sana familia yangu, wake zangu wapendwa kabisa, namuona pale mke wangu mpendwa Kauthar Francis Tarimo, lakini pia Zainab Abdallah Issa, mimi nikiwaona hawa, roho yangu baridiii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nitumie nafasi hii kwa dhati ya moyo kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara yetu ya Maji, *Engineer* Mwajuma, Naibu Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Maji, mama Meena, mama mchungaji. Kwa kweli tumefanya *coordination* nzuri na yale ambayo tumelenga kuhakikisha kwamba tunayakamilisha, nataka niwahakikishie Waheshimiwa

Wabunge, mmezungumza suala la miradi tuliyoianza, twende tukaikamilishe, hicho ndiyo kipaumbele chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge baada ya kutupitishia bajeti yetu, tumejipanga vizuri kuhakikisha miradi yote ambayo tumeianza tunakwenda kuikamilisha ili Watanzania waishio mijini na vijijini wapate huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, kila kwenye mafanikio hapakosi changamoto, bajeti yetu tulivyoisoma utekelezaji wake ni asilimia 84 na utekelezaji wa miradi ya maji unategemea fedha. Kwa kweli kwa dhati ya moyo, nimpongeze na kumshukuru Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa kutupatia fedha Wizara yetu ya Maji na kuhakikisha hii asilimia 84 inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ambayo tumeyapata ndiyo yamezungumzwa hapa madai juu ya wakandarasi. Baada ya maelezo haya na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tumekaa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ametupa *commitment* na hivi ninavyozungumza, Katibu Mkuu wangu wa Wizara ya Maji amenieleza kuwa tumepatiwa shilingi bilioni 68. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, shilingi bilioni 68, twende tukawalipe wakandarasi wetu ili huko katika maeneo ya *site* kuende kuchangamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana wakandarasi, mmewasikia Waheshimiwa Wabunge namna walivyowapigania, mmesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge namna wanavyowatetea, niwaombe sana, fedha hizi tumezipata na nataka nimwelekeze Katibu Mkuu wa Wizara yetu ya Maji, baada ya kuzipata fedha hizi ziende zikawalipe kwa wakati na wahandisi wa maji mikoani na wilayani msilete visingizio vya aina yoyote. Maadam fedha zinapofika mkoani au wilayani wakandarasi wakalipwe fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake wakati mwingine fedha zinaweza zikafika zikaanza visingizio, hapana twende tukafanye tathmini, inakuwaje tathmini, mpaka ume-*rise certificate* mbona ulishafanya uhakiki? Kwa hiyo, muondoe visingizio, wakandarasi wakalipwe fedha zao. Niwaombe sana wakandarasi, fedha hizi ambazo mnaenda kupewa, nendeni mkafanye kazi. Tutaendelea kuwa marafiki kwa wale ambao wanafanya kazi, lakini kwa wale ambao hawatakuwa wafanyaji kazi tutaendelea kushughulikiana kuhakikisha dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wetu ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inatimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna mambo mbalimbali yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Jambo moja ambalo nataka nilisisitize kwa Waheshimiwa Wabunge ni rasilimali za maji ni usalama wa Taifa. Unapokuwa na maji toshelevu, una uhakika wa chakula, unapokuwa na maji toshelevu una uhakika wa nishati ya umeme, unapokuwa na rasilimali toshelevu maana yake una usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, rasilimali za maji tulizokuwa nazo juu ya ardhi na chini ya ardhi ni mita za ujazo 126,000,000,000; mita za ujazo 105,000,000,000 ni maji yaliyokuwa juu ya ardhi na mita za ujazo 21,000,000,000 ni maji yaliyokuwa chini ya ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi, miaka ya nyuma tulikuwa na mito, chemchem lakini kadiri tunavyokwenda leo chemchem zile hazipo na kuna baadhi ya mito imekauka na mingine imepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, tumefanya mabadiliko ya sheria kupitia Bunge lako Tukufu, suala la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji lazima tukubaliane tulinde kwa pamoja. Suala la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji lazima tulipe kipaumbele kama Taifa na haya yaliyotokea lazima yawe mafunzo. Mwaka juzi tuliona Mto Ruvu, Dar es Salaam ulikauka kabisa, ukienda Maswa tulikuwa na Bwawa *New Sola* lilikauka kabisa. Haya yaliyotokea lazima yawe mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana na watendaji wetu na sisi kama Wizara tumeshafanya mabadiliko hasa juu ya utendaji kwa mabonde yetu na hapa kauli ambayo tumeiweka ni moja tu, jamii ipo, ukiishirikisha utafanikiwa, usipoishirikisha utakwama. *(Makofi)*

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, sauti yenu ni kubwa twende tukashirikiane juu ya ulindaji na utunzaji wa rasilimali zetu za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala la mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yapo na mifano yake iko wazi kabisa. Mabadiliko ya tabianchi yana mambo mawili, mabadiliko ya tabianchi yanaleta mafuriko na mabadiliko ya tabianchi yanaleta ukame. Tumeshuhudia ukame ambao umetokea hapa nchini, tumeshuhudia mafuriko ambayo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna jitihada kubwa ambayo tumeifanya juu ya ujenzi wa miradi ya maji, lakini ni lazima tuongeze jitihada katika upande wa uchimbaji wa mabwawa. Uchimbaji wa mabwawa siyo kwa Wizara yetu ya Maji peke yake, tufanye kazi hii kwa mipango na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwa maana ya kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara nyingine za kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia mafuriko yanavyoharibu miundombinu ya barabara, tunashuhudia mafuriko yanavyoleta athari mbalimbali, tunaona mipango ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan tuwe na kilimo cha umwagiliaji.

Waheshimiwa Wabunge, ninachotaka kusema tumepata bahati katika Taifa letu zinanyesha katika vipindi viwili. Badala ya kuleta maafa lazima tutengeneze mazingira, mvua iwe fursa kwa kubadilisha uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uelekeo wa Wizara yetu ya Maji ni kuhakikisha tunajenga mabwawa ya kimkakati na hapa

kwa dhati ya moyo nimshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uthubutu wake juu ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, Bunge lilikuwa linatoa maamuzi ya kila mwaka juu ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uthubutu, leo tunajenga Bwawa la Kidunda, amefanya uthubutu na hivi karibuni tunampata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa, Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ni uelekeo sahihi kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji na kuhakikisha tunakuwa na uvunaji wa maji ya uhakika na kuwa na vyanzo mbadala katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Wizara ya Maji tukubali kubadilika, lazima Wizara ya Maji tuone namna sasa ya kuwa na vyanzo vya fedha vya kimbadala. Tukisema tutegemee fedha kwenye chanzo kimoja, malalamiko yataendelea kuwepo. Bunge lako lilishawahi kutushauri, sisi Wizara ya Maji tunaona namna gani Serikali ilivyo-*invest* pesa nyingi katika baadhi ya taasisi zetu. Leo ukienda *DAWASA*, *investment* kubwa imefanywa na Serikali, ukienda Arusha, zaidi ya shilingi bilioni 520 Serikali ime-*invest* pale, ukienda zako Tabora, zaidi ya shilingi bilioni 600 naa, Serikali ime-*invest* pesa pale, kwa hiyo maeneo mbalimbali ya Mamlaka zetu za Maji zimewekezwa fedha. Wakati mwingine ni aibu kwa Taasisi ama Mamlaka ya Maji inaomba shilingi milioni mia tatu, milioni mia tano kwa ajili ya kwenda kusambaza maji katika kata eti haina maji. Sisi kama Wizara ya Maji tumeona haja ya kubadili uelekeo wa fikra zetu, tumeona haja ya kutafuta vyanzo vingine mbadala ya fedha. Tumeanza Hati Fungani eneo la Tanga, eneo la Tanga wanataka kuhakikisha wanafika asilimia 100 ya upatikanaji wa maji, lakini walikuwa wanahitaji fedha shilingi bilioni 53 tukasema lazima tubadili fikra zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameenda kuanzisha Hati Fungani badala ya kupata shilingi bilioni 53, naomba kukupa taarifa kuwa wamepata shilingi bilioni 54, naendelea kuwapongeza sana *Tanga UWASA*, nimemuona Mwenyekiti wa Bodi ya *Tanga UWASA*, hongereni sana na huu ndiyo uelekeo wa Wizara yetu kupitia mamlaka zetu kuhakikisha kwamba tunawekeza katika Hati Fungani, tunapata fedha mbadala na chanzo mbadala ili suala la kuhakikisha kwamba dhamira ambayo tumeiweka na hatuwezi kuchelewa kuhakikisha kwamba miradi inatekelezwa kwa wakati na fedha zipo ili kuhakikisha kwamba miradi haikwami na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo lingine la kuhakikisha kwamba tunapata fedha, ni kuhakikisha kwamba tunaandika maandiko. Pamoja na maandiko pia kuhamasisha na kuongeza mahusiano zaidi. Hivi karibuni tumeanza ziara nje ya nchi kupitia wadau wetu mbalimbali, tulikwenda katika Shirika la Fedha pale Ufaransa *(AfD)*, baada ya kuzungumza na kuonyesha maandiko yetu, wametupa *Euro* milioni 70 kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza miradi yetu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee narudia tena, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ushirikiano unaotupa, wewe pamoja na Naibu wako na kutupa uelekeo sahihi wa kuhakikisha Wizara ya Maji inakuwa na *alternative source* ya vyanzo vya mapato ili kuhakikisha kwamba miradi yetu haikwami na kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri zaidi katika kuhakikisha tunamtua mwanamama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la vitendea kazi. Wizara inaendelea kuwapatia vitendea kazi wataalamu wetu katika mikoa na wilaya kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Wizara ya Maji imenunua magari 114 ambapo magari 76 yamekwishapokelewa na kusambazwa kwa Mameneja wa Mikoa na Wilaya. Aidha, jumla ya magari 37 yanatarajiwa kupokelewa hivi karibuni na yatasambazwa katika mikoa na wilaya ambazo zina mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, tumefanya tathmini baadhi ya maeneo kwa maana mameneja wetu wa mkoa ambao hawana magari pamoja na wa wilaya. Magari haya 37 ambayo tumeyapata, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tutawapa maeneo ambayo yenye uhitaji kuhakikisha kwamba wanakuwa na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, Wizara yetu ya Maji haina umaskini wa vyanzo vya maji. Ukienda Ruvuma tuna Ziwa Nyasa, ukienda Katavi, ukienda Rukwa, ukienda Kigoma kuna Ziwa Tanganyika, lakini ukienda Mwanza, ukienda Simiyu, ukienda Bukoba, Mara, tuna Ziwa Victoria, ukienda zako Ruvuma na maeneo ya Mtwara, tuna Mto Ruvuma, lakini ukija hapa Rufiji tuna Mto Rufiji, maji mengi yanamwagika baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maamuzi na maelekezo ya rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Maji itumie rasilimali toshelevu kuhakikisha kwamba tunatatua matatizo ya maji kwa Watanzania. Maelekezo ya Kamati ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *National Grid* na ndiyo maelekezo ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata katika hotuba yangu, tumesema tupo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kumpata mtaalamu mshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira yetu ni kuhakikisha maji yale sasa ya Ziwa Tanganyika, tunayatoa Ziwa Tanganyika tunayapeleka Katavi, tunayatoa Ziwa Tanganyika yanaenda Rukwa, tunayatoa Ziwa Tanganyika tunayapeleka mpaka Kigoma. Hiyo kazi sisi tunaiweza na tumekwishaianza. Uwekezaji wa miundombinu mikubwa ya aina hii inahitaji Taifa lenye uthubutu na Taifa hilo ni Tanzania chini ya Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweza kuyatoa maji ya Ziwa Victoria tumeyapeleka Tabora, tumeyapeleka Igunga, tumeyapeleka Nzega na sasa hivi yameshafika mpaka katika Jimbo la kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu pale Iramba. Sasa mkakati wetu ni kuhakikisha maji yale ya Ziwa Victoria yanafika katika Jiji la Dodoma kupitia katika Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia maelekezo ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sasa hivi tunafanya mapitio ambayo mradi ambao tulitaka tuuandae wa kuyatoa maji ya Ruvuma na kuhakikisha yanafika katika Mkoa wa Mtwara. Nataka kuwapa taarifa ndugu zangu Wana-Mtwara, maelekezo ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kwenda kuyachukua maji ya Mto Ruvuma na kuhakikisha kwamba tunayapeleka katika eneo la Mtwara Wana-Mtwara waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ulishawahi kuielekeza kwamba maji sasa hivi tumejenga bwawa kubwa la Mwalimu Nyerere. Maji yale yanatumika kwa ajili ya bwawa lakini mengine yanapotea baharini. Maelekezo ambayo umetupatia ni kuhakikisha kwamba yale maji tunayavuna na yanaweza kutumika kwa ajili ya Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo maelekezo, tunakwenda kumtafuta mtaalamu mshauri kuhakikisha maji yale sasa tunakwenda kuyatumia na kuhakikisha kwamba yanakuwa na faida kwa Wana-Dar es Salaam, yanakuwa na faida kwa Wana-Lindi kuhakikisha kwamba tunakwenda kumtoa mwanamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wetu mwingine, tunajua kabisa kuna maeneo kwa maana ya Tunduma, tuna maeneo kwa maana ya Momba, yamekuwa na changamoto kubwa sana ya maji. Tunakwenda kutumia maji toshelevu ya Mto Momba kuhakikisha Wana-Tunduma, Wana-Momba, Wana-Vwawa, Wana-Mbozi, kuhakikisha kwamba wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama. Lakini tunatambua kwa eneo la Dar es Salaam tumeshafanya kazi kubwa katika maeneo mbalimbali, tunahitaji maji kupeleka eneo la Segerea, lakini tunahitaji maji kwa ajili ya kupeleka eneo la Kibamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mtemvu, tumejipanga, tunasema wali wa kushiba unaoekana kwenye sahani, siyo kushiba tu, sasa hivi tunakwenda mpaka

kusaza. Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kuzungumza kwa Waheshimiwa Wabunge, *National Grid* ndiyo uelekeo wa Wizara yetu ya Maji. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaomba tuendelee kushirikiana, kuhakikisha kwamba hili suala tunakwenda nalo vizuri ili mambo yetu yaweze kuhakikisha kwamba dhamira ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inatimilizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ambazo amezifanya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan juu ya ujenzi wa miradi ya maji, lakini pia uthubutu wa kuhakikisha kwamba anakwamua miradi mbalimbali ambayo ilikwama kwa muda mrefu, tulikuwa na Mradi wa Ng'apa pale Lindi ambao ulikwama kwa muda mrefu, tulikuwa na miradi Kigoma ambayo ilikwama kwa muda mrefu, tulikuwa na Mradi wa Nyabehu pale Bunda, ulikwama kwa muda mrefu, tulikuwa na Mradi wa Same – Mwanga ambao ni mradi ulikuwa ni mfupa mgumu, leo wameugeuza biskuti, mradi tunakwenda kuukamilisha Watanzania waende kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo ninataka kusisitiza, uelekeo wetu wa Wizara ya Maji ni kwenda kuboresha huduma kwa wateja, huo ndiyo uelekeo wetu. Tumeshuhudia sasa hivi, leo mwananchi anataka kuunganishiwa maji, ameshalipia kwa ajili ya maunganisho, wakati mwingine mamlaka inatumia miezi mitatu, miezi minne, miezi mitano mwananchi hajaunganishiwa maji, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini unaona wakati mwingine unapita ziara Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye Mamlaka ya Maji anakwambia Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji, upotevu wa maji hapa asilimia 50, hatuwezi kukubali. Mtu anapokwambia amepoteza maji asilimia 54, maana yake unapofanya ziara katika mitaa, unategemea kuwepo na mabwawa kwa upotevu mkubwa, lakini huyaoni.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kuna baadhi ya viwanda, kuna baadhi ya hoteli kubwa, zimeunganishiwa maji kinyemela, halafu huku katika wateja hawaonekani. Kwa hiyo, nataka kuwaambia Wakurugenzi wa Mamlaka zetu za Maji, kipimo cha kuwepo kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji ni kuhakikisha unahakikisha kwamba upotevu wa maji haupo katika mamlaka yako ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni suala unaliona kabisa, mwananchi wa kawaida anapita mtaani, anaona maji yanapotea, anatoa taarifa, hakuna mtu anayemjibu. Zimetolewa namba za huduma kwa wateja, mwananchi anapiga simu kwa ajili ya kutatuliwa changamoto yake, hajibiwi, anatuma *message* kwa Mheshimiwa Waziri, anatuma meseji kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ukituma, hata kama ilikuwa saa tano usiku, watendaji wanaondoka huo huo usiku wanaenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia watendaji wa Wizara ya Maji, kazi ambayo nimeifanya kwa kipindi kichopita ilikuwa ni ujenzi wa matenki, sasa hivi tunakwenda vizuri, lakini sasa hivi nguvu ambayo tutaelekeza, ni kuhakikisha tunaweka nguvu katika *service delivery* (huduma kwa wateja), tutapima kazi katika huduma kwa wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini leo mteja akutumie *message,* usifanye kazi? Kwa nini utumiwe *message* na Waziri ndiyo unafanya kazi? Nguvu na uwajibikaji ambao unaufanya unapopewa maelekezo na Waziri ama Naibu Waziri, ndiyo iende ukaifanye vilevile kwa wateja wetu kwa sababu mteja, ndiye mfalme wetu, ndiye anayewezesha mamlaka yetu kuhakikisha kwamba inakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana pia nimeeleza juu ya watendaji wetu wakati mwingine kufanya kazi bila utoaji taarifa. Wakati mwingine inaweza ikatokea hitilafu, labda mnataka kufanya marekebisho *pump* imeharibika, kwa nini hamtoi taarifa kwa wananchi. Kwa hiyo, hayo ndiyo mambo ambayo tunataka kwenda kuyasimamia na kuyafanyia marekebisho makubwa katika Wizara yetu ili ufanisi uende kuwa mkubwa ili Wana-

Tanzania waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo lingine, naendelea kulielekeza, ni marufuku kwa Wakurugenzi wa Mamlaka zetu za Maji, kumkatia mwananchi maji siku ya *weekend* au siku ya sikukuu, inakuwa ni usumbufu ambao hauna ulazima wowote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maelekezo yapo kisheria ambayo yameainishwa katika Haki za Mteja katika *EWURA*, kwa hiyo, ni marufuku kwa mteja wetu ama ni marufuku kwa mwananchi, kwa Mamlaka zetu za Maji kuhakikisha kwamba unamkatia maji *either* iwe *weekend* au iwe katika kipindi cha sikukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee ambayo nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, miaka ya nyuma Wizara yetu ya Maji ilikuwa Wizara ya kero na lawama. Moja ya changamoto kubwa ya Wizara yetu ya Maji ilikuwa ufinyu wa bajeti. Ipo miradi ambayo imejengwa tangu mwaka 1970 haijawahi kukamilishwa, amekuja kuikamilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Maji tulikuwa tukija katika Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakizungumzia suala la miradi kichefuchefu.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwaambia, mmefanya mageuzi makubwa, mmefanya mapinduzi makubwa katika sekta yetu ya maji, mwaka juzi Wizara hii ya Maji, tulikuwa na Mwenge wa Uhuru ndiyo Wizara imetangazwa namba moja kwa kufanya vizuri katika miradi yetu ya maji. Mwaka jana tulikuwa na miradi zaidi ya 100, hakuna hata mradi mmoja uliokwama, tulipiga *clean sheet*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nilikukabidhi barua hapo kupitia *World Bank*, Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)*, ndiyo Wizara ambayo inaongoza kwa miaka miwili mfululizo, zaidi ya nchi 40 ambazo zilishindanishwa na *World Bank*,

sisi Wizara ya Maji kupitia *RUWASA* ndiyo inaongoza. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Bunge lako Tukufu, hii ni kazi kubwa ambayo umeifanya Mheshimiwa Spika, hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, Rais aina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hapatikani kila mahali, Rais aina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila wakati, Rais aina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumempata lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania. Itoshe kusema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni suluhu ya matatizo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na 90% ya upatikanaji wa maji mijini, pamoja na 79.6% vijijini, ametupa maelekezo Wizara ya Maji, amesema tufanye tathmini, tuna vijiji vingapi Tanzania, tumemwambia tuna vijiji 12,318, mmefika vijiji vingapi, tumemwambia vijiji 9,737; vimebaki vijiji vingapi, amesema ukiachana na asilimia, nataka wananchi wangu wote vijijini wapate huduma ya maji safi na salama. Ametupa vijiji 900 na ameelekeza kila Mbunge awe na vijiji vitano/vitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna vijiji 2,581, maana yake kwa *phase one* tunakwenda vijiji 900, tukienda *phase two* vijiji 900, *phase three* maana yake vijiji vyote vitakuwa na huduma ya maji safi na salama na hii ndiyo kazi na *legacy* ambayo itakuwa imefanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naendelea kukushukuru kwa kazi kubwa na nzuri unayoifanya na nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa, mmefanya kazi nzuri, tunaomba mtupitishie bajeti yetu, lakini kubwa nawaomba watendaji wetu wa Wizara ya Maji, tunakwenda kupitisha bajeti, mnapokwenda mkoani, nendeni mkatoe taarifa kwa wadau wa maendeleo, mmepangiwa nini,

wajue nini na katika wilaya ili tuweze kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani na viongozi waweze kujua miradi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine Waheshimiwa Wabunge, mmeendelea kufanya kazi kubwa, nawaomba, ni muda wenu muafaka wa kwenda kuzindua miradi ya maji ili ibaki kumbukumbu kwamba kwa kazi hizi kubwa ambazo mmezifanya, ninyi ndiyo mnaifanya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa kabla hatujaendelea, nawatangaza wageni walioko hapa Bungeni.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Maji, hawa ni Makatibu Uhamasishaji Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi Wilaya za Kanda ya Kaskazini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapoa pia Wakandarasi wa Wizara ya Maji, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 55 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Waziri wa Madini ambao ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Kata ya Ipagala Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 36 wa Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati ambao ni *Youth Leadership Forum* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Samwel Katamba ambaye pia ni Meneja wa Kukabiliana na Majanga *Red Cross*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Zaytun Swai, *club* ya *Green Awareness* inayojihusisha na uelimishaji na uhamasishaji jamii kutunza misitu na mazingira, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 43 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia walimu 36 wa Shule ya Sekondari Mzumbe kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*……….......................…….Sh. 4,716,820,988

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri na kuna Waheshimiwa Wabunge wawili hapa wanataka ufafanuzi wa mambo ya kisera.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi mchana wa leo. Kauli ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua ndoo mwanamke kichwani, ni kauli yenye faraja na matumaini makubwa sana kwa wanawake wa Tanzania hususan kwa wanawake wa vijijini ambao wanatumia mwendo mrefu sana kwa ajili ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa michango ambayo Wabunge wamechangia katika Bunge hili, ni dhahiri kabisa kuonesha ziko pesa nyingi sana za miradi ya maendeleo ya maji ambazo zimeshuka kule chini kwa ajili ya lengo la kutimiza kauli njema ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kupata ufafanuzi wa kina na *commitment* kwa Mheshimiwa Waziri kwenye Bunge lako hili kwamba pamoja na pesa nyingi ambazo zimeshuka huko chini, mabilioni ya pesa, kwa kupitia jicho letu la Bunge *CAG*, katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika uendeshaji wa matengenezo ya miradi ya maji na kwa kuzingatia miradi ya maji ambayo tulienda kuitembelea nilipokuwa na Kamati yangu ya Hesabu za Serikali *(PAC),* kunaonesha dhahiri kwamba miradi mingi ambayo tumepeleka bilioni nyingi za pesa kule, wakati mwingine ina changamoto, pesa ile haifanyi kazi kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo inafanya sisi majimbo mengine ambayo bado hatujafikisha hiyo asilimia kucheleweshwa kufikia hizo asilimia za upatikanaji wa maji kwa sababu pesa inapotengwa kama hii kidogo inalazimika kwanza ikamalizie miradi ya wenzetu ambayo imekwishaanza isiishie njiani. Sasa kutokana na muda sitaweza kuisoma taarifa hii ni ndefu sana lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imeshagonga, sekunde thelathini malizia hoja yako.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sekunde thelathini, nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi kwa kiasi ni kipi ambacho ataenda kufanya kuhakikisha pesa hizi ambazo tumempitishia leo atasimamia kikamilifu isipotee hata shilingi moja ili na sisi wengine ambao bado hatujafikia hiyo asilimia tuweze kupata maji kwa sababu tunapata kadhia, upoteaji wa pesa ambao unaendelea kuwepo kama *CAG* anavyosema umefanya na sisi tuendelee kuumia majimbo mengine pamoja na Jimbo la Momba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika kipindi ambacho nimekaa katika Wizara ya Maji nimejifunza sehemu ambapo kuna usimamizi mzuri basi kunakuwa na matokeo mazuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo la msingi ambalo sisi kama Wizara eneo tulililoliimarisha ni suala zima la *monitoring* ambalo siyo kwamba tutaweza kufanya peke yetu, tunawashirikisha Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya kuhakikisha wanasimamia, wanafuatilia, lakini pia kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge wanajua miradi yao na ndiyo maana hata hapa nilivyozungumza nimewataka watendaji wetu wa Wizara, tunapitishiwa bajeti wakawaeleze wadau wa maendeleo nini walichopangiwa ili waweze kujua na kuweza kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Wizara yetu ya Maji ilipotoka na sasa ni vitu viwili tofauti na ndiyo maana tumekuwa na taarifa hata hizo za *CAG* tumekuwa na hati safi lakini tumeona Mwenge wa Uhuru mwaka juzi tumekuwa namba moja juu ya ufanisi wa miradi, kwa mwaka jana hakuna mradi hata mmoja uliokwama lakini huu *World Bank* sisi ndiyo tunaongoza kidunia zaidi ya nchi 50.

Kwa hiyo kikubwa ambacho ninachotaka kukisema Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana juu ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maji ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi ningeomba nipate ufafanuzi na *commitment* ya Serikali, kwa sababu mwaka jana hapa waliahidi na alisimama Waziri wa Fedha kuhusiana na Taasisi za Serikali kutumia maji bila kulipa. Hili jambo ni kubwa, haiwezekani watu wakatumia maji yanafika shilingi bilioni 26 hawalipi bili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia changamoto hapa ya Wizara ya Maji, mbali na kupunguziwa bajeti, hii pesa ndiyo ingeweza kuanzisha miradi mingine kwenye hizi mamlaka zetu za maji, lakini hizi pesa ambazo Serikali wamezikalia zingeweza kuwasaidia mamlaka kujiendesha, vilevile zingeweza kuwasaidia kufanya marekebisho madogo madogo ya miundombinu ambayo yanaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nimesema hapa, leo shilingi bilioni 26. *DAWASA* peke yake wanadai shilingi bilioni 11 kwa taasisi za Serikali hii hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria JWTZ inadaiwa shilingi bilioni 12 Waziri yupo, Mheshimiwa Aweso atafanyaje kazi? Tutamtuaje mama ndoo kichwani? Magereza shilingi bilioni sita, Polisi shilingi bilioni tano, Serikali za Mitaa shilingi bilioni 1.5, Hospitali za Mikoa shilingi milioni 633, Ikulu Ndogo shilingi milioni 102 na Mifugo shilingi milioni 44. Sasa hizi hela zote mnazo, mwananchi wa kawaida kule akiwa na bili tu ya shilingi 50,000 anakatiwa maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sekunde thelathini, hoja yako ni ipi unayotaka ufafanuzi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *commitment* hapa, Waziri wa Fedha unanisikia wewe mwaka jana uliahidi Waziri wa Ulinzi yuko wapi? Waziri wa Mambo ya Ndani yuko wapi? Waziri wa Afya ananisikia pale dada yangu Ummy lipeni maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya, sasa ngoja. Ngoja unataka *commitment* kutoka kwa Waziri wa Fedha ama Waziri wa Maji?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri wa Maji ni Serikali kwa ujumla kwa sababu mwaka jana alisimama akajibu, akaji-*commit* kwamba hizo Taasisi za Serikali zitalipa.

**MWENYEKITI:** Sasa kama tunataka ya jumla ni ile ya baadaye Waziri wa Fedha atakapokuwa hapa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maji.

**MWENYEKITI:** Kama tunataka ya Waziri ya Maji…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo madeni yanalipwa lini ili Mamlaka za Maji huko ziweze kupata pesa zake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, sawa umeshaeleweka, umeshaeleweka.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na nisipopata majibu sahihi leo mwanangu nakamata shilingi yako nakwambia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hutoweza kuishika leo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kulikuwa na hoja moja hapa ya Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi, hoja ya Waraka kutoka *TRA* ukizungumzia mambo ya kilimo.

Sasa hii hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya inahusu malipo ya Taasisi za Serikali au vyombo vya Serikali kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji. Sasa anayetoa hiyo *commitment* hawezi kutoa yule anayedai kwa sababau huyu taasisi zake ndiyo zinazoidai Serikali, sasa yeye atatoaje *commitment?* Maana yake anajidai yeye mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hii hoja nayo ni moja wapo ambazo zinamsubiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini pia na Mawaziri kadhaa ambao taasisi zao zinadaiwa. Inapokuja hoja hapa Waheshimiwa Wabunge ya Wizara ambayo inadaiwa pesa huyo ndiyo tumuulize umeweka kwenye kifungu kipi madai yako ya maji? Madai yako ya kila maeneo wanakodai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo hii hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya, haitaenda kwa Waziri kwa sababu yeye ndiyo anayezidai taasisi za Serikali. Sasa tunaenda kupitisha bajeti kwa mafungu.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR– KATIBU MEZANI:**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 4,716,820,988
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,728,012,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*....................Sh. 2,000,453,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh. 799,411,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*................................Sh. 827,637,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*......Sh. 1,159,806,912
Kifungu 1007 - *Management Information System Unit*............................................Sh. 785,425,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 922,869,000
Kifungu 1009 - *Project Preparation, Coordination and Environmental Management Unit*.......Sh. 705,665,000
Kifungu 1011 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 955,445,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*................................Sh. 7,293,367,050
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*..............................Sh. 2,347,967,000
Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*.............................................Sh. 39,676,831,050
Kifungu 5001 - *Water Development and Management Institute*.......................Sh. 5,743,249,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................................Sh. 800,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 8,200,000,000
Kifungu 2001 – *Water Resources*..............................Sh. 37,224,452,332
Kifungu 2003 – *Water Laboratory*..............................Sh. 1,300,000,000
Kifungu 3001 – *Water Supply and Sanitation Division*..........................Sh.510,590,926,668

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutuoa Taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabuge, hoja imeungwa mkono. Baada ya hoja kuungwa mkono, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, baada ya kuwahoji nanyi kukubaliana na hoja hiyo basi nitumie fursa hii kusema rasmi kwamba sasa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/205 yamepitishwa rasmi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kadri ya taarifa yenu na ya Kamati lakini pia kwa zile ahadi ambazo mmezitoa hapa kwa mwaka ujao wa fedha na tunawatakia kila kheri katika utekelezaji wa hayo ambayo mmesema mnaenda kuyafanya.

Waheshimiwa Wabunge, namshukuru pia Mwenyekiti wetu wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati yetu ya Maji na Mazingira kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuisimamia Wizara hii na hatua zote ambazo wanazichukua, mnawapa mawazo mazuri na mnawasimamia vizuri.

Waheshimiwa Wabunge wote, mawazo yote mliyoyatoa tunawashukuru sana, naamini yatamsaidia Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake Naibu Waziri kufanya kazi vizuri zaidi katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mambo machache, kwa sababu ya yale ambayo yamejadiliwa hapa ndani na Waheshimiwa Wabunge na ili tuweze kuyaweka vizuri hii kazi inabidi wapewe Kamati yetu ya Bajeti waweze kuyatazama haya ambayo nitayasema hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, Kamati ya Bunge ilikuja na wazo na hapa pia Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza la kuongeza shilingi 50 kwa lita ya mafuta, lakini kabla ya kufikia kusema iongezeke hiyo shilingi 50 au hapana mijadala imeashiria kwamba Wizara ya Maji fedha haziendi zile ambazo zinatengwa, lakini pia zile ambazo zinatoka kwenye mfuko kama zinaenda basi kuna hoja ambayo imezungumzwa hapa ya kanuni ya ugawaji wa zile fedha. Kama sasa lazima Kamati yetu ilitazame vizuri tujue tatizo liko wapi? kabla hatujasema fedha *either* iongezeke kwenye mafuta ama isiongezeke? Kama tatizo ni hiyo kanuni ya ugawaji. Kamati iende ikalitazame vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kama ni fedha kutokwenda itakuwa haina uhusiano na kuongezeka shilingi hamsini ili fedha ziende kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa Waziri hapa ni kwamba ziko fedha nyingi ambazo zimekuja Wizarani na ziko tayari kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali, kwa hiyo, tutaipelekea Kamati yetu ikalitazame hilo.

Waheshimiwa Wabunge, hoja nyingine ambayo imezungumzwa hapa, namsikia Mbunge anasema *RUWASA, RUWASA* ndiyo inaingia kwenye kanuni ya ugawaji, kwa sababu mpaka sasa hivi inapewa ila haipewi kwa utaratibu ule ambao pengine inaweza kuleta tija zaidi kwa hiyo siyo kwamba haipo. Isipotajwa *RUWASA* ni kwamba himo kwenye kanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine lililozungumzwa hapa ni kuhusu kupunguzwa kwa bajeti ya Wizara ya Maji kwa jumla ya shilingi 137,714,253,000. Taarifa ya Kamati imeeleza hili na Wabunge wamelisema sana hapa, sasa tunalipeleka kwenye Kamati yetu ya Bajeti ili ikalitazame kwa sababu huenda zile fedha alizozieleza hapa Mheshimiwa Waziri kwamba zinatoka Benki ya Dunia, lakini pia na wadau wengine ambao

anawatafuta pengine inaleta hiyo fedha. Kwa hiyo, kuna sura ambayo pengine italetwa kwa njia ambayo inabidi huku ipungue. Sasa maelezo mazuri tutayapata tukitoa nafasi kwa Kamati kuweza kuhoji upande wa Serikali, halafu Bunge wakati huo sasa litaweza kufanya maamuzi kwa kutumia Kanuni yetu ya 124.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo haya niliyoyasema hapa Kamati ya Bajeti itaenda iyatazame, tusiwe na wasiwasi juu ya hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho nimefanya mabadiliko madogo ya ratiba yetu ya Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge. Kwa hiyo, itagawiwa kwenye vishikwambi vyenu, kwa hiyo upande wa Serikali utazame hiyo ratiba, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wanaojiandaa kwa ajili ya kuchangia waitazame ratiba hiyo, itakuwa imewekwa kwenye vishikwambi vyenu. Tumefanya mabadiliko madogo ya bajeti gani zitatangulia na zipi zitafuata baadaye kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niwashukuru sana kwa uvumilivu muda umeenda kidogo, lakini mmekaa kwa kutulia humu ndani, ninawashukuru sana.

Kwa kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 8.34 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*